

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Kumi – Tarehe 15 Aprili, 2019

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS
(MUUNGANO NA MAZINGIRA):-**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

NAIBU SPIKA: Ahsante, Katibu.

NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali, tutaanza na Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mheshimiwa Kiza Hussein Mayeye, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalii lake.

Na. 78

Malipo Stahiki Kwa Walimu Waliopanda Daraja

MHE. KIZA H. MAYEYE aliuliza:-

Serikali imekuwa ikiwapandisha madaraja walimu lakini haitoi malipo stahiki kwa madaraja hayo mapya kwa kipindi kirefu tangu walipopandishwa madaraja yao:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba walimu wanapata stahiki zao mara wanapopandishwa madaraja?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kiza Hussein Mayeye, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilisitisha kupandisha walimu na watumishi wengine madaraja katika mwaka wa fedha 2015/2016 na 2016/2017 kutokana na uhakiki wa watumishi uliohusisha uhalali wa vyeti, elimu na ngazi za mishahara. Lengo la uhakiki ilikuwa ni kuhakikisha kuwa Serikali inabaki na watumishi wenye sifa na wanaostahili kulipwa mishahara. Kutokana na sababu hiyo, ni kweli wapo watumishi ambao walipandishwa madaraja ambao hawajalipwa mishahara mipya, wapo waliopata mishahara mipya na baadaye kuondolewa na wapo ambao hawakupandishwa kabisa pamoja na kwamba walikuwa na sifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kurekebisha changamoto hizo, Serikali ilitoa maelekezo kuanzia Novemba, 2017 kwa

waajiri wote wakiwemo Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhuisha barua za kupandisha madaraja watumishi hao ili waweze kulipwa stahiki zao. Aidha, kwa wale ambao walikuwa na barua lakini taarifa zao zilikuwa hazijaingizwa kwenye mfumo, waajiri walielekezwa kuhuisha barua zao kuanzia tarehe 1 Aprili, 2018 ili waanze kulipwa stahiki zao. Serikali itaendelea kuweka kipaumbele na kutenga bajeti kwa ajili ya kuhakikisha watumishi wenye sifa na kupanda madaraja wanalipwa stahiki zao.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kiza Hussein Mayeye, swali la nyongeza.

MHE. KIZA H. MAYEYE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize maswali ya nyongeza. Nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri lakini naomba kuuliza maswali mawili, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, wapo walimu ambao mpaka wanastaifu walikuwa wako katika daraja jipya lakini mlipokuja ku-*calculate* mafao yao mka-*calculate* kwa kikokotoo cha mshahara wa zamani. Je, ni lini sasa Serikali mtaona umuhimu wa kuwalipa wastaifu hawa mapunjo yao ya mafao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, pesa ya likizo na matibabu kwa walimu hawa ni takwa la kisheria kwa mujibu wa sheria za kazi lakini walimu hawa wamekuwa wakienda likizo au kwenye matibabu pasipo kupewa pesa zao kwa wakati. Je, ni lini sasa Serikali mtaona umuhimu wa kuwalipa walimu hawa pesa kwa wakati mara wanapokwenda likizo au kutibiwa? Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Kiza maswali yake ya nyongeza mawili, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza Mheshimiwa Mbunge ametaka kujua wale waliolipwa mafao yao kwa kikokotoo cha zamani, naomba nitoe maelekezo kwa waajiri wao na Maafisa Utumishi kwenye Halmashauri zetu, twende *case by case* walifanyie kazi halafu sisi tutashauriana namna bora ya kulishughulikia ili kuondoa changamoto na malalamiko kwa watumishi hawa.

Swali la pili, ni nia ya Serikali kuendelea kulipa watumishi wake na kuwapandisha madaraja kwa wakati. Sasa hivi tumeshafanya *calculation* na tumejiridhisha kwamba tuna walimu zaidi 86,000 ambao wanaidai Serikali zaidi ya shilingi bilioni 43, tuna walimu wa sekondari zaidi ya 18,000 ambao wanadai karibu zaidi ya shilingi bilioni 18. Jumla ya madai ya walimu wote ya madaraja, likizo na malimbikizo mbalimbali kwa maana ya *areas* zao ni jumla ya zaidi ya shillingi bilioni moja. Kwa hiyo, Serikali imefanya utafiti na uhakiki sasa tunafanya mchakato wa kutafuta fedha ili walimu wetu waweze kulipwa madai yao na kupunguza malalamiko ambayo kwa kweli ni mengi sana. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata la Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora), Mheshimiwa Daniel Nicodemus Nsanzugwanko, Mbunge wa Kasulu Mjini sasa aulize swali lake.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako, naomba kwanza kuipongeza Serikali kwa kuzindua Mji wa Serikali Dodoma, hongereni sana. (*Makof*)

Na. 79

TAKUKURU Kuendesha Mashauri Mahakamani Moja kwa Moja

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO aliuliza:-

Tatizo la ujisadi na wizi nchini limeachwa likaendelea kwa muda mrefu sana:-

(a) Je, ni kwa nini TAKUKURU wasiachiwe kuendesha mashauri makubwa ya ufisadi na wizi Mahakamani moja kwa moja bila ya kuomba kibali cha *DPP*?

(b) Je, *DPP* amezuia majalada mangapi ya uchunguzi kufikishwa Mahakamani na ni kwa nini?

(c) Je, Serikali haioni kwamba *DPP* anaweza kutumika kulinda maslahi ya viongozi ambao kwa kiwango kikubwa wanajihuisha na vitendo vya wizi na ufisadi pamoja na matumizi mabaya ya madaraka?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora) majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora), napenda kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Nicodemus Nsanzugwanko, Mbunge wa Kasulu Mjini, lenye sehemu (a),(b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 57(1) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na.11 ya mwaka 2007, TAKUKURU wanayo mamlaka ya kufikisha watuhumiwa waliotenda makosa ya hongo kinyume na kifungu cha 15 cha Sheria Na.11 ya mwaka 2007 moja kwa moja Mahakamani bila kupitia kwa Mkurugenzi wa Mastaka (*DPP*). Makosa mengine yaliyosalia yanapaswa kupata kibali cha *DPP* kabla ya kupelekwa Mahakamani kama ilivyoelekezwa kwenye kifungu cha 57(1) cha Sheria Na.11 ya mwaka 2007.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 57(2) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na.11 ya mwaka 2007, *DPP* yanapaswa kutoa au kutotoa kibali kuwafikisha watuhumiwa Mahakamani ndani ya siku 60 tangu Jalada la Uchunguzi kumfikia. Hata hivyo,

DPP anapokea majalada ya uchunguzi kutoka vyombo mbalimbali vya uchunguzi vikiwemo TAKUKURU, Polisi, na Uhaniaji. Kwa siku *DPP* hupokea takribani majalada 10 kutoka TAKUKURU. Hivyo, kuna kila sababu *DPP* akaongezewa rasilimali watu na fedha ili aweze kutekeleza majukumu yake kwa wakati. Dhana ya kuwa *DPP* anazuia Majalada ya Uchunguzi yasifikishwe Mahakamani siyo sahihi.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba *DPP* ni Ofisi inayojitegemea na mamlaka yake yako kwa mujibu wa Katiba. Hata hivyo, sote tumeshuhudia kwamba viongozi mbalimbali wa Serikali wakiwemo Mawaziri wakifkishwa Mahakamani na kuhukumiwa kwenda jela. Naomba nitumie fursa hii kuwaasa watumishi na viongozi wote wa umma mkiwemo ninyi Waheshimiwa Wabunge kutojihusisha na vitendo vyovypote vile vya rushwa. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko swalilala nyongeza.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na maelezo mazuri ya Naibu Waziri, napenda niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, swalilangu la (b) linauliza ni kesi ngapi *DPP* amezuia majalada hayo ya watuhumiwa, ndio msingi wa swalilangu. Kwa maoni yangu swalilangu naomba ijibiwesasa kwa sababu halikujibowi katika maelezo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Halmashauri ya Mji wa Kasulu tulibibiwa fedha takribani shilingi bilioni 5.9 ingawa baadaye nasikia uhakiki ulibainisha kwamba takribani shilingi bilioni 2 zilitakuwa zimeibowiwa. Washtakiwa wale walismamishwa kazi, wakahojiwana TAKUKURU lakini cha ajabu ni kwamba watuhumiwa hawa hawajafkishwa Mahakamani eti kwa sababu *DPP* hajatoa kibali. Ni kitu gani hicho?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa kaka yangu Nsanzugwanko, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba nimpongeze sana kwa jinsi ambavyo anafuatilia sana masuala ya watumishi wa Jimbo lake la Kasulu amba wanategemewa kutoa huduma kwa wapiga kura wake amba pia ni wapiga kura wake. Jambo la kwanza, kwenye majibu yangu ya msingi hapa nimesema *DPP* ni Ofisi inayojitegemea na ipo kwa mujibu wa Katiba. Kwa maana hiyo, siyo kwanza amezuia isipokuwa majalada haya yamechelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swalii lake la pili, Kasulu siyo kwamba kulikuwa na ubadhifuru wa shilingi bilioni 5.9 bali ni ubadhifuru wa shilingi bilioni 1.6 na kulikuwa na kesi 12. Katika kesi hizo 12 aliyekuwa *DT* wa Halmashauri hiyo ya Kasulu anahusika kwenye hiyo kesi moja lakini kesi sita zenyewe zilifutwa kwa sababu zilikosa ushahidi na kesi tano zinasuasua kwa sababu kuna mashahidi wengine wanaogopa kutoa vielelezo. Kwa hiyo, naomba niliarifu Bunge lako Tukufu na kuwaasa Watanzania wote kwamba wawe na kiu ya kutoa ushirikiano na Taasisi yetu ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kwa sababu rushwa ni adui wa haki. Nakushukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongezee kidogo maelezo kwa kuelezea mamlaka ya *DPP* kwa mujibu wa Katiba ambapo ni lbara ya 59B(2) ambayo inampa Mkurugenzi wa Mashtaka uwezo wa kufungua, kuendesha na kusimamia mashtaka yote nchini. Kwa hiyo, ana mamlaka ya kufungua au kuendesha lakini

kama haendeshi anasimamia mashtaka yote yanayohusu makosa ya jinai nchini. Hata Ibara ndogo ya (3) inaeleza vizuri kwamba mamlaka hayo anaweza kuyatekeleza yeye mwenyewe au mtu mwingine kwa maelekezo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la *DPP* ama anazua au hazuui ma-file kwenda kwenye mashtaka, Mheshimiwa *DPP* hazuui bali anatoa kibali au hatoi kibali. Pia hafanyi hivihivi, anachopaswa kufanya *DPP* kwa sababu yeye siyo Mamlaka ya Uchunguzi bali ni mamlaka ya mashtaka, kwa hiyo ni lazima apime ushahidi ulioletwa kutoka kwenye Mamlaka ya Uchunguzi kama unajitosheleza kuweza kufungua mashtaka. Kama anaona kwamba ushahidi ulioletwa kutoka kwenye mamlaka ya uchunguzi haujitoshelezi kufungua mashtaka hatatao kibali cha kufungua mashtaka, mpaka pale atakapojiridhisha kwamba ushahidi unajitosheleza. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa Mbunge wa Longido, sasa aulize swali lake.

Na. 80

Upungufu wa Watumishi Halmshauri ya Longido

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA aliuliza:-

Halmshauri ya Longido inatakiwa kuwa na watumishi 1,660 wa kada mbalimbali lakini kwa sasa wapo 1atumishi 1,117 tu, hivyo, kuna upungufu wa watumishi 543 na wengi wao ni Watendaji wa Vijiji, Kata, Madereva na Makatibu Muhtasi:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa vibali vya kuajiri watumishi wanaohitajika ili kuondoa upungufu uliopo?

(b) Je, ni lini Serikali itatoa vibali vya kuwathibitisha maafisa wanaokaimu wenye sifa za kuajiriwa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora), napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, Mbunge wa Longido, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inakiri kuwepo kwa tatizo la upungufu wa watumishi kwa waajiri mbalimbali hapa nchini na siyo kwa Halmashauri ya Wilaya ya Longido pekee. Upungufu huu umesababishwa kwa kiasi kikubwa sana na zoezi la kuwaondoa katika Utumishi wa Umma watumishi waliobainika kutumia vyeti vya kughushi katika ajira zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na upungufu wa watumishi katika Halmashauri ya Wilaya ya Longido, Serikali imetoa kibali cha ajira mbadala nafasi tano (5). Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Longido itapatiwa nafasi za Walimu na Fundi Sanifu Maabara kutoka kwenye mgawo wa nafasi 4,549 za Ajira Mbadala za Walimu ambazo mchakato wake unaendelea chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua nyingine, Halmashauri ya Wilaya ya Longido imetengewa jumla ya nafasi 177 za kada mbalimbali zikiwemo Watendaji wa Vijiji, Kata, Madereva na Makatibu Muhtasi katika mwaka wa fedha ule 2018/2019. Katika kuhakikisha suala la upungufu wa watumishi katika Halmashauri ya Wilaya ya Longido linapatiwa ufumbuzi wa kudumu, Serikali itaendelea kutenga nafasi za ajira mpya pamoja na kutoa vibali vya Ajira Mbadala kwa kada za kipaumbele katika mwaka wa fedha 2019/2020 na kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sehemu (b) ya swali la Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, Mbunge wa Longido,

naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba watumishi wa umma wanaothibitishwa katika nafasi za uongozi kwa maana ya madaraka ni wale walioteuliwa rasmi katika nafasi hizo baada ya taratibu za upekuzi kukamilika. Aidha, hakuna utaratibu wa kuthibitisha watumishi wa umma wanaokaimu nafasi za uongozi kwa maana ya madaraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hufanya upekuzi kwa watumishi wa umma wanaokaimu nafasi za madaraka ili kubaini iwapo wanafaa au la. Uamuzi iwapo mtumishi husika anafaa kuteuliwa kwenye nafasi anayokaimu hutegemea na matokeo na upekuzi. Hivyo, pamoja na kuwa na sifa za kitaaluma, Serikali hailazimiki kumthibitisha mtumishi iwapo anakosa vigezo vingine vyta uongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa rai kwa watumishi wa umma wote nchini wanaokaimu nafasi za uongozi wafanye kazi kwa bidii, weledi, umahiri, uzalendo kwa kuzingatia maadili ya kazi ili waweze kukidhi vigezo vyta kuteuliwa na kisha waweze kuthibitishwa kwenye nafasi za uongozi ambazo ni madaraka wanazoteuliwa kuzishika. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Kiruswa swali la nyongeza.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijamuuliza maswali ya nyongeza, nichukue fursa hii kumpongeza Naibu Waziri wa Utawala Bora na Utumishi japokuwa ni muda mfupi tu tangu apewe dhamana ya kusimamia nafasi hiyo utendaji wake unaonekana na kasi yake nafikiri ni sehemu ya kasi anayohitaji Rais wa nchi kuona katika utendaji wa Mawaziri wetu. Hongera sana mama, nakuomba uendelee kukaza buti umsaidie Rais kazi aliyokupa dhamana ya kuifanya. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hilo, swali langu la kwanza, kwa kuwa katika Wilaya ya Longido lenye jumla

ya vijiji 49, kuna vijiji 22 ambavyo mpaka sasa hivi havina Watendaji wa Kijiji walioajiriwa, wako wanaokaimu tena wengine wamekaimu kwa miaka mingi. Ni lini sasa Serikali inakwenda kuipatia Halmashauri ya Wilaya ya Longido kibali cha kuajiri Watendaji hao ili kuziba pengo lililopo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalı langu la pili, naomba kupata majibu kwamba kwa kuwa katika baadhi ya zahanati tulizonazo katika Wilaya yangu ya Longido na vituo vyta afya na kuna vingine viko mbioni kukamilishwa kama kile cha Kimokorwa, Engarenaibo na kadhalika ambavyo vinajengwa kwa nguvu za wananchi na naamini Serikali mwaka huu watatupatia bajeti ya kuvimalizia. Pia Hospitali ya Wilaya ambayo nayo imeanza kujengwa na inakwenda kasi na hata Siha nimeona Hospitali ya Wilaya ambayo imejengwa jumba la ghorofa linakalibia kukamilika.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba watumishi watapatikana ili *facility* hizi ziweze kutoa huduma shahiki kwa Watanzania? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili madogo ya nyongeza yote kwa pamoja ya Mheshimiwa Mbunge Kiruswa wa Longido, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru sana kwa pongezi, nazipokea, aendeleee tu kuniombea kwa Mungu ili nisiwaangushe Watanzania wote na Mheshimiwa Rais mwenyewe. Pia na yeye binafsi nimpongeze kwa kazi nzuri ambayo anaifanya kwenye Jimbo lake la Longido hususani katika kufuatilia huduma zinazotolewa na watumishi wa umma kwa wapiga kura wake wa Jimbo la Longido.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu tu kwa ufupi na kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nafasi zote za kukaimu; kwanza kukaimu ni nafasi ya muda, wala siyo ya kuthibitishwa. Naomba niwaeleze Watanzania wote kwa faida ya wengine, kwa sababu kuna wengine huwa wanafikiri kwamba ukipewa nafasi ya kukaimu, basi ndiyo *leeway* yako ya kuthibitishwa, hapana. Kukaimu unakaimu kwa muda na mara nyingi watu wengi wamekuwa wakikaimu kwa muda mrefu kwa sababu watu wamekuwa wakikaimishwa kienyeji bila kufuata utaratibu. Utaratibu ni kwamba unapotaka kumkaimisha kiongozi ye yole yule ambaye ameshafikia katika ile *level* ambayo tunaita *superlative substansive post* (nafasi ya uongozi) basi unatakiwa kupata kibali kutoka utumishi. Utumishi wakupatia kibali.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile mwaka 2018 mwezi Septemba, Serikali yetu imetoa waraka kwamba nafasi zote zile za kukaimu zisizidi miezi sita. Unapotaka yule Afisa aendelee kukaimu, basi unatakiwa utoe sababu nyingine wewe kama Mwajiri kwa nini unataka aendelee kukaimu? Hiyo yote ni katika lengo la kuboresha ili viongozi wetu wasiwe wanakaimu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, kwenye jibu langu la msingi nimesema katika Jimbo lake la Longido tumetoa vibali na nafasi za ajira 177. Katika hizo 177, 65 zinakwenda katika Sekta ya Afya, 69 zinakwenda katika Sekta ya Elimu na zinazobaki nyingine zote zinakwenda katika kada nyingine mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika zile kada nyingine ambazo ni za kimuundo, zenyewe hazihitaji kukaimishwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge mwaka huu wa Fedha 2018/2019, hizi nafasi 177 tutakuwa tumeshazijaza katika Wilaya ya Longido hususan Jimbo lako.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora naomba nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri, Mwanjelwa kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongeze jibu kwenye swalii linalohusiana na Watendaji wa Serikali za Mitaa. Hii hoja ya Mheshimiwa Mbunge wa Longido ni kweli, lakini naomba niseme tu kwamba kupata Watendaji kwenye ngazi za Halmashauri na huu ni mwaka wa bajeti kwenye Bunge hili Tukufu, tunatarajia Wakurugenzi ambaa ndio waajiri wa watu hawa, Watendaji wa Vijiji, Watendaji wa Mitaa watakuwa wameingiza kwenye bajeti zao ili tupitishe na waweze kupata ajira. Kwa hiyo, Wakurugenzi wanapaswa kujua upungufu wa maeneo yao ya kiutendaji, kama wakiwasiliana na Ofisi ya TAMISEMI kwamba hawa watu wanafanya kazi kubwa sana waweze kusaidiwa utendaji katika ngazi ya chini. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Mheshimiwa Hassan Elias Masala, Mbunge wa Nachingwea sasa aulize swalii lake.

Na. 81

Barabara ya Masasi – Nachingwea – Ruangwa - Nanganga

MHE. HASSAN E. MASALA aliuliza:-

Je, ni lini ujenzi wa barabara ya Masasi – Nachingwea – Ruangwa - Nanganga utaanza kufanyika kwa kiwango cha lami?

NAIBU WAZIRI, UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Elias Masala, Mbunge wa Nachingwea, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Masasi – Nachingwea - Ruangwa hadi Nanganga yenyе urefu wa kilometra 145 ni barabara ya Mkoa inayohudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Nchini (*TANROADS*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa barabara hii kiuchumi na kijamii, Serikali iliamua kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwe lengo la kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami, kazi ambayo ilikamilika mwaka 2018. Hivi sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Serikali inatafuta fedha za ujenzi wa barabara hii, itaendelea kutengewa fedha za matengenezo mbalimbali ili iendelee kupitika wakati wote ambapo katika mwaka wa fedha 2018/2019 jumla ya shilingi milioni 547.4 zimetengwa kwa ajili ya kuifanyia matengenezo barabara hiyo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hassan Elias Masala, swali la nyongeza.

MHE. HASSAN E. MASALA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kupata nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi ya kutafutwa pesa kwa ajili ya barabara hii ni ahadi ya muda mrefu sana, lakini pia naomba niweke kumbukumbu vizuri kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, zoezi la kufanyia upembuzi yakinifu barabara hii ilikamilika mwaka 2015 wakati mimi naingia kuwa Mbunge na siyo 2008. Sasa naomba kujua, nini dhamira ya Serikali juu ya kutekeleza ahadi yake ya muda mrefu kuhakikisha fedha ndani ya mwaka huu wa bajeti

inapatikana ili barabara hii iweze kufanyiwa kazi kwa kiwango cha lami? Hilo ni swali la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili ambalo naomba nipate majibu, barabara hii kwa mujibu wa nyaraka nilizonazo, mwanzo kabisa wakati inafanyiwa upembuzi yakinifu ilikuwa inasomeka Masasi – Nachingwea – Nanganga, lakini baadaye ikaja kuanza kufanyiwa kazi barabara ya kutoka Nanganga – Ruangwa – Nachingwea. Sasa hivi majibu yanayotoka, kuna kipande cha kilometa 45 cha kutoka Nachingwea kwenda Nanganga hakisemwi na hakionekani katika maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujua msimamo wa Wizara juu ya kioande hili cha Nachingwea kwenda Nanganga ambacho ni kilometa 44.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

NAIBU WAZIRI, UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa umakini na ufuutiliaji wa maendeleo ya Nachingwea lakini siyo Nachingwea peke yake, bali pia maeneo ambayo kimsingi yanaunganika na Wilaya hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba kweli usanifu ulikamilika kipindi cha nyuma, lakini kwa jibu ambalo nimelitoa sasa hivi, kwa yale maandalizi ya kuanza ujenzi huwa kuna kitu ambacho tunaita mapitio. Tunafanya *review* ili tuweze kutangaza ujenzi wa barabara. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Masala kwamba *records* ambazo nimeziweka hapa kwa maana ya *review* ilikuwa ni maandalizi sasa ya kuanza ujenzi. Hivi tulikuwa tunafanya mawasiliano na wenzetu wa upande wa Wizara ya Fedha, fedha zikipatikana tunaanza kujenga barabara hii. Kwa hiyo, nimtoe hofu yeye pamoja na wananchi wa Nachingwea na majirani

zake, ni kwamba harakati za kufanya ujenzi wa barabara hii tumezifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la (b); kutokana na *review* ambayo nimeisema hapa imefanyika ili tuanze ujenzi, haimaanishi kipande hiki cha Nachingwea - Nanganga kwamba tunakiacha. Hiki ni vipambele tu kutokana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimwambie Mheshimiwa Masala kipande cha Nachingwea - Nanganga na chenyewe kiko kwenye mpango na vile vile tuwasiliane baadaye, atakuja kuona kwenye mpango mkakati wetu baada ya *review* kwamba tumejipanga vipi kuanza kujenga kwa kiwango cha lami. Kwa maana hiyo ni kwamba tukipata fedha tunaanza ujenzi wa barabara hizi muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Masala ajue kwamba wakati huo tunajiandaa, tunaendelea kushughulikia maeneo ambayo ni korofi, tunaendelea kushughulikia maeneo ambayo ni maalum, tunaendelea kujenga madaraja. Labda kwa manufaa ya wananchi wa Nachingwea niseme kwamba tumeendelea kukamilisha daraja la Lukuledi ambapo barabara niliyoijibia itapita ili tuwaungenishe vizuri wananchi hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tunaendelea kujenga maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Lindi, madaraja ya kule Chumo, kuna daraja Mlowoka, Mtakuja na Nanjilinji. Hii ina maana kwamba maeneo ambayo tumeyatengea fedha za kutosha na maeneo ambayo wananchi walikuwa wanapata usumbufu kupita katika maeneo haya tumeyazingatia. Kwa hiyo, wananchi wa Ruangwa, Nachingwea na maeneo yote ya Lindi, ni kwamba tumejipanga ili tuwahudumie vizuri.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, swali la nyongeza.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba niipongeze sana Serikali kwa kuunganisha barabara nyingi za nchi yetu kutoka Wilayani na Makao Makuu ya Mikoa yetu. Sambamba na hilo napenda niulize swali langu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Bungu - Nyamisati inaunganisha Wilaya ya Mafia na Kibiti. Sasa barabara hii iko chini ya kilometra 50 na kama mnavyojua historia, Mafia ni Kisiwa, wanatumia usafiri mmoja tu ambao ni ndege. Je, ni lini barabara hii itaunganishwa kwa kiwango cha lami ili kuwasaidia wananchi wa Mafia? (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

NAIBU WAZIRI, UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Kikwete kwa namna anavyofuatilia maendeleo ya sehemu mbalimbali. Kwa hiyo mara nyingi nimemsikia akizungumza juu ya Lindi, leo anazungumza juu ya Pwani, kwa hiyo nampongeza sana. Hata maeneo mengine, nimemsikia pia akiwasemea walimu kwa kiasi kikubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili la Nyamisati ni eneo muhimu sana. Nifahamishe tu Bunge lako pamoja na wananchi kwa ujumla, ni kwamba tunatengeneza gati katika eneo hili la Nyamisati kwa lengo la kuhudumia kivuko ambacho pia tumeanza hatua za manunuzi, kivuko ambacho kitatuvusha kutoka Nyamisati kwenda Kilindoni kule Mafia. Tunaendelea vizuri. Kwa hiyo, niwahakikishie tu wananchi hawa wa Nyamisati na wananchi wa Pwani na Watanzania kwa ujumla kwamba tutakuwa na kivuko ambacho kitatusaidia kupunguza usumbufu uliokuwepo kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapotengeneza kivuko pamoja na gati hii lazima ule mnyororo wa usafiri tuuveke vizuri. Ndiyo maana nami nimetembelea eneo hili kilometa kama 48 hivi kutoka Bungu kwenda Nyamisati ili kuhakikisha kwanza barabara tunaiweka katika ubora unaohitajika, lakini pia mipango yetu ipo ili tuje kuweka lami barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii muhimu itatusaidia pia kusafirisha mizigo mingi kutoka Nyamisati kwenda hata sehemu hii ambayo tunajenga umeme (*Stiegler's Gorge*) kwa sababu barabara hii kutoka Kibiti kwenda *Stiegler's Gorge* tumeiboresha na tunaamini kwamba gati hii ikiboreshwaa kutakuwa na vyombo ambavyo vitabeba mizigo mizito kuja Nyamisati ambavyo vinaweza vikahitajika kwenda kwenye maeneo ya mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatumaini kwamba barabara hii kuiboresha pamoja na kuiweka kiwango cha lami itatusaidia sana kubeba mizigo na kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsnate sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lucia Michael Mlowe, Mbunhge wa Viti Maalum, sasa aulize swalii lake.

Na. 82

Barabara ya Makete - Njombe na Itoni - Ludewa

MHE. LUCIA M. MILOWE aliluliza:-

Barabara za Makete Njombe na Itone - Ludewa zipo katika ujenzi lakini ujenzi huo unakwenda pole pole sana:-

Je, ni lini ujenzi wa barabara hizo utakamilika?

**NAIBU WAZIRI, UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
(MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Lucia Michael Mlowe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Njombe - Makete kilometra 107.4 umejengwa katika sehemu mbili za Njombe - Moronga kilometra 53.9 na Moronga - Makete kilometra 53.5 ili kuharakisha utekelezaji wake. Hatua ya utekelezaji inayofikiwa hadi Machi, 2019 ni asilimia 25.2 ambapo kazi zinatarajiwaa kukamilika ifikapo mwezi Januari, 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa ujenzi kwa kiwango cha zege wa barabara ya Itoni – Ludewa – Manda sehemu ya Rusitu - Mawengi kilometra 50 umefikia asilimia 20.14. Mradi huu unatarajiwaa kukamilika mwezi Oktoba, 2020. Napenda nimkahakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa Wizara kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) itaendelea kuwasimamia Wakandarasi wa miradi hii ili waweza kukamilisha ujenzi wa barabara hiyo kwa wakati uliopangwa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lucia Michael Mlowe, swalii la nyongeza.

MHE. LUCIA M. MLOWE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye majibu ya Mheshimiwa Waziri amesema kwamba hadi sasa amefikia asilimia 25.2 barabara inayokwenda Njombe - Makete na asilimia 20 barabara ya Itone – Ludewa: Je, kama sasa hivi ni asilimia 25 na mwakani mwezi wa kwanza iwe imekamilika, ni muujiza gani utatendeka hapo kuikamilisha kwa miezi nane tu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili. Hali ya barabara za Njombe Mjini na Vijiji ni mbaya sana kwa kuwa mvua

sasa hivi zinaendelea kunyesha. Kuna hali mbaya sana kwenye zile barabara na watu sasa hivi wamesimamisha shughuli, hawawezi tena kusafirisha bidhaa au mazao: Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha inakarabati barabara hizi kwa haraka iwezekanavyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI, UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba tuko asilimia hizo 25.2 na asilimia 20 kwa eneo la Itone – Ludewa, lakini labda nilifahamishe tu Bunge lako kwamba Mkoa wa Njombe hali ya jiografia yake ni maalum sana, ni *special*. Udongo wa Njombe siyo mchezo, kwa hiyo, hata kufikia asilimia hizi ilitakiwa Mheshimiwa Mbunge aipongeze Serikali. Ndiyo unaona kwamba barabara hii ambayo tunaijenga Lusitu - Mawengu ni barabara chache sana tumeweza kujenga kwa kiwango cha zege.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kutokana hata na udongo wake tuliotumia kwa ujenzi, ulikuwa unatoka zaidi ya kilometra 200, kwa sababu udongo wa Njombe uko maalum kidogo. Kwa hiyo, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba mpango kazi ambao sisi kama Serikali tunausimamia, tutahakikisha kwamba kila wakati tunakwenda nao ili kama kutatokea zile *natural calamity* kama mvua kuwa nyngi, kama maporomoko katika maeneo haya, hata juzi tu barabara hii illijifunga kwa sababu udongo wake unaporomoka sana. Kwa hiyo, nasi tunachukua hatua kila wakati ili kuhakikisha kwamba tunafanya marekebisho, ujenzi unaendelea, tukamilishe mradi huu kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ule mpango kazi yaani *action plan* tutaendelea kuisimamia ili kuona kama kutakuwa na matatizo makubwa ya hali ya hewa tuangalie *alternative* ya kufanya barabara hii ikamilike na barabara hii

wananchi wa Njombe na Watanzania wanaitumia. Kwa hiyo, miujiza ni ile ya Mungu kwamba tunasimamia vizuri na mvua ziwe nzuri, tuombe Mungu pamoja ili tukamilishe barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu (b), amesema barabara za vijjini hali ni mbaya. Ni kweli kama nilivyosema, hali ya jiografia ni mbaya, lakini sisi tumejipanga vizuri ndiyo mana utaoa kwamba tunao mpango kama tukipata fedha tutaanza kutengeneza hii barabara ya kipande cha kutoka Kibena kwenda Lupembe kwenye mpango wa manunuzi tunaoendelea nao, kilometra 50, tuanze kupunguza na kuwafanya wananchi wa maeneo ya Njombe waweze kwenda Morogoro kupitia Madeke na Mlimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, yale maeneo ambayo yako korofisana, tunaendelea kujenga barabara za zege kwa hiyo, zipo kilometra 126, ukitoka Lupembe pale ziko kilometra ambazo tunaendelea kuziunganisha na wananchi sasa wana-enjoymagari yanatoka Mlimba yanakuja Njombe. Kwa hiyo, ni hatua za Serikali kuwajali wananchi wa Njombe kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimfahamishe tu Mheshimiwa Mbunge, hata hii barabara tunayozungumza ya kutoka Mawengi – Lusitu, sehemu ya Itoni kwenda Lusitu na yenyewe tunaitazama kwa sababu ni muhimu tuwaunganishe vizuri. Pia tunatengeneza daraja kule Mto Ruhuhu ili wananchi hawa wa Njombe tuwaunganishe vizuri na wenzao wa Manda kule Ruvuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme tu kwa ufupi kwamba tumejipanga vizuri, Njombe iko *so special*/lakini nasi kama Serikali tuko *special*/kwa ajili ya Njombe ili wananchi wapate huduma vizuri.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Mary Deo Muro, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalii lake.

Na. 83

Kuhamisha Kituo cha Misugusu Check Point

MHE. MARY D. MURO aliuliza:-

Je, ni lini Kituo cha Misugusugu “Check Point” kitahamishwa, kwani kimekuwa kero kutokana na vumbi linalosababishwa na miundombinu mibovu?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mary Deo Muro, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Nailbu Spika, Serikali inatekeleza mradi wa kituo cha pamoja cha ukaguzi wa mizigo (*One Stop Inspection Station*) ili kuziwezesha mamlaka za ukaguzi wa mizigo kufanya kazi ya ukaguzi katika eneo moja. Mradi huu unatekelezwa sambamba na mradi wa mizani ya ukaguzi wa mizigo iliyopo Vigwaza Mkoa wa Pwani. Taasisi zinazohusika katika mradi huu ni pamoja na *TANROADS*, Polisi na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Mapato Tanzania ipo katika hatua za awali za kujenga na kusimika mifumo ya ukaguzi katika eneo la mradi liliopo Vigwaza, hivyo basi kituo cha ukaguzi wa mizigo kitahamishiwa kutoka Misugusugu kwenda vigwaza mara baada ya kazi ya kujenga na kusimika mifumo itakapokamilika.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mary Deo Muro, swali la nyongeza.

MHE. MARY D. MURO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Swali la kwanza, ni kwa nini Serikali haikufikiri kabla haijaanzisha mradi huo wa maroli kupaki pale Misugusugu mpaka ikafikia wananchi wa Misugusugu wanapata *TB*?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, nini mkakati wa Serikali wa dharura kwa ajili ya kuokoa maisha ya wana Misugusugu? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Deo Muro, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii lake la kwanza kwa nini Serikali haikufikiri kabla, Serikali siku zote inafikiri, ilifikiri enzi hizo na sasa inaendelea kufikiri ili kuendelea kuboresha maisha ya wananchi wetu hasa hawa wa Misugusugu na ndio maana Wizara ya Ujenzi imeanza kuiboresha barabara ile ili kuondokana na changamoto hii ya vumbi pamoja na kwamba Serikali inatekeleza mradi huu wa *Euro* milioni 23 kuhakikisha sasa eneo lile la Misugusugu kituo kile kinaondoka na kinahamia vigwaza. Kuonesha kwamba Serikali inaendelea kufikiri na kutenda kwa ajili ya wananchi wake, haya tunayoyatenda Vigwaza yanakwenda kutendwa Manyoni na pia tunakwenda kutekeleza mradi wa aina hii kule Nyakanazi ili kuhakikisha huduma hizi zinafanyika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii lake la pili, ni mkakati wa dharura, ndio huu ambaa nimeeleza kwamba Serikali inaboresha barabara il, lakini tunahakikisha mradi huu unakamilika kwa wakati. Nitoe wito kwa Watanzania wote kwa ujumla maana ya kuwa na vituo hivi ni kuhakikisha mizigo ile yenye uhatarishi wa upotevu wa mapato tunaendelea kui-control hatua kwa hatua. Hata hivyo, pia wito wangu kwa Watanzania ni kuhakikisha kwamba wao wanakuwa wazalendo zaidi kwa Taifa lao ili mizigo hii ambayo wana-declare kwamba inaenda nchi jirani isiendelee kushushwa ndani ya Taifa letu. Unapoona gari linashusha mizigo ndani ya kijiji chako jilize mara mbili kwa nini halikushusha mjini na lazima Watanzania wafahamu kwamba hakuna maendeleo bila kodi itakayolipwa na sisi Watanzania wenyewe na Serikali

ya Awamu ya Tano imeonesha mfano na tunatenda kwa vitendo kwamba kodi ya Watanzania sasa inapelekwa kwenye miradi inayowafikia wananchi moja kwa moja.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa, Mbunge wa Kalenga, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Venance Methusalah Mwamoto.

Na. 84

Tatizo la Utapiamlo – Iringa

MHE. VENANCE M. MWAMOTO (K.n.y. MHE. GODFREY W. MGIMWA) aliuliza:-

Taarifa mbalimbali za kitafiti zinaonesha kwamba Mkoa wa Iringa unaongoza kwa tatizo la utapiamlo:-

(a) Je, ni vigezo gani vinatumika kufikia kwenye takwimu hizo?

(b) Je, jitihada gani zinachukuliwa na Serikali kunusuru tatizo hilo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa, Mbunge wa Kalenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa ni kweli kabisa Mkoa wa Iringa ni miongoni mwa mikoa inayoongoza kwa tatizo la udumavu

kwa asilimia 42. Wastani wa Kitaifa ni asilimia 34, kwa mujibu wa takwimu za utafiti wa demografia na afya wa mwaka 2015/2016 uliofanywa na Ofisi ya Takwimu ya Taifa kwa kushirikiana na Wizara ya Afya Tanzania Bara na Zanzibar pamoja na Wadau wa Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vigezo vilivytumika kufikia takwimu hizo ni pamoja na kuchukua sampuli za kaya zilizochaguliwa kushiriki kuititia utaratibu maalum wa kitaalaam ili kuziwakilisha kaya nyingine katika Wilaya. Kwa kaya zilizochaguliwa watoto chini ya miaka mitano walipimwa urefu au kimo, uzito, kupimwa wekundu wa damu pamoja na kuhoji maswali kwa Mkuu wa Kaya au mlezi kwa kutumia dodoso maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imechukua hatua mbalimbali katika kunusuru tatizo hilo ikiwa ni pamoja na kuandaa na kutekeleza Mpango Mkakati Jumuishi wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Afua za Lishe (*National Multisectoral Nutrition Action Plan*) wa mwaka 2016/2017 ambayo itaisha mwaka 2021/2022 ambao una vipaumbele vinavyolenga kupunguza utapiamlo ifikapo mwaka 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa lishe inaendelea kutekeleza afua za lishe zenye matokeo makubwa ambayo ni pamoja na:-

(i) Utoaji wa vidonge vya madini chuma na asidi ya foliki kwa wajawazito;

(ii) Utoaji wa matone ya vitamin A na dawa za minyoo;

(iii) Uongezaji wa virutubishi vya madini na vitamin kwenye vyakula hususani unga wa ngano, mahindi, mafuta ya Kula pamoja na urutubishaji wa kibiolojia wa mazao katika viazi vitamu, mahindi, maharage na mihogo;

(iv) Kutoa matibabu ya utapiamlo mkali kwa watoto chini ya miaka mitano;

(v) Utoaji wa elimu na huduma ya lishe kwa wanawake, wasichana na watoto wachanga na wadogo, elimu ya ulaji wa vyakula mchanganyiko na mtindo bora wa maisha; na

(vi) Utoaji wa Ajira Maafisa Lishe katika ngazi za mikoa na halmashauri.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Venance Mwamoto, swali la nyongeza.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba niulize maswali mawili. Swali la kwanza; kwa kuwa tatizo hili sasa ni kubwa na linafahamika kwa muda mrefu hususani Mkoa wa Iringa.

Je, Waziri atakuwa tayari kuja Iringa kuona hali ambayo inaendelea kwa sababu hali ni mbaya hiyo elimu ambayo ilitakiwa itolewe haitolewi kwa muda na watu wanazidi kuathirika?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa shule nyingi wanakunywa uji, je, sasa haoni ni wakati muafaka sasa wa kuchanganya chakula lishe kwenye uji wao ili iwe rahisi zaidi watoto wote wakapata kwa sababu ndio wanaoathirika? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mbunge wa Kalenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru na kumpongeza kwa kuwa ni mdaa wa masuala ya lishe, lakini nipongeze vilevile Bunge lako Tukufu kwa sababu wana Chama cha Waheshimiwa Wabunge ambao wanasi mamia

masuala ya lishe ambacho kinaongozwa na Mheshimiwa Dunstan Kitandula, yote hii inaonesha kwamba na nyinyi kama Bunge mnalisimamia suala hili kikamilifu.

Pia kwa njia ya kipekee vilevile nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuzindua mpango mkakati wa masuala ya lishe nchini na kutoa maagizo kwa Wakuu wote wa Mikoa na kuwapa malengo ambayo ya kusimamia katika masuala haya ya lishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niko tayari muda wowote kwenda Iringa kwenda kuwahamasisha masuala ya lishe katika mkoa huu. Vilevile ninachotaka kukisema ni kwamba hali ya udumavu tunaiona katika mikoa inazalisha chakula kwa wingi Rukwa, Katavi pamoja na Iringa ni mikoa ambayo kwa kiasi kikubwa sana inazalisha chakula kwa wingi, lakini kuna udumavu mkubwa sana kuliko mikoa mingine ambayo haizalishi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, yote hii inaonesha kwamba elimu ya lishe bado ni changamoto kubwa sana na hili sisi kama Wizara tuko tayari kwenda kule kushirikiana na timu zetu za mikoa kuhakikisha kwamba tunalifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nitumie fursa hii kutoa rai kwa jamii sasa hivi kama Taifa tunaona hali ya udumavu inazidi kupungua, lakini tumeanza kuona vilevile lishe iliyopitiliza imeanza kuongezeka, asilimia 10 ya Watanzania wana lishe ambayo imepitiliza, maana yake ni nini? Ni kwamba wote hapa wengi hatuzingatii misingi ya lishe, tunakula bora chakula kuliko chakula kilicho bora.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe tuulize maswali kwa kifupi na Mawaziri pia mjibu majibu kwa kifupi. Tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi Mbunge wa Ukerewe sasa aulize swalii lake.

Na. 85

Matumizi ya Nyavi Kuzingatia Aina ya Dagaa

MHE. JOSEPH M. MKUNDI aliuliza:-

Kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi Na.22 ya mwaka 2003, Dagaa wanapaswa kuvuliwa kwa wawu wenyewe matundu mm 8 – mm10, lakini sheria hii haijazingatia aina tofauti za dagaa:-

Je, kwa nini Serikali isifanye utafiti utakaoainisha matumizi ya nyavi kutegemea aina ya dagaa wanaopatikana kwenye Ziwa husika?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ina jukumu la kulinda, kuhifadhi na kuendeleza na kuhakikisha kuwa rasilimali za uvuvi hapa nchini zinavunwa kwa busara ili ziwe endelevu kwa manufaa ya kiuchumi, kijamii na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria na kanuni zinazosimamia uvuvi nchini zinalenga uvuvi unaofanyika uwe endelevu ambapo Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (*TAFI/RI*) hufanya tafiti ili kubaini athari za matumizi ya dhana na mbinu mbalimbali za uvuvi kwa rasilimali za uvuvi na kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 66(1)(k) cha Kanuni za Uvuvi za mwaka 2009 kinaeleza kuwa nyavi za dagaa zenyehukubwa wa machi chini ya milimita nane zimakatazwa kutumika kwa uvuvi wa dagaa katika maji baridi

ikiwemo Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa. Aidha, tafiti zilizofanyika katika Ziwa victoria zinaonesha kuwa aina moja tu ya dagaa anayejulikana kwa jina la kitaalam *Rastrineobola argentea*. Utafiti pia unaonesha nyavu zenyé macho kuanzia milimita nane zikitumika kuvua dagaa hawa Ziwa Victoria zitavua dagaa waliopevuka na matumizi ya nyavu zenyé matundu chini ya milimita nane zikitumika zitavua dagaa wachanga na hii itaathiri uvuvi wa dagaa katika Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Uvuvi na Kanuni zake imezingatia aina ya dagaa katika maji baridi na maji bahari. Aidha, *TAFI/R* itafanya utafiti ikiridhika kuna haja ya kufanya hivyo katika Ziwa Victoria kuhusiana na uvuvi wa dagaa. Serikali inaendelea kusisitiza wavuvi kuzingatia sheria na kanuni zilizopo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Nitumie fursa hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake na nimshukuru kwa ushirikiano ambao amekuwa anautoa kwa masuala ya uvuvi. Nina maswali mawili ya nyongeza; la kwanza uvuvi wa dagaa wanavuliwa kwa kuchotwa, kwa hiyo isitegemee kwamba wategemee dagaa wale wanase kwenye nyavu, ndio maana ni muhimu angalau matundu yake yawe madogo kidogo. Sasa kwa kuwa dagaa wanaopatikana Ziwa Victoria hawatofautiana sana na dagaa wanaopatikana Bahari ya Hindi na natambua kuna mchakato wa kufanya utafiti kwenye Bahari ya Hindi ili dagaa wanaovuliwa kwenye Bahari ya Hindi wavuliwe kwa nyavu za milimita sita na kuendelea. Je, Serikali haioni sababu sambamba na utafiti utakaofanyika Bahari ya Hindi ufanyike vilevile na uvuvi utakaofanyika Ziwa victoria kwa dagaa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, wavuvi wa Ukerewe wa samaki aina ya *gogogo* au *ngere* wanapata

buguza sana wakati wanavua samaki wale kwa kisingizio kwamba sheria hairuhusu, lakini mazingira ya uvuvi wa samaki wale na aina yake ni tofauti sana na samaki wengine. Je, Serikali iko tayari sasa kutoa tamko ili wavuvi wa *ngere* kwenye Visiwa vya Ukerewe na maeneo mengine wasibughudhiwe ili wafanye shughuli zao za uvuvi wa samaki hawa bila shida yoyote. Nashukuru sana? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

NAIBU WAZIRI MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Mkundi na timu ya Waheshimiwa Wabunge katika eneo la Ziwa Victoria kwa namna ambavyo mara kadhaa wamekuwa wakisimamia maslahi mapana ya wapigakura wa eneo hili ikiwa ni pamoja na kulinda rasilimali za nchi yetu kupitia sekta hii ya uvuvi. Sasa swalii la kwanza la Mheshimiwa Mkundi linahusu juu ya ya Serikali kuwa tayari kufanya utafiti katika eneo la Ziwa Victoria kama ambavyo tunafanya utafiti kwenye maji ya bahari ili kuweza kuruhusu nyavu ya chini ya milimita nane kuweza kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge kuwa, kwa upande wa bahari bahari zilizokuwa zikitumika ni milimita 10 na zimekubalika kuonekana na maoni ya wadau kuwa milimita 10 zimeshindwa kukamata dagaa na ndio maana Serikali tukaielekeza Taasisi yetu ya Utafiti (*TAFIRI*) kufanya utafiti na kujiridhisha ya kwamba tufanye mabadiliko ya kanuni kwa haraka ili ikiwezekana tuweze kutumia nyavu za milimita nane ili kuweza kuwabnufaisha wavuvi wa upande wa bahari.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa rai hii ya kutaka tutumie njia hiyo ya utafiti kwa upande wa Ziwa Victoria, naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mkundi na

Waheshimiwa Wabunge wote wavuvi wa kutoka Ziwa Victoria tunaichukua rai hiyo na tutawaelekeza *TAFIRI* waweze kufanya utafiti na kuweza kujiridhisha bila ya kuathiri sekta hii ya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili la Mheshimiwa Mkundi linahusu uvuvi wa samaki aina ya *gogogo, ngere* na *ningu*. Samaki hawa ni samaki wenye kupendwa sana katika eneo la Ziwa Victoria naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge katika mabadiliko ya kanuni tunayoyafanya hivi sasa tumezingatia kwamba tufanye makubaliano ya kuweza kuitisha kanuni rasmi sasa ya kuweza kuvua na kutumia rasilimali hii ya samaki hawa aina ya *gogogo, ninguna ngere* ambao wameonekana katika kanuni zilizopita kuwa hawakutajwa moja kwa moja. Naomba niwahakikishie wavuvi wote wa eneo la Ziwa Victoria Serikali inalifanya kazi jambo hili na muda si mrefu watapata matokeo ili waweze ku-*enjoy* na kufurahlia rasilimali za Taifa lao.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Maji Mheshimiwa Dkt. Mary Michael Nagu, Mbunge wa Hanang, sasa aulize swalii lake.

Na. 86

Tatizo la Maji – Wilaya ya Hanang

MHE. DKT. MARY M. NAGU aliuliza:-

Maeneo mengi katika Wilaya ya Hanang' yana matatizo ya maji ingawa Kata za Dirma, Lalaji, Wandela, Gawidu, Bassodesh na Mwanga zina visima vilivyo chimbwa licha ya maji kutopatikana:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kutatua matatizo ya maji katika wilaya hiyo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Dkt. Mary Michael Nagu, Mbunge wa Hanang', kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika juhudii za kutatua matatizo ya maji katika Wilaya ya Hanang', Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi ya maji katika maeneo mbalimbali ya Wilaya hiyo katika Vijiji vya Hirbadaw, Kata ya Hirbadaw na Murumba, Kata ya Lalaji utekelezaji wa miradi upo katika hatua za mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Vijiji vya Bassodeshi, Nyabati, Gijetamuhog, Murumba, Gorimba, Diloda na Qalosendo katika Kitongoji cha Merekwa wananchi wanapata huduma ya maji kupitia visima vilivyochimbwa. Sehemu ya Kijiji cha Dirma iliyopo Kata ya Dirma inapata maji kutoka kwenye Mradi wa Maji ya Mtiririko wa Nangwa. Kijiji cha Gawidu ni mionganini mwa vijiji vitakavyojumuishwa katika miradi ya Bassotu ambapo utekelezaji wa mradi huo umefikia asilimia 90. Aidha, utekelezaji wa mradi huo utaendelea katika vijiji vingine kwa awamu kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa Serikali ni kuendelea kutekeleza miradi mipyaa, kukamilisha inayoendelea na kukarabati ya zamani kwa kadri fedha zitakapopatikana ili kuhakikisha wananchi wa Wilaya ya Hanang' wanapata huduma ya maji na yenye kutosheleza.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, swalii la nyongeza.

MHE. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kujibu swalii vizuri na naishukuru Serikali kwa jitihada zake zinazoelekezwa Hangang' hasa ziwe Bassotu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Swalii la kwanza, ni kweli visima vimechimbwa, lakini nafikiri ni Wilaya ya peke yake ambayo zimewekwa *solar* ambazo hazina betri na ni

Wilaya ambayo *temperature* yake iko chini kwa hiyo maji hayapatikani kila wakati. Sasa nataka kujua wakati kwingine kunawekwa *solarza* betri kwa nini Wilaya ya Hanang' katika visima mbalimbali vilivyo chimbwa kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri hawakuweka betri hizo na hasa Masakta ambapo ilipangiwa shilingi bilioni 1.2 mpaka leo tatizo liko palepale? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Wilaya ya Hanang' iko kwenye bonde la ufa na kwa hivyo kuna joto chini, kwa hiyo kupata maji kwenye visima ni ngumu sana. Sasa nataka Mheshimiwa Naibu Waziri anieleze kama bwawa linalotakiwa Dirma linachimbwa na bwawa la Gehandu na Gidahababieg linachimbwa kusudi tatizo hilo la ujumla la Hanang' liweze kukabiliwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana mama yangu Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu kwa kazi kubwa anayofanya. Ni miongoni mwa wamama ambao wamejitoa kupigania suala zima la maji katika jimbo lake la Hanang.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali la kwanza la changamoto ya betri, nimuagize Mhandisi wa Maji wa Mkoa wa Manyara afuatilie kwa haraka ili changamoto hizi tuweze kuzitatua kwa haraka ili wananchi wake waendelee kupata huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yenyewe ukame au yaliyopitiwa na bonde la ufa, uchimbaji wa visima imekuwa ni changamoto kubwa sana, mfano Dilma. Sisi kama Wizara ya Maji tumeona haja sasa ya kuchimba mabwawa. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, sisi kama Wizara ya Maji hatutakuwa kikwazo katika uchimbaji wa mabwawa ili

wananchi wake waweze kupata huduma hii muhimu na kuweza kumtua mwanamama ndoo kichwani. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Kilimo na hili ndio swali letu la mwisho. Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 87

Kukamilisha Ujenzi wa Bwawa la Umwagiliaji Kijiji cha Ishololo – Wilaya ya Shinyanga

MHE. AZZA H. HAMAD aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha mradi wa ujenzi wa Bwawa la Umwagiliaji katika Kijiji cha Ishololo, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA): Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Azza Hilal Hamad, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa ujenzi wa Bwawa la Ishololo uliopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini ni moja kati ya miradi iliyokuwa ikitekelezwa kuitia Mradi wa Uwekezaji katika Kilimo katika Wilaya (*DAS/P*) chini ya iliyokuwa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Utekelezaji wa mradi huo ulifikia ukomo wake mwezi Desemba, 2013 ambapo Benki ya Maendeleo ya Afrika ilisitisha kutoa fedha za utekelezaji wa miradi wakati utekelezaji wake ukiwa haujakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inayo dhamira ya kukamilisha skimu zote za umwagiliaji ambazo utekelezaji wake haujakamilika kutokana na sababu mbalimbali,

ikiwemo ukosefu wa fedha. Skimu hii ipo mionganoni mwa skimu za umwagiliaji zitakazopewa kipaumbele katika kutekeleza Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji (*Irrigation Master Plan 2018 - 2025*) ambapo kwa sasa umeanza kutekelezwa. Kwa kuzingatia umuhimu wa miradi hii ikiwemo mradi wa umwagiliaji wa Ishololo, tayari Serikali imekwishaanza mazungumzo na wadau mbalimbali, ikiwemo Serikali ya Japan kupitia Shirika lake la Maendeleo la JICA kwa lengo la kuboresha miradi yote ambayo haijakamilika na ile inayofanya kazi chini ya ufanisi uliokusudiwa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, swalii la nyongeza.

MHE. AZZA H. HAMAD: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali ya nyongeza. Kwanza nilshukuru Serikali kwa majibu yake mazuri, lakini sasa naomba nimuulize Naibu Waziri maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la kwanza, je, Serikali ipo tayari sasa kuipa kipaumbele Skimu ya Umwagiliaji ya Ishololo ili iweze kuleta tija kwa wakulima wetu mara itakapokuwa imepata fedha?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, ni lini Serikali itachimba bwawa katika Skimu ya Umwagiliaji ya Nyida ambayo imekuwa ikitegemea maji ya mto ambao ni wa muda?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA): Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Azza Hillal kwa kuonesha uongozi kwa mfano. Tunamfahamu ni mdau wetu mzuri katika sekta ya kilimo, ni mkulima mkubwa wa mpunga, anawaongoza watu wake wa Shinyanga yeye mwenyewe kwa kuwa mbele na wale wanaoongozwa kuwa nyuma. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza kujibu swalilake la nyongeza la kwanza, nimhakikishie kwamba Serikali ipo tayari kuipa kipaumbele hii Skimu ya Ishololo pale ambapo tutaanza kupata pesa. Kama nilivyosema kwenye majibu yetu ya awali, tumeshaanza mazungumzo na wadau wetu mbalimbali ikiwemo Serikali bya Japan kuititia Shirika lake la *JICA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swalilake pili kuhusu suala la ujenzi wa bwawa katika hii Skimu ya Nyida, nimhakikishie Mheshimiwa Azza Hillal Serikali inafahamu na ipo katika mipango mikakati yetu kwa miradi yote ile inayotumia maji katika mito ambayo ni ya msimu kuijengea mabwawa ukiwemo huu wa Nyida ili tuweze kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuleta kilimo chenye tija, chenye manufaa kwa wakulima wetu.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali. Nitaleta kwenu matangazo tuliyonayo siku ya leo. Kwanza ni matangazo ya wageni tulionao. Tutaanza na wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Kuna wageni wawili wa Mheshimiwa Antony Mavunde ambaye ni Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana na Ajira) ambaao ni wapiga kura wake kutoka Jijini Dodoma, Ndugu John Msawa na Ndugu Hadija Amrani. Karibu sana. (*Makof!*)

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Mwita Waitara ambaye ni Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI ambaao ni watoto wake kutoka Ukonga, Jijini Dar-es-Salaam, Ndugu Johnson Waitara, Ndugu Jefferson Waitara na Ndugu Chacha Mwita. Karibuni sana. (*Makof!*)

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Naibu Waziri wa Kilimo, ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe, Ndugu Dawson Paulo. Karibuni sana. (*Makofii*)

Wageni 27 wa Mheshimiwa Daniel Mtuka ambaao ni walimu wa Shule ya Sekondari Manyoni, wakiongozwa na Ndugu Jackson Thadayo. Karibuni sana. (*Makofii*)

Wageni saba wa Mheshimiwa Sonia Magogo ambaao ni familia yake kutoka Jijini Dar-es-Salaam, wakiongozwa na kaka yake Ndugu Edwin Magogo. Karibuni sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni sita wa Mheshimiwa Shamsia Mtamba ambaao ni familia yake kutoka Mkoani Mtwara wakiongozwa na mume wake Ndugu Salehe Kanoga. Karibuni sana. (*Makofii*)

Wengine ni wageni sita wa Mheshimiwa Seif Gulamali ambaao ni wanachuo kutoka Chuo cha Ualimu Morogoro wakiongozwa na Ndugu David Mwangamba. Karibuni sana. (*Makofii*)

Wageni 10 wa Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa ambaao ni Viongozi wa Chama cha Mapinduzi, Wilaya ya Rufiji, wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Rufiji, Ndugu Rajab Mbonde. Karibuni sana. (*Makofii*)

Wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo na kundi la kwanza ni wanafunzi 105 kutoka Shule ya Msingi Feza. Wamekuja kujifunza namna Bunge linavyoendesha shughuli zake wakiongozwa na Mwalimu Salum Shoo. Karibuni sana. (*Makofii*)

Tunao pia wanafunzi 35 na walimu 2 kutoka Shule ya Sekondari ya *Mteria Dam* iliyopo Jijini Dodoma ambaao wamekuja kujifunza namna Bunge linavyofanya shughuli zake. Karibuni sana. (*Makofii*)

Wengine ni wanafunzi wa mwaka wa tatu kutoka Chuo Kikuu cha Doaoma wanaochukua mchepuo wa *Media, Arts and Design*. Wamekuja kujifunza shughuli za Bunge wakiongozwa na Ndugu Heri Daimon. Karibuni sana. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, hao ndiyo wageni tulionao siku ya leo Bungeni. Pia, ninalo tangazo hapa la kazi, Waheshimiwa Wabunge, mnatangaziwa kuwa mchukue nakala za Taarifa za CAG kwenye *pigeon holes* zenu kwa kuwa zimekuwepo humo kwa muda mrefu, mnazuia Ofisi ya Bunge kuendelea kuwawekea taarifa kwa wale ambao sehemu zenu zimejaa. Hizo taarifa humu ndani mlikuwa mnadai mnazihitaji sana, sasa mkazichukue mmeshawekewa huko kwenye *pigeon holes* zenu. (*Makofii*)

Tangazo lingine, kuna mtu alisahau miwani yake, ataenda Ofisi ya Bunge ili aweze kuchukua. Aliisahau miwani yake humu ndani karibu na kitu cha Mheshimiwa Nyongo. Miwani ni ya rangi nyeusi, sijajua kama ni ya aina gani, kwa hiyo, mtaenda mchukue ofisi ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tunaendelea na ratiba yetu.

HOJA YA HAKI ZA BUNGE

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, Hoja ya Haki za Bunge.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nimepata taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mnyika ya kusudio lake la kuwasilisha Hoja ya Haki za Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 51(1). Kwa namna Kanuni zetu zilivyoandikwa ukiisoma hii Kanuni ya 51 inamtaka Mheshimiwa Mnyika alete taarifa hii kwa Mheshimiwa Spika mapema ili kusudio lake hilo liweze kupata fursa ya kuwasilishwa hapa Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, kwa taarifa aliyoitoa ambayo nimeletewa hapa Mezani, nataka kuamini kwamba

ameiandika akiwa hapa kwa sababu haijapokelewa rasmi na ofisi kwa sababu haina mhuri wa Katibu. Hata hivyo, kwa matakwa ya Kanuni yetu inanitaka nimsikilize kwa muda mchache ili nifahamu kama jambo lake nitaliamua vinginevyo. Kwa hiyo, nakupa dakika tatu Mheshimiwa Mnyika nikusikilize ili niweze kutoa maamuzi.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Gazeti la leo la Fahari Yetu limeandika katika ukurasa wa mbele kwamba, 'Bunge lamtupa rasmi CAG, lamtaka akajieleze kwa Rais Magufuli'. Hakuna uamuzi wowote ambao Bunge hili limeufanya wa kumtupa CAG wala wa kumtaka CAG kwenda kujieze kwa Rais Magufuli. Azimio ambalo Bunge imelifanya ni la Bunge kutokufanya kazi, kwa kadiri ya ufanuzi wa Spika na Profesa Assad.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kitendo cha Gazeti la Fahari yetu kuandika kwamba, 'Bunge limemtupa rasmi CAG', habari hii kimsingi imeingilia haki za Bunge kwa sababu hakuna uamuzi wa Bunge hili ambao limeufanya wa kumtupa CAG. Pia kitendo cha gazeti hili kusema kwamba, 'Bunge limefanya uamuzi wa kutaka CAG akajieleze kwa Rais Magufuli', sisi hatujafanya uamuzi wowote wa kumtaka CAG akajieleze kwa Rais Magufuli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hiyo basi, naomba kutoa hoja kwamba suala hili lijadiliwe kwa kuwa limegusa haki za Bunge ili hizi taarifa za kwamba Bunge limefanya uamuzi wa kumtaka CAG akajieleze kwa Rais Magufuli zitupiliwe mbali na CAGaendelee kutekeleza wajibu wake wa kikatiba na Bunge lipewe haki ya kufanya kazi kama inavyotakiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla hamjaunga mkono hoja tufuate utaratibu wetu ambao tumejiwekea. Kama nilivyozungumza Mheshimiwa Mnyika amepewe fursa ya kuzungumza kama Kanuni ya 51

inavyozungumza. Ukiisoma fasili ya (3) na ya (4) inanitaka mimi niwe nimetazama hilo jambo na kuona kama ni jambo ambalo linaweza kupewa fursa ya kujadiliwa hapa ndani. Hata hivyo, fasili ya (2) inamtaka Mbunge aeleze kwa kifupi sababu zinazofanya aamini kwamba jambo analoliwasilisha linahusu haki za Bunge zilizotajwa kwenye Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, wote tumemsikia Mheshimiwa Mnyika, pengine kuna aliyemsikia akitaja kifungu gani kimevunjwa lakini mimi sjamsikia. Hata hivyo, wakati akitoa maelezo ameelleza mambo mengi pamoja na yale ambayo yanaelekea kwenye maamuzi ambayo Bunge hili lilikwishakufanya na hatuwezi kurudi huko mpaka hoja mahsusи kuhusu jambo hilo iwe imeletwa hapa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu taarifa aliyoleta Mheshimiwa Mnyika inazungumzia mambo ambayo yametajwa kwenye gazeti fulani ambalo mimi sijalisoma na sitaki kuamini kwamba Waheshimiwa Wabunge mmeshapata fursa ya kusoma ili jambo hili sasa tuweze kulijadili hapa ndani.

Kwa maana hiyo, tutachukua ule utaratibu wa kawaida wa kulipitia hilo gazeti kama yale anayoyasema Mheshimiwa Mnyika ndiyo yaliyoko kwenye lile gazeti, utaratibu wetu wa Bunge wa kuchukua hatua dhidi ya chombo au mtu ambaye anakuwa amelivunja haki zake na heshima yake utafuatwa. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge kwenye hoja hii tutafuata utaratibu huo na mtatangaziwa baada ya gazeti hilo kusomwa na kuona hatua gani tutazichukua baada ya haya. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo tunaendelea na utaratibu wetu, Katibu.

NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwa wa Fedha 2019/2020 - Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi Umma na Utawala Bora

(Majadiliano Yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano yetu. Tutaanza na Mheshimiwa Susan Kiwanga dakika tano, atafuatiwa na Mheshimiwa Pascal Haonga dakika tano.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi wa kwanza, hasa nikiwa kwenye Kwaresma hii na wiki hii ambayo ni ya mateso ya Bwana wetu Yesu Kristo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na utawala bora katika hii wiki ya mateso, tumesikia kwenye vyombo vya habari Mkuu wa Majeshi alikuwa anamwambia Rais Magufuli kwamba ye ye aachiwe kazi anachunguza mambo ya uchochezi kwa wanasiasa kwa kauli ambazo zinaenda kuvunjisha amani. Sasa katika utawala bora nataka Serikali inipe majibu, je, Mkuu wa Majeshi wa nchi hii amekuwa DPP? Anasema anafanya uchunguzi ye ye anajingiza moja kwa moja kwenye siasa? Y44eye ndiyo nataka kuiingiza nchi katika matatizo makubwa. Nakemea kwa nguvu zote na ashindwe katika Jina la Yesu. *(Makofi)*

WABUNGE FULANI: Amen. *(Makofi)*

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda katika masuala ya TAMISEMI kwa sababu nina dakika tano, niende moja kwa moja kuhusu masuala ya walimu.

TAARIFA

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, dakika zangu ni tano tu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jenista.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu kumpa taarifa ili tuliweke suala hili vizuri. *CDF* hakusema kwamba anachunguza wanasiasa, ye ye alizungumzia masuala ya amani, utulivu, ulinzi na usalama kwa ujumla wake na hakusema wanasiasa, ni lazima tuliweke vizuri jambo hili. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, wakati mwingine kauli zile hasa ambazo hatuna uhakika, zinazohusu viongozi wengine...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU SPIKA: Tusikilizane vizuri, hasa ambazo hatuna uhakika nazo tuwe waangalifu kwa sababu mimi nilikuwepo na alisema wanafuatilia siyo wanachunguza. Kwa hiyo, ndio maana nasema tuwe waangalifu, sisi wenyewe ni viongozi na kauli wanazotoa wengine tunapotaka kuzisema kwa namna fulani tuwe na hakika na kile kilichosemwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Susan Kiwanga, endelea.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nadhani umenilindia muda wangu. Hata kama nimekosea kusema lakini kufuatilia, ye ye kwa mujibu wa Katiba anaafuatilia masuala ya watu mbalimbali hapa nchini? Je, *DPP* atafanya kazi gani? Kifungu kipi cha Katiba

kinamruhusu yeye aseme anafuattilia wachochez? Yeye alinde mipaka bwana ya nchi yetu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu masuala ya walimu, katika vitabu vyao TAMISEMI wanasema wanaenda kuajiri walimu elfu nne lakini ndani ya Wilaya ya Kilombero tuna upungufu wa walimu 1,018. Kati ya hawa walimu elfu nne watakaoajiriwa, je, elfu moja na zaidi ndiyo wanaenda Kilombero na wilaya nyine watapata nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wajiri walimu, tumechoka kusubiri, elimu haisubiri. Watu wanazidi kuwa mambumbumbu huko chini, tunazidi kuliangamiza Taifa. Leteni haraka ajira za walimu na mishahara, posho na madaraja yao wapandishwe. Wafanyakazi nchi nzima hawajapandishwa madaraja, wanasoma lakini hawabadiishiwa mishahara. Naomba TAMISEMI na Utawala Bora mshughulikie masuala haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyakazi nchi nzima hawajapandishwa madaraja, wanasoma lakini hawabadiishiwa mishahara. Ninaomba katika Utawala Bora na TAMISEMI mwelekeze hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu masuala maalum. Ndani ya Jimbo la Mlimba kuna masuala mengi ambayo yanahu TamISEMI. Kuna madaraja kuhusu TARURA. Naomba TARURA waongezewe hela ili tupate kujengewa madaraja na barabara katika maeneo yetu, kwa sababu tumechoka kusubiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuhusu masuala ya maji, pale Mlimba hakuna maji, kuna kisima kimoja tu na ule mji unazidi kukua. Kwa hiyo, tunahitaji maji ya kutosha ili wananchi wapate maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la Mlimba, ni mji. Ndani ya Jimbo la Mlimba kuna mji kadhaa ambayo inakua ovyo ovyo. Ilishatamkwa kwamba kuna Mji Mdogo wa Mlimba, lakini mpaka leo unatamkwa vijiji. Katika bajeti

hii na uchaguzi unaokuja, tunaomba Mlimba tusitoe tena vijiji, tunataka tuchague vitongoji. Kwa hiyo, TAMISEMI nawaomba chonde chonde angalau mtupe mji mmoja wa Mlimba ili tuone tunapanga vizuri mji wetu usiwe ovyo ovyo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu masuala ya uendeshaji wa miji midogo. Sasa kama Mlimba hakuna miji midogo, miji haipangwi tutaendeshaje hiyo miji. Kwa hiyo, naomba chonde chonde haya mambo yafanyike. Nitafurahi sana na wananchi wa Mlimba watafurahi sana kama mtatangaza Mji Mdogo wa Mlimba uanze kazi katika Serikali ya Mitaa hii inayokuja, wachague vitongoji siyo viji tena. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu masuala ya Tume Huru ya Uchaguzi. Tume Huru ya Uchaguzi ni muhimu sana. Kiatu usichovaa huwezi kujuia kinabanje. Nimeshuhudla mwenyewe kule Malinyi, Sophy, Mkurugenzi anamtangaza Diwani wa CCM aliyeshindwa kwa kula 29 anamtangaza wa CCM anamwacha wa CHADEMA. Mpaka leo nina kesi Mahakamani. Ili kuvunja soo, wakanikamata wakanipeleka mahabusu ili nisifuatilie hiyo kesi Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, huo utawala bora sisi ndio tunaumia, sio ninyi mlioko upande huo. Nilisikitika sana na Kwaresma hii, ndugu yangu Mheshimiwa Jenista akisema Tume iko huru, sijui nini. Uhuru gani? (*Makof!*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda wako umekwisha Mheshimiwa. Ahsante sana. Mheshimiwa Pascal Haonga, Mheshimiwa Waitara ajandae.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naomba na mimi niweze kuchangia kidogo, lakini naomba nianze na suala la vitambulisho vya ujasiliamali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka labda njue kwa sababu Serikali iko hapa, kwa sababu mchakato wa vitambulisho vyta wajasiliamali halikulewa Bungeni, tumeona Mkuu wa Nchi, Rais amewaita Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya Dar es Salaam amewapatia vitambulisho na kwenda kuvipeleka kwenye Mikoa au kwenye Wilaya ili waende kuza shilingi 20,000/=. Sasa swali langu ambalo naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha atuambie, kitambulisho kimoja kilitengenezwa kwa shilingi ngapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ambalo nitaomba anijibu baadaye atakapokuwa anahitimisha, atuambie Mheshimiwa Rais alipokuwa anasema kuanzia wajasiliamali wa mtaji wa shilingi milioni nne kushuka chini, alikuwa anamaanisha kwamba kushuka chini hadi shilingi ngapi? Je, hata mwenye mtaji wa shilingi 500/= naye anahuksika? Kwa sababu kuna akina mama ambao wanaiza nyanya mafungu mawili; ana mtaji wa shilingi 1,000/= leo anaambiwa akalipe kitambulisho cha shilingi 20,000. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mama mwinge anaiza nyanya chungu, ana mtaji wa shilingi 500 anaambiwa naye aliipe kitambulisho cha shilingi 20,000/=. Sasa je, ilikuwa shilingi milioni nne hadi shilingi ngapi? Hapa Mheshimiwa Waziri atatuambia. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ambalo naomba Mheshimiwa Waziri atuambie, je, tenda ilitangazwa ili kupata yule atakayetengeneza vitambulisho? Kama tenda hii ilitangazwa, ni nani alireshinda? Kama tenda haikutangazwa, tafsiri yake ni kwamba kuna makosa yanayofanyika inawezekana vitambulisho vyta ujasiliamali likawa ni dili la mtu na Bunge sisi tusijetukatumika kama *rubber stamp* kuitisha mambo ya mtu binafsi. Kwa hiyo, tenda ilitangazwa? Nani alireshinda tenda hii? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine niseme tu kwamba ukweli ni kwamba sisi wote tunafahamu ukienda leo kule Mbozi kwa mfano pale Mlowo au ukaenda kule Kijiji

Igambo au Hampangala akina mama wanahangaika sana. Hii imekuwa kama ni kodi ya kichwa imerudishwa. Leo mama mmoja anauza nyanya kwenye nyumba moja, anaambwiwa ali pe shilingi 20,000/=; baba anauza miwa, anaambwiwa ali pe shilingi 20,000/=, mtoto mw ingine anauza bamia, ali pe shilingi 20,000/=, mtoto mw ingine anauza nyanya chungu shilingi 20,000/=. Nyumba moja shilingi 80,000/=. Sasa hii ni zaidi ya kodi ya kichwa. Kama Serikali imeleta kodi ya kichwa, wawaambie Watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, najua wewe unatoka kule Rungwe, wapo akina mama wanaohangaika. Kama leo wamerudisha kodi ya kichwa Bunge hili liwaambie kwamba kodi ya kichwa imesharudishwa na hii Wabunge hatutakuwa tayari kukubali suala hili la kodi ya kichwa kurudishwa kwa mara nyingine tena. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, leo Serikali ilisema kwamba itapeleka shilingi milioni 50 kila kijiji. Badala ya kupeleka shilingi milioni 50 ya kila kijiji, imeenda kuwadai watanzania wote shilingi 20,000/=. Kwa sababu kama Serikali iliahidi shilingi milioni 50, kwa nini hazijapelekwa? Badala ya kuzipeleka, imeanza kuchukua shilingi 20,000/= kwa kila Mtanzania, kwa sababu nchi hii imewaambia hadi wapiga debe, makonda, wanaoziba pancha za baiskeli, kila mtu. Sasa hali hii ni mbaya sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, amezungumza dada yangu hapa Mheshimiwa Suzan Kiwanga, naomba haya maneno ya kuhusu ndugu yangu Jenerali Mabeyo Mkuu wa Majeshi, nimeyanukuu hapa; ili mkisema kwamba kama kuna ushahidi, nimeyanukuu yapo hapa na ushahidi upo. Katika baadhi ya maneno yake alisema kwamba, "ndani ya nchi yetu kwa kushirikiana na vyombo vingine, tutawalinda wananchi na mali zao, tutakabiliana na matishio ndani ya nchi yetu na sasa hivi tunaendelea kufuatilia kauli tata zinazoashiria uchochezi na machafuko ndani ya nchi yetu." (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kulinda wananchi na mali zao ni kazi ya Jeshi la Polisi, siyo kazi ya Jeneral Mabeyo. Siyo kazi yake hii. Maana yake kama anataka uteuzi kuwa /GP, atuambie ili Rais amwondoe kwenye nafasi yake... (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: ...ya Mkuu wa Majeshi ampeleke kuwa /GP. Maana yake hii siyo kazi yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ye ye kazi yake ni kulinda mipaka ya nchi hii. Siyo kazi hii... (*Makofi*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda wako umekwisha Mheshimiwa. Ahsante sana.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Lushoto lina zaidi ya shule za msingi 33 nasekondari 26 za Serikali, lakini katika shule hizi kuna changamoto nyingi kama:-

(i) Ukosefu wa nyumba za walimu wa shule ya sekondari na msingi;

(ii) Ukosefu wa *hostel*/katika sekondari zetu;

(iii) Fedha za ukarabati wa shule za msingi za Kilole, Kwemashai, Malibwi, Kwembago, Ngulwi, Ubiri, Milungui, Kwemakame na Yogoi;

(iv) Kumalizia maabara zilizojengwa kwa nguvu za wananchi;

- (v) Upungufu wa walimu wa shule ya msingi na sekondari;
- (vi) Walimu kutolipwa posho zaonakuwekewa miundombinu rafiki;
- (vii) Watumishi kutopandishwa madaraja; na
- (viii) Ukozefu wa fedha za kumalizia maboma yote ambayo hayajakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kuwasilisha.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuchika namheshimu na kumwamini sana. Hoja yangu niviporo vya *TASAF II*, Kata ya Bungulwa kuhusu ujenzi wa barabara ya Bungulwa Nhundya; yapo makalvati zaidi ya 50 kwa zaidi ya miaka 10 lakini hakuna kinachoendelea. Nataka majibu ni nini hatma ya kiporo hicho au ndiyo imeshindikana? Hii si mara ya kwanza kuuliza swali hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majibu wakati wa kuhitimisha.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe na Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama na kutoa mchango katika hoja hii muhimu ya Makadirio ya Mapato na Matumishi ya Ofisi ya Rais, Utumishi kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja kwa sababu Serikali inafanya kazi nzuri ya utawala bora unaozingatia matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wengine kwa kazi nzuri wanayofanya na kwa kuandaa na kuwasilisha vizuri hotuba yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi, napenda kutoa ushauri katika maeneo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kuhusu uhaba wa wafanyakazi. Pamoja na kazi nzuri iliyoanywa na Serikali ya kuajiri wafanyakazi katika sekta mbalimbali kama ilivyoelezo kwenye hotuba ya Waziri bado tatizo la wafanyakazi ni kubwa sana na hasa katika sekta za afya, elimu na kadhalika. Nashauri Serikali iendelee kutafuta fedha kwa ajili ya kuajiri watumishi hasa katika sekta ya afya na elimu na hasa walimu wa sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili niwatumishi wa kujitolea. Nashauri Serikali ianzishe mpango wa wafanyakazi wa kujitolea katika kada mbalimbali kama ilivyokuwa ikifanyika zamani. Hii ni kwa sababu wataalam tunazalisha wa kutosha na hawana ajira, hivyo, wakipata hata kazi ya kujitolea wataendelea kuongeza maarifa na uzoefu na kutoa mchango kwa taifa na nafasi zikipatikana wao ndiyo wapewe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu ni kuhusu vibali vya kuajiri watumishi kupitia vyanzo vya ndani. Zipo taasisi ambazo zina uwezo wa kuajiri watumishi kupitia vyanzo vya ndani. Nashauri taasisi hizo zitambuliwe na kutoa nafasi za kuajiri watumishi kupitia vyanzo vya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne ni upekuzi kwa viongozi na watumishi (*vetting*). Zoezi la upekuzi kwa watumishi wanaostahili kuongezewa madaraka lifanyike kwa wakati ili kupunguza tatizo la upekuzi kufanyika kwa muda mrefu na hivyo Halmashauri nyingi kukumbwa na tatizo la kuwa na watu wanaokaimu. Zoezi la upekuzi liendelee kufanyika kwa umakini na uadilifu ili kutotoa mwanya kwa watendaji na viongozi wasio waaminifu na waadilifu kupenya na kupewa nafasi katika vyombo mbalimbali vya maamuzi na umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne ni mpango wa *TASAF*.Naungana na Kamati kuwa uhakiki wa kuondoa kaya

zisizostahili ufanyike kwa umakini na uadilifu mkubwa ili wasiostahili waondolewe na wanaostahili wanufaike na mpango wa kuhudumia kaya masikini ikiwa ni pamoja na kuongeza wigo kwa kaya zingine zinazostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano ni kuhusu TAKUKURU kudhibiti mali za umma. Napongeza TAKUKURU kwa kuendelea kufuatilia vitendo vya rushwa katika kutekeleza miradi ya maendeleo na katika taasisi za umma za kutoa huduma. Nashauri jitihada ziendelee ili kuokomesha vitendo vya rushwa na matumizi mabaya ya mali za umma ili nchi yetu iweze kufikia maendeleo tunayoyataka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. SILAFU J. MAIFI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pongezi za dhati kwa Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuwaletea maendeleo wananchi. Waziriwa TAMISEMI, Mheshimiwa Selemani Jafo, Naibu Mawaziri wake, Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu wanafanya kazi iliyotukuka na kwa ufanisi na maendeleo yaoonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri George Mkuchika na timu yake wamejitalidi kuweka hali sawa ya utawala bora na kutoa vibali vya ajira na kujaza nafasi za utumishi za kada mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu asilimia 10 ya mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu inayotoka ndani ya mapato ya Halmashauri zetu, kazi hii inaendelea ndani ya Halmashauri zetu kwa kiwango tofauti. Tunaomba Waziri, Mheshimiwa Jafo kwa umahiri wake kuona umuhimu wa kutoa usafiri wa pikipiki angalau kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Vijiji na Mitaa na ngazi ya Wilaya (Halmashauri) na Mkoa wapatiwe magari kuliko kutegemeahurumaya Wakurugenzi wao. Pia tunaomba ajira ya Maafisa Maendeleo ya Jamii, kwani wana kazi kubwa ya kuelimisha wananchi

hasa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kuunda vikundi vya ujasiriamali ili waweze kupata mikopo.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kuhusu malipo ya watumishi waliorejeshwa kwenye mfumo. Kuna watumishi ambao waliondolewa kimakosa kwenye *payroll/na baadaye* wakarejeshwa, hata hivyo, hawajalipwa malimbikizo yao. Mfano, Mafinga wapo watumishi 51 na jumla ya madai ni Sh.118,164,330na mpaka sasa hawajalipwa. Hali hii pia iko kwanchi nzima, naomba Serikali itusaidie watumishi hawa walipwe madai yao hayo.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu na wafanyakazi wote kwa kazi kubwa wanazofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya watumishi wa Urambo,nashukuru sana kwa vituo viwili vya afya. Ahsante sana, ni msaada mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wilaya ya Urambo ina kata 18 na kwa sasa tumepata vituo viwili vya afya, kwa heshima tunaomba vituo viwili vya afya kwenye kata zenye wakazi wengi na ziko kwenye barabara kubwa katika eneo la Songambele na Vumilia. Pia, tunaomba walimu na wafanyakazi wa afya ili wakafanye kazi kwenye vituo hivi, tunatanguliza shukrani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Urambo ni moja ya Wilaya inayonufaika na Mfuko wa Rais wa Kujitegemea. Wananchi wa Urambo wameufurahia sana huduma ya mikopo. Je, Serikali inawaambia nini waliokuwa wanaendelea kupata huduma za Mfuko huu ambapo ghafla wameambiwa umesitishwa?Wafanyaje kuhusu marejesho? Je, isingekuwa vizuri Serikali kuwapa nafasi wanufaika na wanafakazi kukamilisha mikopo kwa mfano isingeweza kutoa *noticena* kusema kuanzia mwaka wa fedha 2020/2021 hakutakuwa na Mfuko wa Rais? Je, Serikali haioni kuwa Mfuko

imesitishwa ghafla sana? Tunaomba Mfuko huu upewe muda wa kutosha ilivyo sasa ambapo taarifa imetolewa ghafla sana na masuala ya fedha hajakaa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Urambo wanashukuru sana huduma ya MKURABITA. Tunaomba MKURABITA iendeleze huduma zake za biashara na kurasimisha ardhi ili wananchi wanufaik kwa kupata hati. Aidha, tunaomba fedha ziongezewe ili MKURABITA ifanye kazi kwa ufanisi zaidi.

MHE.DKT. CHRISTOPHER K. CHIZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Wasaidizi wake wote kwa hotuba nzuri. Nimesikiliza hotuba kwa makini sana, imenikumbusha mambo kadhaa yanayohusu mawasiliano Serikalini *Standing Orders* na hata *Financial Orders (Stores Regulations)* nakadhallika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya LAAC. Katika kupitia hoja za ukaguzi za CAG zinazohusu Serikali za Mitaa na baada ya ziara ya kukagua miradi katika Halmashauri 12, nimejiridhisha kwamba Serikali inaweza kupunguza hoja za ukaguzi kama watumishi wanaopewa dhamana kuwa Maafisa Masuuli (*DEDs*) wangepata uelewa wa shughuli za Serikali. Watendaji wengi wakiwemo Wakuu wa Idara wapo wasiojua kanuni na taratibu za uendeshaji shughuli za Serikali. Baadhi yao hata hawajajua nini maana ya uwajibikaji na utunzaji wa siri za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kamani gharama kuwapeleka viongozi wa Serikali kufundishwa katika Chuo cha Utumishi Serikalini, nashauri Chuo na Maafisa Waandamizi wa Serikali wafanye semina hizo katika maeneo ya kazi. Athari ya kuwa nawatumishi wasiojua Miiko ya Utumishi (*The DO's and DON'Ts*) inaweza kuigharibu Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa George Huruma Mkuchika,

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora) pamoja na Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa kazi kubwa wanayofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naombawaangalie suala la watumishi wa afya walioajiriwa kihalali na Serikali baada ya kuwalegezea masharti ya ajira na ambao waliondolewa kwenye utumishi wa umma kwa kukosa sifa ya kumaliza kidato cha nne. Ni vyema watumishi hao wakarudishwa kazini ama kustaaafishwa na kulipwa mafao yao. Baadhi ya watumishi hao wapo wa kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo ambao wameleta malalamiko yao ya kutotendewa haki kwa Katibu Mkuu Dkt. Laurean Ndumbaro na nakala ya malalamiko hayo nilimkabidhi Mheshimiwa Dkt. Mary M. Mwanjelwa, Naibu Waziri. Watumishi hao wamekuwa wakipoteza nauli mara kwa mara kuja Dodoma kufuatilia majibu ya malalamiko yao na hivyo kujiongezea machungu na umaskini. Naomba suala lao lishughulikiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nikipokea vilio vya baadhi ya watumishi wa Serikali hususan wa TAMISEMI (Makao Makuu) wanaolalamikia maslahi duni. Wanasema wenzao wa kada moja walioajiriwa kwenye Taasisi za Serikali wanapata mishahara minono wakati wao walioajiriwa TAMISEMI mishahara wanayoipata haikidhi kabisa mahitaji ya msingi na hivyo kujikuta na madeni lukuki na kuendelea kuishi kwa kuombaomba. Wameniomba nifikishe killio chao kwa Mheshimiwa Rais kupitia Wizara hii yenyе dhamana na mishahara ya watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia 100 na naomba kuwasilisha.

MHE.JANETH M. MASABURI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapongeze Mawaziri, Naibu Mawaziri na watendaji wote kwa kazi nzuri wanayofanya chini ya uongozi wa Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Awamu hii ya Tano ya utawala wa Jemedari wetu Mkuu, Rais wetu mpandwa

Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, ameudhihirishia ulimwengu inaumahiri na uhodari, maarifa na umakini mkubwa wa kufanya mageuzi ya kiutendaji kwa watumishi wa umma na kupiga vita rushwa na ufisadi, uzembe kazini na uwajibishwaji wa viongozi wazembe. Kwa sababu hiyo na nyinginezo, nashauri kuwe na mfumo endelevu kwa awamu zote za utawala wa nchi utaozingatia uwajibikaji na uwajibishwaji watumishi wa umma ambao hawazingatii viwango vilivyopangwa ili kuleta tija kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itasaidia baada ya awamu hii muda wake wautawalakuisha. Nidhamu na mifumo hii iendelee bila kutupwa kapuni kama yalivyonupwa au kuachwa mambo mazuri ya Awamu ya Kwanza. Mazuri mengi ya Mheshimiwa Rais, Dkt. John Magufuli, Rais wa Tanzania hayapaswa kuachwa hata kidogo. Kizazi hiki kitahukumu iwapo Awamu zinazofuata zitasahau mazuri haya. Mungu ibariki Tanzania naviongozi wote, amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia 100.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumpongeza Waziri wa Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa *Capt.* Mkuchika; Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa; Makatibu wote wawili na Watendaji wa Wizara hii kwa kazi nzuri sana wanayoifanya na pia kwa kuwasilisha hotuba yao hapa ili tuweze kuijadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mkurugenzi wa *TASAF* kwa kazi nzuri aliyofanya katika Mkoa wetu wa Iringa. *TASAF*imefanya vizuri sana, imeweza kusababisha hali ya kaya masikini na kuwa na hali zenye unafuu wa maisha japokuwa mwanzoni kulikuwa na ukiritimba katika kuzibaini. Kuna baadhi ya watendaji walitaka kutumia kisiasa kaya za watu masikini na wale mavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Waziri wa Utumishi Mheshimiwa *Capt.* Mkuchika kwa kuitembelea kaya

masikini na yenye watoto walemavu zaidi ya watatu inayoishi katika Kijiji cha Lulami na kujionea jinsi ilivyo na kuiongezea kipato na kuipatia TV. Nilikuwa naomba kujua: Je, kaya masikini na yenye watoto wenye ulemavu kama hiyo, Serikali inawasaidiaje kuwapatia angalau mradi endelevu unaoweza kusaidia watoto wenye ulemavu kama hao ambao hawana hata uwezo wa kutembea kabisa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na tatizo kubwa sana la upandishwaji wa madaraja kwa Walimu na wanapopandishwa marekebisho ya mishahara hayafanyiki kwa wakati na kusababisha mpaka wakati mwingine Mwalimu anastaafu lakini mshahara wake unakuwa haujarekebishwa. Je, nini mkakati wa Serikali kwa changamoto kama hiyo? Hii inasababisha usumbufu mkubwa sana kwa wastaafu ikiwa ni pamoja na ucheleweshaji wa mafao yao wanapostaaifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na ucheleweshaji mkubwa sana kwa wafanyakazi wanapokaimu nafasi kuthibitishwa. Je, sheria inasemaje ili kumpatia haki mtu anapokaimu kwa muda mrefu?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. OTHMAN OMAR HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuzungumzia mishahara na maslahi katika utumishi wa Umma. Watumishi Serikalini wanakatishwa tamaa na maisha. Hii ni kutohana na kipato cha mishahara, hakikidhi mahitaji yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, punguzo la 11% hadi 9% linatekelezwa kwa wafanyakazi wenye mishahara ya kima cha chini. Kodi kubwa hadi kufikia asilimia 30 inaendelea kukatwa kwa wafanyakazi wenye mishahara ya kima cha juu. Wafanyakazi sasa hulazimika kutafuta kipato cha ziada kwa njia nyininge, jambo ambalo linaweza kuathiri uzalishaji na kupunguza pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu ajira katika utumishi wa Umma. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri hajitatueleza kiwango cha Watumishi wa Umma ambao wameajiriwa, lakini kuna taarifa kwamba kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2015 - Desemba, 2018 takribani vijana 594,300 waliomba ajira Serikalini, lakini ni vijana 6,554 sawa asilimia 1.1 pekee ndio waliopata ajira. Kwa mujibu wa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato (*TRA*) ya Desemba 10, 2018, taasisi yake ina upungufu wa wafanyakazi 1,930 ambapo athari yake ni ucheleweshwaji wa ukusanyaji wa kodi. Baadhi ya Wilaya wameshindwa kufungua ofisi na Serikali inakosa mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni mpango wa kunusuru kaya masikini. Wazee wetu walio wengi ni masikini na Serikali yetu ilijipiga kifua kuwa watatoa shilingi bilioni 66.5 kwa ajili yao. Inasikitisha kuona Serikali hili inajisifu kuwa inatetea wanyonge (Serikali ya wanyonge) kwamba tokea ilipoingia madarakani (2015) mpaka tarehe ya leo imetoa shilingi bilioni 1.35 kati ya shilingi bilioni 4.35 zilizotolewa tokea kuasiwiwa kwa mpango huu hapo mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utawala bora, Tanzania ni mionganoni mwa nchi 16 za Afrika na ndiyo nchi pekee Afrika Mashariki iliyokataa kutia saini na kuridhia Mkataba wa Umoja wa Afrika unaohusu demokrasia, uchaguzi na utawala bora (*ACDEG*). Mkataba huu unalenga kuchochaea mijadala mionganoni mwa wadau wanaotetea utawala bora na demokrasia Barani Afrika. Kama haitoshi, Tanzania pia imejiondoa katika makubaliano ya kuondokana na kasumba ya kuendesha mambo kwa siri kati ya Serikali na wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya Tanzania kujitoa katika mpango wa uendeshaji wa shughuli za Serikali kwa uwazi na ukweli (*Open Government Partnership*) inazua wasiwasi kuhusu utekelezaji wa Sera ya Uwazi. Kutohana na hatua hizo, inaonyesha kwamba Tanzania imekusudia kuendeleza kuminya demokrasia na uhuru wa watu wake kutoa maoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora aya ya 37(xii), madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi wa Umma 34,346 yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 79 inaonyesha hayajalipwa mpaka sasa. Hata ya shilingi bilioni 29 ambayo yamehakikiwa nayo hayajalipwa mpaka sasa. Serikali iache kutumia kisingizio cha uhakiki mwingine wa Wizara ya Fedha kuendelea kuchelewa kuwalipa wafanyakazi madai yao ya mishahara. Hivyo katika majumuisho, Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge, ni lini hasa madai hayo ya wafanyakazi yatalipwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika aya ya 51 na 78 zinazohusu Bodi ya mishahara na maslahi katika utumishi wa Umma, zinaonesha kwamba Serikali hajafanya maamuzi ya kupandisha mishahara ya watumishi wa Umma. Bado Serikali inajificha katika kivuli cha kufanya utafiti wa hali ya maslahi ya watumishi wa Umma na kuandaa taarifa za gharama za maisha, kukwepa kupandisha mishahara ya watumishi wa Umma. Visingizio kama hivi vimetolewa katika hotuba za 2016/2017, 2017/2018 na 2018/2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo ni vyema ripoti ya utafiti iliyotajwa kwenye aya ya 51 na taarifa mbili za gharama za maisha ziwasilishwe Bungeni na Bunge katika majumuisho ya mjadala wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora itangazwe kwamba mishahara ya watumishi wa Umma itaongezwa katika bajeti hii ya mwaka wa fedha 2019/2020. Pia ili kukabiliana na gharama za maisha, ni vyema Serikali ikawapunguzia mzigo wafanyakazi wote wa Sekta ya Umma na Binafsi kwa kupunguza kiwango cha kodi ya mapato kwa wafanyakazi (*PAYE*) kama ilivyowaahidi wafanyakazi kwa nyakati mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu agizo la Serikali la watumishi wa Umma wa Wizara na Taasisi zake kuhamia Dodoma. Kuna umuhimu kwa Ofisi ya Rais

Menejimenti ya Utumishi wa Umma na wakala zilizo chini yake kufanya utafiti juu ya athari za maamuzi hayo yaliyofanyika bila maandalizi ya kutosha kwa maisha ya watumishi wa Umma. Watumishi wa Umma walipokuwa Dar es Salaam wapo ambao wenzi wao wanafanya kazi katika sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dodoma Sekta Binafsi haijapanuka kwa kiwango cha kuwezesha wenzi wa wafanyakazi hao nao kuweza kuhamia Dodoma kwa haraka haraka. Matokeo yake ni kuwa, kuna familia nyingi zimetengenishwa hali ambayo italeta athari za muda mrefu na kuathiri utendaji wao kwa kipindi cha muda mfupi. Aidha, kwa wafanyakazi wa kada ya chini na kati, hali hii ya kuwa na Miji miwili; Dar es Salaam na Dodoma kwa mishahara yao midogo, imeleta madhara ya kiuchumi kwa watumishi wa Umma.

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mungu kwa fursa hii ya kuwepo hapa kujadili hotuba hii ya Wizara muhimu sana katika kuchangia na kukuza maendeleo ya Taifa letu. Nakushukuru kwa fursa ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa George H. Mkuchika, Mbunge wa Newala na Waziri katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, Katibu Mkuu na Watendaji wote na taasisi zote zilizo chini ya Wizara hii kwa kazi kubwa wanayofanya kuhakikisha kuwa utendaji wa Serikali ni mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuipongeza Serikali kwa utekelezaji mzuri wa mpango wa kurasimisha rasilimali na biashara za wanyonge (MKURABITA). Mpango huu ni muhimu sana kwa kuhakikisha kuwa wananchi wote wenye uwezo wanajumuishwa kwenye uchumi wa nchi kwa kuwawezesha kutumia rasilimali za kukopa au kuwekeza kiuchumi. Kwa umuhimu wa mradi huu na faida na mafanikio yaliyopatikana hadi sasa, tunapenda kuona Serikali ikizidisha juhudui katika kuwekeza fedha nyingi zaidi kuthamini na kutoa

hati nyingi zaidi nchi nzima hasa kule ambako fursa za kiuchumi ni kubwa na utayari wa wananchi kuchapa kazi ni kubwa pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta isiyo rasmi ni kubwa sana na ina mchango mkubwa katika kuondoa umasikini, kuongeza ajira na kuchangia pato la Taifa. Kwa hiyo, MKURABITA upanuliwe na uenee nchi nzima kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TASAF*, naipongeza Serikali sana kwa mpango huu wa ruzuku kwa kaya masikini. Mpango umeonesha matokeo mazuri sana. *TASAF* ipo sasa awamu ya tatu na inatekeleza mpango wa kunusuru kaya masikini kuanzia mwaka 2013. Kumekuwa na mafanikio makubwa kwa kaya zilizoandikishwa na kupata ruzuku. Maisha yao yameboreshwa na wanashiriki vizuri katika shughuli za kiuchumi kuweza kuongeza kipato zaidi katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua mpango huu haukuwafikia masikini katika vijiji na mitaa yote na pia katika vijiji ambavyo vimefikiwa, kuna kaya nyingine masikini hazikuridhishwa kwa sababu mbalimbali. Kwa mfano Wilaya ya Ileje, kati ya vijiji 71 ni 50 tu zilizofikiwa. Vijiji 21 bado havijafikiwa. Sasa ni lini hizi kaya masikini zitaingizwa kwenye mpango? Ninapata maswali mengi kutoka Jimboni kwangu kwa wapiga kura wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya uendelevu wa mpango huu: Je, kuna mikakati ipi ya ufadhili wa mpango huo? Kwa sababu sehemu kubwa ya fedha zinazotumika ni michango ya wadau wa maendeleo na Serikali inachangia kidogo, tunaona hata katika bajeti Serikali inatoa kidogo na sehemu kubwa ni fedha ya nje. Je, ikikosekana?

Mheshimiwa Naibu Spika, watumishi wa Umma wengi bado wanafanya kazi kwa mazoea. Wengi hawabebi haya maono ya Mheshimiwa Rais na wala hawaendani nayo. Hii inazorotesha watendaji, inapunguza tija na huzidisha gharama. Iko haja kuhakikisha kuwa Chuo cha Utumishi

kinajikita zaidi katika mafunzo yaliyokuwa yakinolewa kwa watumishi wa kada ya kata ili kuwajengea uwezo wa jinsi ya kutekeleza majukumu yao Serikalini, kuwa na weledi wa masuala mbalimbali ya utumishi wa Umma. Hii itasaidia katika kuboresha ufanisi wa watumishi wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, huko nyuma Chuo cha Mzumbe kilitumika kutoa mafunzo yaliyojenga uwezo wa Watendaji Wakuu wa Taasisi za Umma, lakini walipoamua kukigeuza kuwa chuo cha kawaida na kupoteza fursa ya kuwajengea uwezo viongozi wa Mashirika ya Umma. Kwa sababu hiyo, ninapendekeza ufanywe utaratibu wa kutumia Chuo cha Uongozi (*Institute*) kutoa mafunzo ya Watendaji Waandamizi kabla ya kupangiwa taasisi za Umma kuziongoza. Hii itasaidia kuongeza ufanisi wao na kuboresha huduma za wateja wao na kuvutia uwekezaji, uzalishaji kwa jumla na kuongeza mapato ya Serikali na kukuza uchumi kwa jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukuzaji wa taaluma, kukidhi ubora unaotakiwa, kuongoza taasisi zetu, uzingatiwe na hii iendane na suala zima la uteuzi wa watumishi wenyewe vigezo na watakaopewa viashria vyta kutumika kuwapima. *Vetting* ya wateule wa taasisi inachukua muda mrefu na kusababisha kuzorota kwa kazi za Serikali na Mashirika yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, rushwa imepungua na kama inafanywa, kwa kiasi kikubwa watu wanajificha, lakini bado zile taasisi zilizoendeleza rushwa kama Polisi, Mahakama, Mamlaka ya Kodi, Hospitali na ambako rushwa bado inafanywa bila kificho. Ili kupunguza rushwa kubwa, tunaishauri Serikali ipunguze kutoka shilingi bilioni moja ili iwezeshe watu wengi zaidi wanaojihuisha na rushwa kupelekwa kwenye Mahakama ya Ufisadi na kupunguza vitendo vyta rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, watendaji waliokuwa wanafaidika na mfumo uliokuwa unatoa mwanya wa rushwa wameamua kufanya kazi kwa kukomoa na kula rushwa kwa kisingizio cha Hapa Kazi Tu na hawa wamekuwa wakiharibu

jina la Serikali na kuwapaka matope viongozi wetu. Iko haja ya kutupia jicho eneo hili kama *TRA*, Taasisi na Idara za huduma muhimu za Serikali zinazotoa vibali, leseni na kadhalika. Serikali ijjitahidi kueneza mifumo ya *TEHAMA* ili kupunguza mawasiliano ya watu na watendaji hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri hajazungumzia lolote juu ya Watanzania walio ughaibuni kama sehemu yenyeye fursa ya utumishi wa Umma. Kwa bahati mbaya Watanzania wengi wamekuwa na mtazamo hasi dhidi ya Watanzania walioko ughaibuni, lakini mimi ninaamini kuwa tukiwa na utaratibu mzuri wa kuwatumia ni hazina kubwa kwa Taifa letu na wengi wanapenda kurudi kufanya kazi Tanzania wakipewa nafasi. Nchi nyingi hata za jirani wamewatumia sana raia wao walio ughaibuni na kunufaika na weledi na ujuzi wao. Wakati umefika kubadilisha mtazamo wetu juu ya wenzetu walioko kwenye *Diaspora* ili wachangie maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Mheshimiwa George Mkuchika, pia Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Mkurugenzi wa *TASAF* kwa kazi nzuri ya kusaidia kupunguza makali kwa wananchi walio masikini, angalau kwa sasa wanakula milo mitatu, watoto wanaenda shule na wanawake wengi wamepeleka watoto *Clinic*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa awamu ya tatu isaidie walengwa ambao wamefanikiwa kujikwamua kwa maendeleo ili wale ambao hawakuingia awamu ya kwanza na ya pili, kutoa nafasi nao wawezeshwe. Pongezi kwa kutafuta wafadhili wenye mikopo nafuu ili kusaidia maendeleo kutoptana na bajeti kuwa finyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni MKURABITA. Serikali iongeze bajeti ya maendeleo ili kupunguza migogoro ya

ardhi, pia wananchi waweze kupata hati za kimila na kuweza kukopa. Serikali iendelee kufuatilia fedha za maendeleo za mwaka 2018/2019 ili zitolewe kabla ya Juni, 2019 zifanye kazi iliyokusudiwa. Hata hivyo, naomba MKURABITA ibuni jinsi ya kupata wafadhili kwa kuandika michangonuo ya mikopo yenye riba nafuu kama walivyofanya *TASAF* kwa kutegemea Serikali hawajafikia malengo waliyokususidiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iangalie jinsi ya kumaliza suala zima la watumishi wanaokaimu kwenye ofisi mbalimbali, kupandisha madaraja kwa wale wanaostahili, uhakiki na madeni ya watumishi yafanyike haraka, vibali vyaa ajira vitoke haraka kwenye Wizara mbalimbali kutoekana na wahitaji ili watumishi waajiriwe hasa katika huduma ya afya na elimu.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nichukue fursa hii nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa siku ya leo. Nichukue fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa na nzuri anayofanya yeye na Serikali yake. Vile vile naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Kapteni Mkuchika na Naibu wake, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, Katibu Mkuu na timu yake nzima kwa kazi nzuri wanayofanya. Naomba kushauri baadhi ya masuala ili kuboresha huduma na hasa katika Utumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni suala la *OPRAS*; ni muhimu sana jambo hili lisisitizwe ili uadilifu na uwajibikaji uwe wa hali ya juu. Pia naomba Wizara iboreshe Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, sekretarieti hii hufanya kazi nzuri na kubwa, ingetumika pia kwa ajili ya ajira kwa taasisi za watu binafsi iwe sehemu ya kuwa benki ya wanaotafuta ajira. Wote wanaohitaji ajira waweze kuweka rekodi zao pale na wenyewe kuhitaji watumishi basi wapate orodha kutoka Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nashauri suala la watumishi wanaokaimu kwa muda mrefu utoke mwongozo na pawe na kanuni juu ya nafasi ya kukaimu; Babati Vijijini

tunao wakuu wa idara wanaokaimu zaidi ya saba. Pia Serikali iangalie suala la kukaimisha watumishi bila utaratibu na inaleta gharama kwa halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la huduma kwa mteja (*customer charter*); suala hili likumbushwe kila wakati na itangazwe kwa wananchi, kila idara, taasisi iweke wazi suala la huduma kwa mteja (*customer charter*). Nashauri pia Sekretarieti ya Maadili ya Umma pia iweze kuweka mfumo wa kielektroniki ili tuweze kujaza fomu hizo kwa njia ya kielektroniki na pia tukihitaji kupata taarifa zingine na kujaza taarifa muhimu tuweze kujaza kwa njia ya kielektroniki (*update information*). Nashauri pia kuwa na mfumo mpya wa urasimishaji wa uendelezaji wa biashara (*One Stop Center*) hii itasaidia kupunguza gharama urasimu na muda wa kupata huduma.

MHE. MAFTAHA A. NACHUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, suala la utawala bora ni pamoja na Serikali kushirikisha wananchi. Nchi hii ina mfumo wa ushiriki wa wananchi kupitia wawakilishi wanaochaguliwa na wananchi wenyewe. Wawakilishi hao ni Wenyeviti wa Mitaa, Madiwani, Wabunge pamoja na Rais wa Jamhuri ya Muungano na Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kushangaza sana kumekuwepo na mpango wa makusudi wa kuzuia wawakilishi kufikisha kero za wananchi pale viongozi wa Kitaifa wanapotembelea maeneo yetu, kwa mfano Mtwara Mjini, Novemba 6 mwaka jana, mwaka 2018, tulizindua Mji Mkongwe wa Mikindani ambapo mgeni rasmi alikuwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Hasunga, lakini jambo la kushangaza Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Mtwara alikataa mimi Mbunge wa Jimbo kusalimia wananchi katika mkutano nilioshiriki kwa kiasi kikubwa kuwaomba wana Mtwara Mjini kushiriki uzinduzi huo, hali iliyosababisha wananchi wengi kuchukia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipomuuliza Mkuu wa Mkoa kwa nini hanipi nafasi, alisema kwa mdomo wake kuwa, hivyo ndivyo tulivyopanga kama hujaridhika fanya unavyojuia

wewe. Kama Mbunge niliumia na kauli ya Mkuu wa Mkao kwani alitaka mimi nibishane naye ili apate *kick* ya cheo chake. Niliamua kukaa kimya nikafikisha kwenye kikao na Mheshimiwa Waziri akasema kweli haikuwa sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 2 Aprili, 2019 Mheshimiwa Rais alikuja Mtwara Mjini kufungua miradi kadhaa, siku mbili kabla tulipewa ratiba ya ziara hiyo. Tukiwa kwenye uwanja wa mukutano, *Airport Mtwara*, nilimuuliza Mkuu wa Mkao kuhusu utaratibu wa Mbunge wa Jimbo ambaye ni mwenyeji kuhusu ukaaji, kusalimia na kumpokea Mheshimiwa Rais pale aliposhuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika kusema kuwa, Mkuu wa Mkao, Mkuu wa Wilaya na baadhi ya Wabunge wa chama tawala walikataa mimi Mbunge mwenyeji:-

- (a) Walinizuia kwenda kumpokea Mheshimiwa Rais badala yake wakawekwa watu wa CCM na yeze mwenyeje Mkuu wa Mkao na Mkuu wa Wilaya tu wakati mimi ni Mbunge mwenyeji;
- (b) Mkuu wa Mkao wa Mtwara akanizuia hata kukaa viti vya nyuma ya Rais, kama Mbunge mwenyeji, wakasema huruhusiwi kukaa huku hata kama ni Mbunge, viongozi wa CCM wamepewa nafasi; na
- (c) Mkuu wa Mkao akanizuia hata kusalimia wananchi wangu na kumkaribisha Mheshimiwa Rais, kama Mbunge mwenyeji. Mbaya zaidi nilipouliza kwa nini mnamzuia Mbunge aliyechaguliwa na wananchi wengi, wakaniambia ungekuwa CCM ungepewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaomba kujua utawala bora tunaozungumza ni wa aina gani? Kwani huyu Mkuu wa Mkao wa Mtwara na DC wa Wilaya ya Mtwara hawajui kama nchi hii ni ya vyama vingi na Mbunge wa Jimbo ni kiongozi halali kikatiba? Naomba kujua kwa nini umlazimishe mtu kuhama chama?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mbunge wa Jimbo la Mtwara Mjini nimeamua kufanya siasa safi kwa kuwa, nataka amani na utulivu Mtwara Mjini na Kusini kwa ujumla. Haya yanayofanywa na Mkuu wa Mkoaa na *DC* kwa utashi wake noamba yakomeshwe mara moja maana nguvu ya Mbunge wa Mtwara Mjini kwa wananchi ni kubwa sana, nddio maana nikifanya mikutano Wananchi wananiitika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kama humuhitaji Mbunge wa *CUF*, lakini ndio kawekwa na wananchi wa Mtwara Mjini, lazima apewe heshima na haki yake kama mimi ninavyowaheshimu *RC*, *DC* na Wabunge wote wa CCM nawaheshimu sana. Naomba tuendelee kutunza heshima hii na amani ya Mtwara kwa kuheshimiana, kama wote viongozi wa wananchi.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii siku ya leo kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuendelea kuniweka hai na afya njema na leo kunipa uwezo wa kutoa mchango wangu kwenye hoja hii. Pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais Mheshimiwa Dkt. John J.P. Magufuli kwa kuliongoza Taifa letu kwa uadilifu mkubwa na kwa umahiri anaouonesha katika kusimamia rasilimali ya nchi yetu ili ilete manufaa kwa Watanzania wote. Uongozi unaozingatia, Katiba, usawa, haki, sheria na utu. Jambo linaloendelea kudumisha amani ya nchi yetu. Kwani hivyo ndivyo vielelezo vyta amani yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nianze mchango wangu kwa kuishauri Serikali katika mambo yafuatayo:-

Kwanza, Watumishi wa Umma; kumekuwa na uhaba mkubwa sana ya watumishi katika Idara mbalimbali za Sekta ya Umma kama vile afya, elimu, ugani, Mahakama na kadhalika. katika idara nydingi za umma watumishi wengi wamekuwa wakikaimu, nafasi mbalimbali za utumishi, nafasi hizi wanakaimu kwa muda mrefu kiasi cha kuwapunguzia

ufanisi katika suala la upungufu wa watumishi. Mfano Wilaya ya Liwale ina upungufu kama ifuatavyo:-

- (a) Walimu shule za Msingi upungufu 298;
- (b) Afya zahanati na vituo vya afya 261; na
- (c) Maafisa Ugani upungufu ni 28.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hawa wachache waliopo, kuna ucheleweshaji mkubwa wa kupandishwa madaraja na pale wanapopandishwa madaraja mishahara mipya huchelewa kutolewa. Hivyo kupelekea Serikali kuwa na madeni mengi au makubwa.

Pili, ni *TASAF*; nashauri Serikali kufanya utafiti wa kutosha ili wale walionufaika na kuonekana wameshatoka kwenye kaya maskini ili waweze kuondolewa na wengine kupewa hizo nafasi, kwani bado ziko kaya nyngi zenyenye uhitaji hazijafikiwa na utaratibu huu. Vilevile Serikali ione umuhimu wa kuendelea kushirikisha wanufaika wa *TASAF* kwenye kubuni miradi mbalimbali, kwani iko miradi iliyoshindwa kufikia mafanikio tarajija kutokana na miradi kutokuwa shirikishi kwa wanufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika dhana ya utawala bora Serikali ione umuhimu wa mafunzo kwa wateuliwa wapya juu ya majukumu yao. Uzoefu unaonyesha mara wateule hao wanapotekeleza majukumu yao wengine wanashindwa kujua mipaka ya majukumu yao. Aidha, Serikali ione umuhimu wa kuimarissha au kuboresha Chuo cha Utumishi wa Umma, sambamba na hilo kuwe na utaratibu wa kila mtumishi wa umma awe amepitia kwenye Chuo hicho hata kwa angalau miezi mitatu (3) iwe mara baada ya kuajiriwa au kuteuliwa kwa nafasi au ajira husika. Kama ilivyo kwa Chuo cha Utumishi wa Umma vilevile Serikali ione umuhimu wa viongozi kwenye ngazi mbalimbali wawe pia wamepata mafunzo ya uongozi. Kozi au mafunzo hayo, yatawajengea watumishi au viongozi hao kufanya kazi kwa uzalendo, utaifa na ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba Idara ya Polisi na Mahakama kuonekana ina tatizo kubwa la rushwa, lakinrushwa iliyoko kwenye Idara ya Uhamiaji ni ya hatari zaidi na idara hii rushwa zake ni ngumu sana kuzigundua, pamoja na madhara yake ni makubwa sana. kama ilivyo kwa Idara ya Uhamiaji, vilevile Idara/Wizara ya Uwekezaji inakuja kwa kasi kubwa sana jambo linalopunguza ari kwa wawekezaji wa ndani na nje. Hivyo nashauri Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini kutupia macho sana taasisi hizi mbili nilizozitaja hapo juu. Sababu ya kutamalaki kwa rushwa kwenye Taasisi hizi ni kutokana na sababu kuu mbili:-

(1) Upungufu wa watumishi kwenye idara hizo; na

(2) Urasimu mkubwa uliopo unaotokana na watumishi wengi kushindwa kutoa maamuzi hata yale yaliyo chini au ndani ya uwezo wao, hivyo kufanya hali ya njoo kesho, njoo kesho zinakuwa nydingi na kutengeneza mazingira ya rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, napenda kutoa pongezi kwa wateule wote katika Wizara hii wakiongozwa na Waziri mwenye dhamana pamoja na Naibu wake, bila kusahau, viongozi wa taasisi zote zilizo chini yake, kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kulitumikia Taifa hili kwa weledi mkubwa. Kazi hii ya kutukuka inathibitishwa na amani na utulivu uliopo hapa nchini. Kwani ni jambo lililo wazi hakuna amani wala utulivu, mahali ambapo hakuna utawala bora.

Mungu ibariki Tanzania, Mungu ambariki Rais Mheshimiwa Dkt. John J. P. Magufuli.

MHE. JORAM I. HONGOLI: Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa uongozi wake wa kutukuka kwa Watanzania. Nawapongeza pia Mawaziri, Mheshimiwa Suleiman Saidi Jafo na Kapteni Mstaafu Mheshimiwa George H. Mkuchika na Manaibu Waziri wote Mheshimiwa Josephat Kandege, Mheshimiwa Mwita

Waitara na Mheshimiwa Dr Mary Mwanjelwa kwa kazi kubwa wanazozifanya usiku na mchana kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuendelea kuboresha miundombinu ya Shule za Msingi na Sekondari. Shule nyingi za msingi zimepatwa na ongezeko kubwa la wanafunzi, udahili wa wanafunzi wa darasa la kwanza umeongezeka. Ongezeko hili limesababisha upungufu mkubwa wa madarasa, hivyo, Serikali iongeze fedha za ujenzi wa madarasa. Wananchi hasa wa maeneo ya vijiji ni hawana uwezo wa kumudu kujenga madarasa mfano katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, shule nyingi hasa zilizojengwa zamani hazina madarasa ya kutosha, naiomba Serikali itusaidie au ituongezee fedha za ujenzi wa madarasa hata kwenye shule zilizojenga nyuma ya miaka ya 1970. Mfano wa shule kongwe ni Sovi (1950s), Lupembe (1950s) na Kanikelele (1970). Majengo ya shule hizo za msingi yamechoka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa sekondari ni muhimu sana shule zetu za sekondari za katiki, kujengwa mabweni kwa ushirikiano wa Serikali na wananchi. Shule nyingine za kata hazina mabweni na majengo mengineyo muhimu kama vile majengo ya utawala na mabwalo ya chakula. Uwepo wa majengo hayo huongeza ufaulu wa wanafunzi. Wanafunzi wanakuwa huru kusoma wanapoishi bwenini na ufaulu wao huongezeka. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe shule ambazo hazina mabweni ni Shule za Sekondari ya Ninga, Ikuna na Mlunga, Kidegembye (bweni la wavulana), Lupembe (mabweni yaliyojengwa zamani (yamechakaa), Sovi (bweni la wavulana) na Itipindi (hakuna mabweni ya A-level).

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukusanyaji wa Mapato; Halmashauri nyingi hazikusanyi mapato au zinakusanya chini ya makadirio, Halmashauri nyingi zinakusanya chini ya asilimia hamsini hii inatokana na:-

Moja inawezekana kuna uzembe wa ukusanyaji mapato na kupelekeea kukusanya chini ya kiwango; au Pili, inawezekana wataalam waliopo katika Halimashauri zetu wanashindwa kubuni miradi ambayo itawaingizia kipato cha uhakika sambamba na hali ya Halmashauri zao au kutegemea vyanzo hivyo bila kutabiri uendelevu na vyanzo hivyo. Mfano wa Halmashauri za Mikoa ya Katavi, Kigoma, Mtwara na Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TASAF*; naipongeza Serikali kwa kuendelea kuzisaidia kaya zenye kipato kidogo kupata mahitaji ya msingi na kuwawezesha kujkwamua kwenye wimbi la umaskini kupitia mpango wa *TASAF*. Kuna baadhi ya vijiji havukuingizwa kwenye mpango wa *TASAF*, tunaomba vijiji hivyo viingizwe kwenye mpango huu ili kuondoa malalamiko. Mfano, katika Halimashauri ya Wilaya ya Njombe kuna Kijiji cha Sovi killirukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Barabara Vijiji na Mijini (*TARURA*), wanafanya kazi kubwa sana. Watanzania zaidi ya asilimia 75 ni wakulima, kwa hivyo barabara za vijiji ndiyo tegemeo kubwa sana kwa wakulima hawa. Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ina jumla ya barabara za vijiji zenye urefu wa kilomita 582. Eneo la Jimbo la Lupembe, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ni eneo la uzalishaji wa mazao mbalimbali kama vile chai, kahawa, miti ya mbao na nguzo, mahindi, maharage, nanasi, parachichi na mihogo. Mazao mengi kati ya hayo huzalishwa wakati wa mvua nyngi na ni kipindi hicho barabara hizo huharibika sana na kukwamisha shughuli za uzalishaji na usafirishaji wa mazao hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili barabara hizi ziweze kufikika na mazao kufikia kufika sokoni, ni muhimu kutenga fedha za dharura ili kufanya matengenezo ya muda kwenye barabara hizi hasa kwenye maeneo yenye mvua nyngi kama Jimbo la Lupembe. Mwaka huu kutokana na mvua kubwa ilioanza kunyesha Mwezi Februari, mpaka sasa barabara nyngi hazipitiki. Kuna baadhi ya maendeo hata madaraja yamekatika mfano barabara ya Lole – Maduma na

Kidegembye – Image. Madaraja ya barabara hizi yanatakiwa kujengwa upya, hivyo ni muhimu Serikali kuwaongezea bajeti Wakala wa Barabara Mijini na Vijiji (TARURA) ili kusaidia kuchochea uchumi wa halmashauri na mkoa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja za Wizara zote mbili.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, atafuatiwa na Mheshimiwa Josephat Kandege.

NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Hoja ni nyingi lakini nitajaribu kuititia zile ambazo nitaweza ndani ya muda huo na nyingine kila Mheshimiwa Mbunge ambaye ametoa mchango wake kwenye eneo hili tutampa majibu ikiwezekana kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja katika michango ya Waheshimiwa Wabunge ilikuwa inazungumzia Watumishi wa Umma ambao wanakaimu kwa muda mrefu. Naomba tuwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba hoja hii tumeipokea, tunatoa maelekezo kila ngazi ya Serikali za Mitaa wakusanye taarifa zao wazilete ili wale watu ambao wanakaimu kwa muda mrefu na wanakidhi vigezo, basi waweze kuthibitishwa kazini ili waweze kufanya kazi kwa umakini zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, tunafajamu kwamba tuna upungufu wa wahandisi katika Halmashauri zetu, ni kweli, wahandisi wengi walipelekwa TARURA, lakini jambo hili limeshachukuliwa na Serikali linafanyiwa kazi ili tupate wahandisi hasa wa majengo na waweze kusimamia miradi mbalimbali ambayo kwa kweli kwa awamu hii ya tano miradi mingi Serikali imepeleka fedha ujenzi wa vituo vy'a afya, nyumba za viongozi wetu wa Wilaya na mikoa. Kwa hiyo, hili jambo limechukuliwa litafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa mchango wa Mheshimiwa Mbunge mmoja, alijaribu kutoa maelezo ya kupotosha ya elimu msingi bila malipo. Naomba niseme tu kwa watanzania wote na Waheshimiwa Wabunge kwamba kwa kweli kama kuna jambo kubwa ambalo Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli amefanya, ni maamuzi thabiti ya kuruhusu elimu msingi bila malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na wanafunzi wengi waliopata fursa ya kusoma na gharama imekuwa ikiongezeka. Tumepanda kutoka shilingi bilioni 249 sasa mwaka huu wa fedha tunaozungumza ni shilingi bilioni 288 elimu msingi bila malipo. Hili siyo jambo la kubeza, ni jambo la kumpongeza Mheshimiwa Rais na Watanzania wana macho wanaona; na masikio na nina uhakika wataendelea kumuunga mkono katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna madai yamezungumzwa hapa ya Waheshimiwa Madiwani na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa. Jambo hili limesemwa kwa upana na uzito. Tumelichukua Ofisi ya TAMISEMI linafanyiwa kazi na baada ya muda siyo mrefu sana litapata muafaka na naamini kwamba kero hiyo itakuwa imeondoka. Kwa hiyo, linafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchangajie ambaye amemaliza sasa hivi amezungumza kama wengine ambavyo wamesema habari ya madarasa, nyumba na mambo mbalimbali ya miundombinu ya elimu, lakini ukweli ni kwamba Serikali ya Awamu ya Tano ya Chama cha Mapinduzi imejitahidi sana kuboresha miundombinu ya elimu. Changamoto nyingi ilikuwa tunajaribu kuboresha maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2019 kwa mfano, tulikuwa na shida ya magari, hapa tunafanya mchakato wa kununua magari 26; kila mkoa Maafisa Elimu wa Mikoa watapata magari mapya kabisa ili waweze ku-move kutoka eneo moja kwenda lingine kusimamia suala zima la elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika bajeti hii ambayo tumezungumza tutanunua magari 40 tena ambayo yataelekezwa kwenye ngazi ya elimu sambamba na kujenga nyumba za Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Makatibu Tarafa. Ukiangalia kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI utaona imezungumzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumejenga madarasa 4,400, matundu ya vyoo zaidi ya 8,000, maabara 22, tumepeleka fedha mwezi wa Pili hapa shilingi bilioni 29; tupo kwenye mchakato wa kupeleka shilingi bilioni 34 kwenda sasa kukamilisha maboma ya shule za msingi. Zaidi ya maboma 2,000 yatafanyiwa kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na hoja hapa ambazo zimezungumzwa, naomba niseme tu, mwingine alisema nitaje uwezo wangu, nisiwe nachangia kama Naibu Waziri. Nijibu na nianzie hapa hapa nazungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, demokrasia ambayo inazungumzwa katika nchi hii mimi siielewi. Mheshimiwa Msigwa sijui kama yupo humu ndani. Mheshimiwa Msigwa wakati anagombea Uenyekiti wa Kanda, walienda wakaondoa wagombea wa CHADEMA akabaki peke yake. Pamoja na hayo, walipowaondoa alienda akapata kura asilimia 48 za hapana. Huyo ndio Mheshimiwa Msigwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa mlimsikia Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kambi Rasmi ya Upinzani anazungumza kwamba leo mafisadi ambao wamekamatwa kudhulumu Taifa hili, leo anasema waondolewe wasichukuliwe hatua. Huu ndio ulikuwa wimbo wao wa siku zote. Kwa kweli katika mazingira haya hatuwezi kukubaliana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza ukaona, hivi Mkuu wa Majeshi ambaye anaangalia ulinzi wa nchi hii, hutaki atoe kauli juu ya ulinzi wa nchi hii kweli! Kama kuna chokochoko ndani za kichochezi, anaachaje? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Selasini ni Mjumbe wa Kamati ya Utawala na TAMISEMI, amekuwa kwenye vikao vyote vya Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, naomba nimpongeze Mheshimiwa Selasini, ametoa michango mizuri sana. Wakuu wa Mikoa ambao walikuwa na matatizo ambao hatukatai, tumezungumza nao, tumetoa maelekezo na wamebadilika. Alikuwa na malalamiko ya Mfuko wa Jimbo, tumeongea na Mkurugenzi, imeisha. Haya mambo ya jumla jumla hayatakubalika. Kama kuna mtu ana kesi *specific, case by case* alete tuchukue tuifanyie kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo chetu cha Hombolo Kimetoa semina kwa mafunzo mbalimbali. Niseme kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi ipo kazini na kwa kweli siasa ni kupambanisha hoja siyo vioja. Tumeshuhudia kwenye Bunge hilli, wenzetu wana vioja, CCM wana hoja, chapeni kazi. Huo ndiyo ukweli na Watanzania wanaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, inawezekanaje Mbunge anasema patachimbika. Hivi hao Watanzania mnaowazungumzia, ni hawa tunaokaa nao sisi au nyie ndio mnajua! Kama patachimbika, mtakuwepo, tutakuwepo. Huu mchezo dakika 90 haziishi, hao Watanzania tupo nao wote. Kwa hiyo, maneno kama hayo ya kuchochaea watu, kuandaa kifujofujo, Serikali haiwezi kuruhusu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka tupate hoja za wanasiasa makini kama akina Mheshimiwa James Mbatia, wanatoa hoja hapa mtu unafurahi, akina Mheshimiwa Selasini na wengine. Wale ambao hawataki kufanya siasa kwa vyama hivi; leo amekuja Prof. Pierre Lumumba, anasema *Magufulification of Africa*, yaani Rais wa Tanzania, John Pombe Magufuli anakuwa referred Afrika nzima. Huyu ni Rais wa mfano. Miradi ambayo ameitoa ni ya kimkakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Chama cha Mapinduzi mna huruma sana. Miradi pale Rombo tumepeleka, Iringa inajengwa lami, Tarime kuna mpango wa kimkakati, soko liko pale zaidi ya shilingi bilioni kadhaa, Majimbo yamepewa

fedha mbalimbali, watumishi wamepelewa; mnataka nini ndugu zangu wa upinzani? Mnataka mpewe nini? Gunia la chawa! (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka niwashauri ndugu zangu wa Upinzani kwa kazi hii inayofanyika ya Chama cha Mapinduzi, ilitakiwa tupange vizuri namna ya kutoa hoja. Mahali pa kukosoa ukosoe vizuri, wala siyo kutukana... (*Makofi*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha. Mheshimiwa Josephat Kandege atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa.

NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niwe mmojawapo ambao wamepata fursa ya kuchangia hoja na kupata fursa ya kujibu baadhi ya hoja ambazo zimeletwa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kipekee nianze kwa kushukuru kamati yetu ya Utawala na TAMISEMI kwa maelekezo ambayo wamekuwa wakitupatia lakini pia Waheshimiwa Wabunge katika michango yao yote ya kujenga. Kama kuna Wizara ambazo zimetendewa haki ni pamoja na Wizara yetu. Kwa ujumla nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja ya kuhusiana na TARURA ambayo imeongelewa na Waheshimiwa Wabunge wengi kuanzia kamati yetu, lakini pia Kambi Rasmi ya Upinzani imeongelea juu ya suala zima la TARURA kuongezewa fedha, lakini kama siyo kuongezewa fedha, pia wameongelea suala zima la kutaka mgawanyo wa fedha utazamwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika na Waheshimiwa Wabunge wote ni mashuhuda, hali tulioanza nayo kuhusiana na suala zima...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Hawanisikilizi eeh!

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe ni shuhuda jinsi ambavyo tulianza Waheshimiwa Wabunge wengi walikuwa wanalamikia jinsi ambavyo utendaji kazi wetu wakati matengenezo ya barabara yalikuwa chini ya Halmashauri. Kila Mheshimiwa Diwani na Wabunge sisi tukirudi kule ni Madiwani, kila mmoja alikuwa anaomba kipande angalau kilometra moja kitengenezwe. Kwa hiyo, *value for money* ilikuwa haionekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tupokee pongezi ambazo tumepokea kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge juu ya utendaji bora wa *TARURA*. Wengi wamesifia juu ya chombo hiki, lakini ni ukweli usiopingika kwamba tuna safari ya kuhakikisha kwamba tunaimarisha *TARURA* ili ule upungufu ambao Waheshimiwa Wabunge wamesema uweze kurekebishiha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ni ukweli usiopingika kwamba kilometra ambazo zinahudumiwa na *TARURA*, chombo hiki ambacho tumekianzisha sisi wenyewe, takribani kilometra 108,000 ni nyingi. Pia wameomba ikiwezekana mgawanyo ubadilike kutoka asilimia 30 kwa 70. Zipo sababu za msingi kwa nini tulikwenda kwenye hiyo *formula*? Nasi Serikali tumesikiliza kwa Waheshimiwa Wabunge, imeundwa Tume ambayo inafanya tathmini kupitia upya ili pale ambapo tukija na majibu ya uhakika tushirikishe Bunge letu katika kuwa na *formula* ambayo itahakikisha kwamba *TARURA* inafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna suala zima la ukosefu wa vitendea kazi ikiwepo magari. Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeliona hili na ninaomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba tumeanza kununua magari ili kuhakikisha maeneo yote ambayo hakuna gari ziweze kufikishwa. Tumeanza na gari 22 katika kipindi kilichopita na safari hii tunaenda kununua gari 22. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge maeneo yote ambayo yana uhitaji mkubwa wa magari tutayazingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala zima la ujenzi na ukarabati wa vituo vya afya. Kipekee naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tumeweza kupata kiasi cha shilingi bilioni 100.5 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa vituo vya afya na hospitali. Tumeanza na hospitali 67 na Waheshimiwa Wabunge wote ni mashuhuda kwamba katika bajeti ambayo tutaomba baadaye watupitishie tunaenda kuongeza tena hospitali 27. Ni kazi kubwa na nzuri; ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kwamba huduma ya afya inasogezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba waheshimiwa Wabunge tusaidiane tuhakikishe kwamba tunasimamia malengo ambayo tumeweka Ofisi ya Rais TAMISEMI kufika tarehe 30 mwezi Juni, yale majengo saba yawe yamekamilika na wananchi wa Tanzania waanze kupata huduma ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hilo halitoshi, pia tunaenda kuongeza hospitali nyingine 27. Fedha imetengwa na ninaamini muda siyo mrefu Waheshimiwa Wabunge watapitisha ili tuweze kwenda kujibu kijibu kiu kubwa ya Watanzania kuhakikisha kwamba wanapata huduma ya afya umbali usiokuwa mrefu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala zima ambalo napenda niongelee kidogo kuhusiana na usafiri wa mabasi ya mwendokasi kwa Dar es Salaam. Hili limechangiwa sana na Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaam. Naomba niwahakikishie azma ya Serikali ya kuhakikisha

kwamba msongamano wa usafiri kwa Dar es Salaam unapungua, iko pale pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mchakato ambao tulikuwa tumeanzisha wa kumpata mwendeshaji wa mwanzo ambaye kwa mujibu wa mkataba *interim operator* ilikuwa a-*oparate* na mabasi 140, lakini ndani ya mwezi huu Aprili tutahakikisha kwamba kandarasi inatangazwa na ukifika mwezi wa nane Mwenyezi Mungu akijaalia tutakuwa tayari tumeshampata mkandarasi wa kuendesha mabasi hayo na yataongezeka kutoka mabasi 140 mpaka mabasi 305. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, naomba niwahakikishie kwamba mchakato tutahakikisha unakwenda vizuri. Kama hiyo haitoshi, tunaenda kujenga barabara ya kuanzia katikati ya Mji wa Dar es Salaam kwenda *Kilwa Road* kwenda Gongolamboto kwenda Tegeta. Ni azma ya Serikali ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kuhakikisha kwamba wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam wanapunguziwa adha ya usafiri kwa maana ya msongamato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hilo halitoshi, kuna suala zima la *DMDP*, naomba niwahakikishie Wabunge na hasa Wabunge wanaotoka Dar es Salaam, tupo vizuri tumejipanga muda siyo mrefu wao wenye watajionea jinsi ambavyo mchakato unakamilika na barabara hizi zinaanza kutengenezwa ili kuhakikisha kwamba Dar es Salaam inaendelea kuwa mahali salama pa kuishi na wananchi kufurahia matunda ya chama chao cha CCM.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala zima limeongeleta kuhusiana na asilimia 10 ambayo inatakiwa itolewe kwa ajili ya akinamama, vijana na watu wenye uhitaji maalum kwa maana ya watu wenye ulemavu. Wewe ni shuhuda kwamba tumepitisha sheria, kwa hiyo ni takwa la kisheria kwa Wakurugenzi wote kuhakikisha kwamba wanatenga asilimia 10 kutohana na mapato yao ya ndani. Tayari kanuni zilishakuwa tayari, muda wowote ndani ya

mwezi huu kanuni zitakuwa zimetoka, kwa hiyo Mkurugenzi yeoyote hatakuwa na kisingizio kwa nini hatengi hizo fedha na kuhakikisha kwamba fedha hizo zinakwenda kuwafikia Watanzania tulio wakusudia, ikiwa ni akinamama, vijana na watu wenye ulemavu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mengi, naomba ni wahakikishie Waheshimiwa Wabunge wote, kila Mbunge ambaye alitoa hoja yake tutajibu kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukru sana kwa muda wako. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mary Mwanjelwa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nichukue fursa hii kukushukuru wewe binafsi, lakini kwa sababu leo ni mara yangu ya kwanza na ni bajeti yangu ya kwanza, nimshukuru sana Jehova, lakini nimshukuru Mheshimiwa Rais pia kwa kuendelea kuniamini na kunipa nafasi hii nimsaidie kwenye eneo hili. Nimshukuru pia Waziri wangu, Mheshimiwa Kapteni Mstaafu George Huruma Mkuchika, kwa kunipa ushirikiano mzuri na vilevile kunipa mwongozo mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajibu kwa ufupi, lakini nichukue fursa hii pia kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia kwa mdomo na vilevile wale waliochangia kwa maandishi katika hotuba yetu au bajeti ya ofisi yetu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Vilevile niishukuru Kamati yetu ya Bunge na niombe tu kusema kwamba yale yote ambayo yamechangiwa kwa maandishi, kwa mdomo tumeyapokea tumeyachukua na tutayafanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ufupi kabisa kama nilivyosema nitayajibu kwa pamoja nikianza na lile la kukaimu. Leo asubuhi nimejibu hapa suala hilohilo la kukaimu kwamba

kuna watumishi wengi, kuna viongozi wengi wanakaimu kwa muda mrefu. Ukweli ni kwamba wamekuwa wakikaimu kwa muda mrefu kutokana na kwamba hizi nafasi huwa wanakaimishwa kule na waajiri wao kienyeji tu, unakuta kwamba huyu anampenda basi anaona ni bora akakaimu kwenye hiyo nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba, kuna waraka kabisa umetumwa mwaka jana Septemba, 2018 kwamba nafasi zote zile za kukaimu lazima zipate kibali kutoka Utumishi na kukaimu kwenyewe kusizidi miezi sita. Kukaimu ni nafasi ya muda, sio kwamba maana yake wewe utathibitishwa au tayari umeshateuliwa, hapana. Kwa hiyo niwatake waajiri wote nchini kuhakikisha kwamba wanafuata sheria, kanuni na taratibu wanapokuwa wanakaimisha wale viongozi kule katika maeneo yao ya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kwa ufupi ni kuhusu watendaji wakuu kuhamahama na watumishi kwenda kwenye ofisi zao nytingine. Naomba niliambie Bunge lako Tukufu kwamba watendaji wakuu kuhama na watumishi hiyo sio sahihi kwa sababu utumishi wa umma ni *obedience*, utumishi wa umma ni utii, kokote kule unakokwenda, kwanza ukipewa *transfer* unatakiwa kufanya kazi mahali popote utakapokuwa umepangiwa, lakini vilevile na kule unakokwenda na kwenyewe kuna watumishi wa umma. Kwa hiyo sio vizuri kusema kwamba unahamahama na watumishi, utawakuta kule na wao sana sana unachotakiwa kufanya ni kuwajengea uwezo ili na wenyewe waweze kuwa ni watendaji wazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu muda wa likizo ya uzazi; naomba niseme mimi pia ni mama, tunaelewa adha ya kujifungua. Likizo ya uzazi, naomba niseme, sisi kama Serikali katika zile siku 84 tumeongeza siku 14 zaidi, lakini tunaelewa kama wanawake *consequences* za kujifungua mtoto zaidi ya mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine lilirozungumzwa ni idadi ya wanawake ile 50 kwa 50. Katika utumishi wa umma,

naomba niseme kinachoangaliwa ni sifa, vigezo, ubunifu na umahiri wako wa kazi na vilevile je, unaendana na ubunifu na kasi ya Serikali tullyopo, sio tu kwamba eti kigezo chako kitakuwa kwa vile ni wewe ni mwanamke, kuwa mwanamke ni sifa ya ziada endapo kuna maeneo mawili labda umechuana na mwanaume lakini sasa wewe kwa sababu ni mwanamke basi hapo unapewa *priority*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ndugu zangu wanawake sote tunaelewa sisi ni jeshi kubwa, tuendelee kujiamini, tunaweza tukipewa, kubwa la msingi na sisi tunapobebwa tuoneshe kwamba tunabebeka. Hili sizungumzii masuala ya Madiwani na Wabunge, nazungumzia katika utendaji kazi kwenye utumishi wa umma na wanawake ni jeshi kubwa. Kwa hiyo tukibebwa lazima tuoneshe tunabebeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kutowapandisha watumishi mishahara. Hili suala lilikuwa limesitishwa kutokana na sababu mbalimbali, lakini sisi kama Utumishi, naomba niliambie Bunge Iako Tukufu kwamba vijana wetu wa kizalendo, vijana wetu wa Kitanzania tumekuwa tukitumia ule Mfumo wa *Lawson, Version 9*, lakini sasa hivi hawa vijana wetu wa Kitanzania wanaleta mfumo mwingine mpya ambao una nguvu zaidi, *capacity*yake ni kubwa zaidi na gharama zake ni ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu mfumo tutaanza kuutumia kuanzia Juni na naomba niseme katika mfumo huu tutakuwa tumeboresha mambo mengi sana; masuala kwa mfano yale ya *OPRAS*, utendaji kazi Serikalini, watu wamekuwa wakifanya kazi kimazoea. Kwa hiyo ule Mfumo wa *OPRAS* ambao tutakuwa tumeuanzisha kutokana na mfumo wetu huu, wenyewe utasaidia kuziba mianya ya upendeleo, lakini vilevile kuziba mianya ya chuki, kwamba mwingine kwa vile anampenda fulani basi anamwongeza cheo au mwingine kwa sababu hujamsalimia asubuhi basi hakupendekezi. Kwa hiyo mfumo huu utakuwa ni wa kuongeza ufanisi katika utumishi wa umma. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kwenye mfumo huu pia tunatarajia kuanzisha *One Stop Centre* katika maeneo yote ambayo yanatolewa huduma na utumishi wa umma. Tunategemea kuanzisha *One Stop Center* ili kusiwe na Mtanzania yeyote, mwananchi yeyote wa Kitanzania ambaye yuko katika Serikali ya uadilifu ya Awamu ya Tano kwamba asafiri kutoka Kigoma mpaka kwenda Mwanza, kwa hiyo *One Stop Center* kuitia mfumo huu itakuwa imeanzishwa katika mkoa mmoja na huduma zote atakuwa anazipata mahali pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie suala la utumishi wa umma; michango mingi imetoka hapa na sote tunaelewa kwamba Chuo cha Utumishi wa Umma ni chuo nyeti na naomba niliambie Bunge lako Tukufu kwamba watumishi wa umma wote wanaoajiriwa kwa mara ya kwanza, nitoe rai, hata kwa waajiri, wote nchini kuhakikisha kwamba wanapitia kwenye Chuo chetu cha Utumishi wa Umma, hii ni *mandatory*wala sioombi na wale wote ambao watakiuka maagizo haya watachukuliwa hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu unapopita kwenye Chuo cha Utumishi wa Umma kule kuna mambo mengi ambayo inabidi tufundishwe; jinsi gani ya kutunza siri za Serikali, jinsi gani ya kuwa na uadilifu, jinsi gani ya kuwa na uzalendo na mambo kama hayo. Kwa hiyo naomba nitoe rai kwa waajiri wote nchini kuhakikisha wale wote wanaoajiriwa wanapita kwenye Chuo cha Utumishi wa Umma ili kupikwa kama watumishi wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja na ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwanza kabisa naomba nitambue uwepo wa Mheshimiwa Charles Kitwanga. Tunamshukuru Mungu kwamba umerejea salama na tunafurahi kukuona, karibu sana. (*Makofi*)

HOJA YA KUSITISHA BUNGE KABLA YA MUDA WAKE

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 28(2) na kwa mujibu wa taratibu zetu ambazo huwa tunazo nimemaliza majina niliyokuwa nimeletewa hapa kwa ajili ya wachangiaji wa asubuhi na Kanuni hii na fasili hii inanitaka niwahoji Waheshimiwa Wabunge kabla sijasitisha shughuli za Bunge kabla ya saa saba, kwa hiyo nitawahoji.

*(Hoja Iilitolewa lamuliwe)
(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

NAIBU SPIKA: Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni leo.

(Saa 4.50 Asubuhi Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudi)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Majadiliano yanaendelea sasa tutamsikia mtoha hoja, Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Mheshimiwa Waziri una dakika 45.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda sana kumshukuru Mwenyezi Mungu, muumba mbingu na ardhi kwa kuniwezesha kutoa hoja yangu hapa Bungeni ya hotuba ya Bajeti Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii kukupongeza wewe Naibu Spika lakini kumpongeza Spika wetu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Job Ndugai kwa kazi kubwa mnayofanya. Pia

niwashukuru sana Wenyeviti wote wa Kamati za Bunge kwa weledi, ufanisi na kwa kazi kubwa waliyofanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi kwa nafsi ya moyo wangu napenda sana kumshukuru Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani yake kubwa kwangu kunipa Wizara hii kubwa ambayo bajeti yake ni zaidi ya asilimia 18 ya bajeti yote ya nchi, Mheshimiwa Rais nakushukuru sana. Nimshukuru Makamu wa Rais, mama yetu Samia Suluhu Hassan, halikadhalika nimshukuru Waziri wetu Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kwa uongozi wake mahiri sana ambao unatuwezesha kufanya kazi zetu kama Mawaziri ambapo yeye anatengeneza timu hiyo kama kiongozi wetu hapa hapa Bungeni na Serikali kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimshukuru sana Mwenyekiti wetu wa Kamati, Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijiini kwa uongozi wake mahiri akisaidiwa na Mheshimiwa mama Mwanne Mcemba, Makamu Mwenyekiti, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Tabora kwa watani wangu Wanyamwezi, nawashukuru sana. Pia naishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na TAMISEMI kwa kazi kubwa waliyofanya katika kipindi hiki chote wakati tunaendelea na mchakato huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Capt. Mkuchika, Waziri pacha mwenzangu katika Ofisi ya Rais, kwa ushirikiano mkubwa aliotupatia. Vilevile niwashukuru Naibu Mawaziri wangu; Mheshimiwa Joseph Kandege na Mheshimiwa Mwita Waitara kwa ushirikiano mkubwa walionipatia. Pia nimshukuru Katibu Mkuu wangu *Engineer Nyamhanga* na Naibu Makatibu Wakuu wote Tixson Nzunda na dada yangu Dorothy Gwajima. Niwashukuru sana watendaji wote wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ushirikiano mkubwa na dada yangu Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumshukuru Dkt. Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango lakini Ndugu yangu Dotto James kwa ushirikiano mkubwa sana walio tupatia katika utekelezaji ya bajeti ya mwaka 2018/2019 na katika mpango wetu wa bajeti ya mwaka 2019/2020. Kwa hakika sisi tumejivunia, kwa kweli kazi imeenda vizuri sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jedwali tulilowasilisha hapa, napenda kufanya marekebisho kidogo katika kiambatanisho katika ukurasa 158 hadi 159 kinachohusu ujenzi wa vituo vya afya 52 katika mwaka wa fedha 2019/2020 kama ifuatavyo: Kituo cha Mapera katika Halmashauri ya Mbinga kihamishiwe katika Kituo cha Afya Nangirikiri na Kituo cha Afya cha Kabwe kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi kihamishiwe kwenda Kituo cha Afya cha Ninde katika Halmashauri hiyohiyo ya Nkasi. Halikadhalika katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Kituo cha Afya cha Ikuna kihamishiwe kwenda Kituo cha Afya cha Kichiwa na katika Halmashauri ya *Kasulu TC*, Kituo cha Afya Kigadye kiende Heri Juu katika Halmashauri ya Kasulu Mji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Fungu 56 - Ofisi ya Rais, TAMISEMI limeongezewa shilingi bilioni 33 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ambayo inaenda *TARURA*. Baada ya kusikiliza kilio cha Wabunge humu ndani, Serikali imeona vyema iongeze takribani shilingi bilioni 33 ambayo kwa kiwango kikubwa inaenda kutatua matatizo ya wananchi wetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kutokana na hali hiyo, kuna baadhi ya mafungu katika Fungu 56 yatakuwa na mabadiliko. Kwa mfano, kutasomeka shilingi 496,563,123,910 katika Fungu la Maendeleo badala ya shilingi 463,563,123,910. Hivyo, kufanya Fungu 56 katika Miradi ya Maendeleo na Matumizi ya Kawaida kuwa na shilingi 550,200,093,910. Kwa maana hiyo, bajeti nzima ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI itakuwa na jumla ya shilingi 6,240,992,779,769. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya marekebisho hayo, sasa naomba kuwatambua Waheshimiwa Wabunge 130 waliochangia bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI; wakiwemo Wabunge 86 waliochangia kwa kuzungumza na Wabunge 44 walichangia kwa maandishi. Naomba niwashukuru sana kwamba hoja yangu imechangiwa na Wabunge wengi na hii inanipa ishara kwamba Ofisi ya Rais, TAMISEMI ni eneo ambalo tunapata huduma kwa ujumla wake. Kutokana na maelezo yetu ya kikanuni, naomba majina hayo nisiyasome ila naomba yote yatambuliwe katika *Hansard* za Bunge kama Waheshimiwa Wabunge walivyochangia kuhakikisha kwamba Ofisi hii inatekeleza vizuri wajibu wake. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hakika Ofisi yetu ilikumbana na hoja nyingi lakini hoja hizo zimegawanyika katika maeneo yafuatayo: Posho za Madiwani, Wenyevit wa Vijiji na Vitongoji; kujenga uwezo wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; uchaguzi wa Serikali za Mitaa; mgawanyo wa fedha wa Mfuko wa Barabara zilizotengwa kwenda kwenye Halmashauri (*TARURA*); ushiriki wa wadau; utekelezaji wa Mradi ya Mabasi yaendayo Haraka lakini ujenzi na ukarabati wa hospitali za halmashauri pamoja na vituo vya afya na zahanati; ununuzi wa vifaa tiba katika hospitali zetu na vituo vya afya; miundombinu ya elimu; ajira za walimu wetu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; vyanzo vya mapato vya Halmashauri na maeneo mengine kadhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi nishukuru sana michango katika maeneo hayo yote lakini niwashukuru sana Naibu Mawaziri wangu asubuhi waliweza kujibu baadhi ya hoja na wamezitendea haki sana. Niwashukuru sana wapiganaji hawa mahiri sana hasa ndugu yangu Mheshimiwa Waitara na Ndugu yangu Mheshimiwa Kandege, kwa kweli wamefanya kazi kubwa sana. Kwa hiyo, mimi nitaenda kimuktadha, kwa upana mkubwa tu wa Ofisi hii jinsi gani inafanya kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo ambalo limezungumzwa ni suala la vitambulisho vya wajasiriamali, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa nia yake

njema kwa wafanyabiashara wadogo wadogo waliokuwa wakitaabika ambapo sehemu nyingine walikuwa wanakamatwa na Mgambo, wanapigwa virungu na kunyang'anywa vyakula vyao, hali yao ilikuwa ni taabani. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa maono yake ya kuwajali Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili nimesikia hoja za Wabunge mbalimbali wakisema kwamba inawezekana nia ikawa ni njema lakini utaratibu uliotumika siyo sawasawa. Kwa upande wangu kazi yetu ni kuchukua maoni ya Wabunge baadaye kwenda kuyafanya kazi jambo ambalo halijaka vizuri. Lengo ni kwenda kulirekebisha na hasa kuangalia vitambulisho hivi vinatolewa kwa akina nani. Lengo ni kwa wale ambao hawako katika sehemu rasmi sasa wanarasimishwa ili nao waweze kushiriki katika uchumi na mwisho wa siku waweze kupata kipato chao kwa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme eneo hilo inawezekana kweli kuna upungufu lakini hili jambo linatofautiana kutoka eneo moja na lingine. Kwa mfano, ukiangalia maeneo ya Dar es Salaam na maeneo ya miji mara nyingi sana hata kama kuna changamoto siyo kubwa sana. Hata hivyo, tumechukua maoni na ushauri wote wa Waheshimiwa Wabunge ili tukaangalie jinsi ya kuboresha jambo hili ambalo nia yake ni njema lakini lifanyike kwa uzuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala zima la posho za Madiwani, Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji. Naomba nikiri kwamba Wabunge wengi walichangia hapa na Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Bunge na Kamati yake walianza kuchangia kuanzia kwenye Kamati na hapa Bungeni. Vilevile Wabunge mbalimbali walichangia hoja, nawashukuru sana. Hoja hii ilipata michango mingi kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge. Niseme wazi kwamba jambo hili inaonekana lina *interest* kwa Wabunge wote kuona ni jinsi gani tutaangalia suala za posho za Madiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikiri wazi kwamba Madiwani wanafanya kazi kubwa sana, tunapopeleka fedha kule Madiwani kwa kweli wanasimamia kwa karibu zaidi. Hata posho yao kama nilivyosema iliongezwa awali lakini Wabunge wamesema kuna haja ya ku-reviewhizi posho. Kwa hali ya sasa kwa sababu tunaangalia muktadha wote nini kifanyike, kwa ujumla niseme kwamba tumelichukua wazo hili kwenda kulitafakari zaidi ni jinsi gani tutafanya hawa Waheshimiwa Madiwani kwa siku za usoni angalau kile kipato chao kiweze kuongezeka kwa sababu wanafanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo ambalo limeonekana ni tete nalo ni la mwongozo wa utoaji wa posho imeonekana kwamba umekuwa ni changamoto kubwa. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, Ofisi yangu imejipanga tutaenda ku-review tena ule mwongozo vizuri na haraka iwezekanavyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo kubwa ni tuweze kubainisha wapi Diwani anatoka kwa mfano ukienda Jimbo la Mbinga kule Diwani mwingine anatoka kama mwezi anakwenda kwene mkutano atafanyaje na maudhui ya kazi wanayofanya. Kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba jambo hili mimi na wataalam wangu tutali-review vizuri ili Madiwani wetu wasiwe na kinyongo katika utendaji wao wa kazi ili kazi ziweze kufanyika vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine lilikuwa ni uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Kama mnavyofahamu mwaka huu tunatarajia kwenda kufanya uchaguzi wa Serikali za Mitaa na uchaguzi huu unaongozwa na Katiba yetu, Ibara 144 na 146 imezipa mamlaka Serikali za Mitaa lakini zikatungwa sheria zetu, Sura Na. 287 na 288 ambapo huko tumeenda kuhakikisha uchaguzi huo unasimamiwa katika mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza uchaguzi huu unaandaliwa na kanuni, tumeanza kuandaa kanuni,

wataalam waliandaa zile kanuni kwa kina na umahiri wa hali ya juu. Pia tuliweza kuwashirikisha wadau mbalimbali kama Wakurugenzi wote wa Halmashauri; Wakuu wa Wilaya; Maafisa; Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakuu wa Mikoa. Pia tukapanua goli zaidi ikaenda kwa wadau wa kisiasa, tukaenda kufanya mukutano wa siku mbili, tarehe 1 mpaka tarehe 2 kuhakikisha kwamba vyama vyana siasa vyenye usajili vinashiriki kutoa maoni yao katika rasimu hii ya kanuni. Naomba nikuhakikishie, mukutano wetu na vyama vyana siasa ulikuwa mzuri sana na wadau walishiriki vizuri sana katika kuhakikisha kanuni hizi wanaziboresha na kutoa mapendekezo. Sasa jambo hili lipo katika hatua ya mwisho ya ku-accommodate yale maoni ili kuhakikisha kanuni hizi zinafanya na baadaye kwenda kuzitangaza katika Gazeti la Serikali. Tunatarajia mwishoni mwa mwaka huu tutaenda kufanya uchaguzi wetu, matarajio yetu ni Novembra 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni suala nzima la utoaji wa mikopo. Nishukuru Naibu Mawaziri wangu wamelizungumzia, ni kweli utoaji wa mikopo umekuwa na changamoto kubwa sana hasa mikopo ya asilimia 10 ya vijana, akina mama na watu wenye ulemavu. Nilishukuru Bunge hili, katika *Finance Bill* iliyopita wajumbe hawa walifanya marekebisho ya sheria na ilielekeza mikopo hiyo sasa itolewe kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona kwamba hapa mwanzoni mikopo ilikuwa inasuasua sana lakini naomba nisiwe mchoyo wa fadhila niishukuru sana Kamati ya Bunge la TAMISEMI na Utawala Bora ilivyokutana na mikoa yote kupitisha bajeti ilikuwa ni hoja mahsus sana na ilijadiliwa kwa kina zaidi. Naomba nitoe taarifa kwa Waheshimiwa Wabunge ndani ya siku hizi chache za wiki mbili baada ya maelekezo yenu, mwanzo zilikuwa zimetoka karibu shilingi bilioni 13 peke yake leo hii napozungumza mpaka tarehe 30 Machi, zimetoka takribani shilingi bilioni 20.7, haijawahi kutokea ndani ya kipindi kifupi ambayo ni utekelezaji wa lengo takribani asilimia 38.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikujulishe wazi kwamba tulipaswa Ofisi yetu itoe kanuni na kanuni hizo

zimeshatoka na zimetoa maelekezo na zimeshatangazwa katika Gazeti la Serikali, hivi sasa ni kwamba ma-*accounting officer* ambapo Wakurugenzi wetu wa Halmashauri wanawajibu wa ku-comply na kanuni zilizotoka. Waliokuwa wanafuatilia vyombo nya habari siku ya Ijumaa asubuhi nilitoa taarifa kwa Wakurugenzi wote wa Halmashauri wahakikishe ile mikopo yote itakapofika tarehe 28 Juni, takribani asilimia 83.3 ya mikopo ya vijana, akina mama na watu wenye ulemavu lazima yote iweze kutoka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini asilimia 83? Ni kwa sababu mwezi Juni wanakuwa bado hawajafunga mahesabu na ndiyo maana nimesema ikifika tarehe 20 Julai, bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019 mikopo hiyo inatakiwa itoke kwa asilimia 100. Kanuni ambazo tumezitoa zimewabana ma-Accounting Officer wale watakaoshindwa kupeleka mikopo hiyo kuna utaratibu wa kisheria ambao utaenda kuchukuliwa dhidi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naamini si rahisi kwamba kuna Mkurugenzi ambaye anataka kuingia kikaangoni kwa makusudi kwa kushindwa kutoa mikopo hii ya asilimia 10 ambayo ipo kwa mujibu wa sheria. Naomba nikuhakikishie katika jambo hilli tutakuwa wakali sana, hatuna masihara kwa sababu hii ni haki ya vijana ambao wengi wao wamemaliza vyuo vikuu na wamekosa ajira, huu ni mlango mwingine mbadala wa vijana kujilingiza katika suala zima la ajira kuhakikisha wanaenda kujenga uchumi wa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo limezungumzwa sana humu ndani na nishukuru sana karibuni Wabunge wote walizungumza ni suala zima la elimu. Tunambiwa kwamba nchi zimegawanyika, kuna nchi zenyе rasilimali mbalimbali na nyngine ni masikini zaidi lakini kuna nchi zimewekeza katika elimu. Ndiyo maana leo kuna mifano ya dhahiri kabisa, kuna nchi duniani mfano Switzerland na Nordic Countries ukiangalia rasilimali walizonazo ni chache lakini sasa hivi ndiyo watu ambao wanatawala dunia kiuchumi, ni kwa sababu wamewekeza katika maarifa ya

watu. Ndiyo maana binafsi na Ofisi yangu inamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa programu ya Elimu bila Malipo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi hiki tokea Serikali ya Awamu ya Tano na Mheshimiwa Rais kuelekeza sasa wananchi wa Tanzania wapate elimu bila malipo, upande wa elimu ya msingi peke yake zaidi ya shilingi bilioni 374.3 zimetoka kusaidia elimu msingi bila malipo. Kwa upande wa sekondari zaidi ya shilingi bilioni 479.9 zimetoka kwa ajili ya elimu bila malipo. Jumla kuu ni zaidi ya shilingi bilioni 854.3 ambapo ni fedha nyingi haijawahi kutokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili tukiri wazi watoto wa maskini na *voiceless people* wamepata msaada mkubwa sana. Tunaona shule zingine zinafurika ni kwa sababu watoto hawa wa maskini zamani walikuwa wanakosa elimu leo dirisha limefunguliwa, kipa katoka, sasa watu wanapata fursa ya kupata elimu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikuhakikishie miaka ijayo dirisha la kuhakikisha tunajenga uchumi kwa pamoja itakuwa siyo kwa watu wenye uwezo peke yake bali na watoto wa maskini waliofunguliwa dirisha hili sasa tunasema tutajuwana mbele ya safari. Mheshimiwa Rais amenipa wajibu wa kulisimamia eneo hili, kwa kweli tunamshukuru sana kwa programu ya elimu bila malipo ameitendea haki nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala la ajira ambalo limezungumziwa na wajumbe mbalimbali. Naomba niseme, Serikali ya Awamu ya Tano kwa lengo la kuangalia changamoto iliyojitokeza mpaka sasa zaidi ya walimu 13,632 walijiriwa na kuripoti katika shule zetu za msingi na sekondari lakini si muda mrefu tutatoa ajira zingine zaidi ya 4,549 ambazo ziko katika hatua ya mwisho kabisa ambapo tumeshatangaza na watu wameshaomba ambapo jumla ya walimu watakaoingia katika soko la ajira watakuwa ni 18,181. Hii inaonyesha *commitment* Serikali iliyo nayo katika suala hili la ajira na lengo ni kuongeza idadi ya walimu. Naomba nikiri

wazi kwamba tutaendelea kuongeza idadi ya walimu ili watoto wetu katika shule zetu waweze kupata elimu bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, hapa juzi juzi aliweza kutoa takriban shilingi bilioni 29.9 kwa lengo la kwenda kumalizia maboma. Waheshimiwa Wabunge hawa ni mashahidi, maboma zaidi ya 3,200 yote yameenda kumaliziwa ukarabati. Siyo hivyo tu, mwezi wa Pili Mheshimiwa Rais ametoa zaidi ya shilingi bilioni 56 hapa. Serikali imetoa fedha hiso, ambapo ukija kuangalia lengo lake ni kwenda kujenga madarasa mapya 934 kwa ajili ya kuongeza madarasa. Vile vile kujenga mabweni mapya 210 ili kuhakikisha kwamba watoto wakiingia Kidato cha Tano waweze kupata mazingira mazuri ya kusomea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunaenda kujenga matundu ya vyoo yapatayo 2,141. Hiki ni kipindi tunatarajia kabla ya mwezi wa Sita kazi zote ziwe zimekamilika. Vile vile tutajenga nyumba za walimu, hali kadhalika tunajenga mabwalo yapatayo 76 katika shule zetu. Hii yote ni kazi kubwa kwa lengo kubwa la kuhakikisha kwamba elimu inasonga mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikujulishe, tayari zimeshatoka shilingi bilioni 16 kwa ajili ya kununua vifaa vya zaidi ya maabara 1,280. Hii ni kazi kubwa. Lengo letu kubwa ni kwamba maabara hizi nazo ziweze kufanya vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, suala la ununuzi wa magari, takribani magari 26 kwa Maafisa Elimu Mikoa, manunuzi yameshafanyika na wiki tatu zilizopita nilitoa siku tisini nataka nione mikoa yote imeshapata magari. Lengo kubwa ni Maafisa wetu wa Elimu waweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo katika hotuba yangu nilizungumza wazi kwamba *investment* kubwa inaenda kufanyika hivi sasa katika suala zima la ujenzi wa miundombinu. Kwa mfano, kupitia mpango wa EP4R zaidi ya madarasa 1,200 tunaenda kuyajenga, zaidi ya matundu ya vyoo 3,000 yatajengwa na zaidi ya mabweni mengine ya

ziada 300 yatajengwa, zaidi ya vyumba vya madarasa vingine vipatavyo 1,500 vingine mbadala, halikadhalika tutajenga nyumba za walimu na mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikuhakikishie kwamba Serikali hii ya Awamu ya Tano ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, imejipanga kuhakikisha kwamba tunaenda kushughulikia changamoto ya kielimu na lengo letu kubwa ni kwamba Serikali inavyojielekeza kwenda katika uchumi wa kati lazima tuijiwekeze vizuri katika suala zima la elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, Serikali haijalala, inafanya kazi usiku na mchana. Hata hivyo niwahakikishie, mmeona jinsi gani tumefanya mabadiliko makubwa katika ujenzi wa miundombinu katika shule zetu kongwe. Tumemaliza awamu ya kwanza shule 48 ambapo sasa hivi tunaendelea na shule 25 na bajeti ya sasa hivi ina shule 15. Lengo kubwa ni nini? Shule zetu sasa zirudi katika hadhi yake ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge hawa ni mashahidi, hata walipokuja hapa kuapishwa, wakati Mheshimiwa Rais alipokuja kuzindua Bunge hili, shule hata ya Dodoma Sekondari haikuwa hivi. Nenda hapo Dodoma, nenda Bihawana, Kondoa, Mpwapwa, Moshi Tech, Mtwara Tech kokote unakokwenda miundombinu imeboreka kwa kiwango kikubwa. Hii ni ajenda ya Serikali ya Awamu ya Tano. Lengo kubwa, shule zote kongwe zirudi katika ubora wake. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana nimesema shule hizi leo hii naomba na Waheshimiwa Wabunge tembeleeni maeneo yenu mkaone maajabu. Hata wale wa Dar es Salaam, nendeni Pugu Sekondari pale, nendeni Jangwani Sekondari pale, mtakuta maajabu makubwa yamefanywa ndani ya Serikali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, nimesema bajeti hii ya kwangu sasa hivi ambayo nime-*present* hapa tunaenda

kuboresha shule nyingine 15. Imani yetu ni nini? Tunataka shule zote ambazo zamani zilikuwa maarufu, lazima zirudi katika utaratibu wake ule ili Watanzania waweze kusoma vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajenda nyingine ambayo kwa kiwango kikubwa imejadiliwa hapa, ni suala zima la ujenzi wa miundombinu ya afya. Namshukuru sana Naibu wangu, amezungumza kwa kina katika eneo hili la afya.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, kwa dhati ya moyo wangu, naomba sana nilishukuru Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sana tu. Waheshimiwa Wabunge ninyi mnaingia katika historia ya mpya. Nchi yetu ilikuwa na changamoto kubwa sana katika Sekta ya Afya. Siku zote huwa nazungumza, toka Uhuru mpaka Serikali ya Awamu ya Tano tullkuwa na Hospitali za Wilaya 77 peke yake. Vituo vya afya vilivyokuwa na uwezo wa kufanya huduma ya upasuaji, vilikuwa 118 peke yake. Ninyi Waheshimiwa Wabunge mmeingia katika historia, ndani ya kipindi kifupi, vituo vya afya 352 vimeboreshwa, haijawahi kutokea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi mmemwona Mheshimiwa Rais alivyokuwa Mikoa ya Mtwara na Ruvuma alituzindulia vituo vya afya kule; vya Mbonde, pale Masasi na Kituo cha Afya cha pale Madaba. Hii ni kazi kubwa, haijawahi kutokea. Naomba nirudishe heshima hii kwa Waheshimiwa Wabunge, msingekubali bajeti, vituo hivi visingepita. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika watu nchi hii wataingia katika historia ni Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge la Kumi na Moja, litaingia katika historia. Pia hamkuwa watu wenye hiana, mwaka 2018 nililetajua bajeti hapa kuomba tujenge hospitali mpya 67, ninyi Wabunge mliridhia ikapita shilingi bilioni 100.5 na ujenzi unaendelea huko makwenu. Hii haijawahi kutokea na ujenzi huo unaendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimewapa *deadline*, yale majengo saba, tarehe 30 mwezi Juni, nataka nione majengo yote yamesimama vizuri. Nilisema mwaka 2018, majengo yale ni kingiambago tu, yaani ni kianzio. Mwaka huu ndiyo maana katika majengo yale yale, Serikali imetenga fedha nyingine kwa ajili ya kuendelea kujenga majengo hayo. Vijana wa Tandale wanasesma kampa, kampa tena. Mwanzo mmepata na mwaka huu mmepata tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hiyo haitoshi, Bunge hili limekuja na vituo vingine vya afya na hospitali nyingine za Wilaya 27. Kwa *interest* ya Bunge hili naomba nivitaje; tunaenda kujenga Hospitali ya Wilaya ya Chalinze, Hospitali ya Wilaya ya Kondoa, tunaenda kuimarisha Hospitali ya Wilaya pale Kongwa, Hospitali ya Wilaya ya Mbogwe, Hospitali ya Wilaya ya Biharamulo, Hospitali ya Wilaya ya Msimbo, Hospitali ya Wilaya ya Kakonko, Hospitali ya Wilaya ya Livale, Hospitali ya Wilaya ya Babati *DC*, Hospitali ya Wilaya ya Sengerema kwa watani wangu Wasukuma, Hospitali ya Wilaya ya Mbeya, Hospitali ya Wilaya ya Kilombero, Hospitali ya Wilaya ya Newala, Hospitali ya Wilaya Kwimba, Hospitali ya Wilaya ya Sengerema, Hospitali ya Wilaya ya Manispaa ya Sumbawanga. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, tunaenda kujenga Hospitali ya Wilaya ya Madaba, Hospitali ya Wilaya ya Msalala, Hospitali ya Wilaya ya Ikungi, Hospitali ya Wilaya ya Tunduma, Hospitali ya Wilaya ya Manispaa ya Tabora, Kaliua, Handeni, Mkinga; jamani mnataka nini? (*Vigelegele/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana rafiki yangu Mheshimiwa Mwakajoka siku ile alipokuwa anachangia nikasema, Mwakajoka shukuru basi.

NAIBU SPIKA: Nadhani atakuwa ana ndiyo yako leo huyu. (*Kicheko*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, haitoshi. Lengo letu ni kuhakikisha tunaboresha mazingira haya.

Ndugu zangu, sisi tumepewa dhamana kama viongozi. Tutakuja kuulizwa kwa hizi dhamana tulizopewa. Niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge, hata hao wanaosema hapana, siyo mbaya, kwa sababu tunakubali wote bajeti hii kwa pamoja. Hii ni bajeti ya kwenda kuwasaidia wananchi wetu siyo jambo lingine. Bajeti ya watu wasiokuwa na sauti (*a voiceless people*) bajeti yao ndiyo hii hapa hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na jambo la ajenda hapa ya suala zima la ujenzi wa miundombinu. Naishukuru sana Kamati ya Bunge ya TAMISEMI na Utawala Bora, lakini nawashukuru Wabunge, kwa kazi kubwa inayoendelea kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wanavyosimamia miradi kule *site*. TAMISEMI sisi tunasimamia miradi katika maeneo makubwa manne; kuna miradi hii ya *TARURA* kwa ujumla wake, lakini kuna miradi inayoboresha Jiji la Dar es Salaam, *DMDP* ambayo thamani yake ni shilingi bilioni 660.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuna miradi ya *TSP* ambayo ukienda Mbeya unaikuta, Arusha utaikuta, Mwanza utaikuta, Ilemela, ukija Dodoma hapa unaikuta, ukienda Mikindani unaikuta na ukienda hata kwa ndugu yangu Mheshimiwa Zitto Kabwe pale Kigoma Ujiji utaikuta. Lengo la miradi hii ni kuimarisha miundombinu ya barabara. Tunajenga barabara za lami kuweka taa na madampo ya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna miradi katika Halmashauri zote za Miji, ndiyo maana leo mnawonwa Mheshimiwa Mwanri anasema, ukifika Tabora ni kama umefika Toronto. Hii ni kazi kubwa iliyofanyika. Tunaimarisha Halmashauri zote za Miji na Manispaa. Ndiyo maana leo ukienda Bariadi, mji ni tofauti, Musoma, Tabora, Morogoro, Iringa, Sumbawanga, Mpanda, Korogwe, Moshi, miji ni tofauti. Hii ni kazi inayofanyika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, mwaka huu tutaendelea tena kujenga ujenzi wa madaraja katika maeneo mbalimbali. Nashukuru sana, baada ya kilio cha Waheshimiwa Wabunge tena, zaidi ya shilingi bilioni 33 imeongezeka; hii ni faraja kubwa sana. Nina imani jambo hili linaenda kutatua changamoto zetu katika mamlaka ya Serikali katika Serikali za Mitaa, katika ujenzi wa miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikuhakikishie zaidi ya madaraja 113 mwaka huu ambayo tunatarajia kuyajenga chini ya *TARURA*. Pia kuna makalavati makubwa zaidi ya 273 tutayajenga; na makaravati madogo zaidi ya 2,403 yote tunaenda kuyajenga. Hiyo ni ukiachia mifereji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi kubwa inaenda kufanyika katika Jiji la Dar es Salaam. Niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya TAMISEMI walivyoenda kutembelea miradi ya *DMDP* pale Dar es Salaam, waliona maajabu makubwa katika maeneo ambayo mwanzo yalikuwa yamejishika. Mpaka kaka yangu Mheshimiwa Selasini alipofika pale eneo la Tuangoma alishangaa kuona hawa watu wa Mbagala Kuu na Kijichi walivyounganishwa na watu wa Kibada kwa barabara ya mfano hajawahi kutokea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nenda Kijichi pale, tembelea hali ni tofauti, nenda Mbagala Kuu, hali tofauti; maeneo ya Makumbusho hali ni tofauti, maeneo ya viwandani hali ni tofauti. Hii kazi lengo lake ni kwenda kubabilisha Jiji la Dar es Salaam. (*Makofii*)

Ndugu zangu, naomba niwaambie, tutaendelea kuimarisha ujenzi wa vituo vya mabasi. Najua tulimaliza kule Korogwe, tumemaliza pale Songea, juzi juzi tumeaita Songea lakini tunaimarisha kutokea Songea na maeneo mengine. Lengo letu ni kwamba madampo ya kisasa, magari ya kuzolea taka, lakini kila eneo lazima tulimarishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine tunaloenda kulifanya kazi, ni suala zima la ujenzi wa masoko. Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, mwaka 2018 niliomba bajeti

hana; ujenzi wa Stendi ya Dodoma, halikadhalika ujenzi wa Soko Kubwa la Dodoma. Wengine walikuwa wananiambia, hii Jafo *Power Point Presentation* ni kanyaboya? Nikawambia mtaona vitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi, mnapoenda pale Nane Nane mnakuta stendi ya kisasa na soko la Kisasa linajengwa. Jukumu letu kubwa ni nini? Ni kuhakikisha tunabadilisha miundombinu yetu yote, wananchi wapate faraja kwa utendaji wa umakini wa utekelezaji wa llani ya Chama cha Mapinduzi chini ya Serikali ya Awamu ya Tano. Katika hili mimi sina hiana, ninafahamu wazi Waheshimiwa Wabunge tutaendelea kushirikiana vya kutosha kuhakikisha miradi hii yote inaenda kufanyika kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiachia na mambo mengine yote kwa ujumla wake na hasa niwaombe Waheshimiwa Wabunge, ofisi yangu ina watu wengi, kuna suala zima la mahusiano, mkubwa wangu Mheshimiwa Mkuchika hapa atakuja na suala zima la utawala bora; hata hivyo, tunaendelea kutoa mafunzo mbalimbali kwa viongozi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nanyi mnafahamu hali tuliyotoka mwanzo na sasa hivi ni tofauti sana. Mwanzo tulikotoka hali ilikuwa siyo shwari sana, lakini baada ya mafunzo mbalimbali ambayo kupitia Chuo cha Uongozi, mnaona kidogo kwa kiwango kikubwa kama tuna changamoto ambazo tunaweza tukazitaja eneo kwa eneo, lakini kwa kiwango kikubwa sasa hivi kazi inaenda vizuri. Hata hivyo, tutaendelea kuimarisha suala zima la mafunzo na *program* mbalimbali kwa lengo la kujengeana uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo tufahamu kwamba watu wengine hawa ni vijana zaidi, sawa eeh, kwa hiyo, lazima kidogo kuna vitu vingine lazima *training*, tuwe tunapeana mawazo ili kuhakikisha kwamba mambo yanaenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe Waheshimiwa Wabunge jamani, msiwanyong'onyeshe watu wanaofanya kazi. Naomba niwaambie, katika ofisi ambayo hailali ni ofisi yangu. Hawa Manaibu wangu, mwangalie Mheshimiwa Waitara huyu, toka ateuliwe hajapumzika. Mwangalie Mheshimiwa Kandege, wanahangaika. Nimewaelekeza wafike kwenu wawasikilize waangalie changamoto. Sasa ikitokea Mbunge hapa anakuja anasema hakuna lolote, inawanyong'onyeza sana hata watendaji wetu. Tufikie wakati angalau tushukuru kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo mengine sitaki kusema tu, kaka yangu hapa alisema sijui TAMISEMI nini, ovyo kabisa. Jamani! Kulikuwa hakuna hospitali ya Wilaya kule, vituo vya afya vitatu vimeenda. Acha ukarabati wa shule na vitu mbalimbali watu wanafanya wanahangaika. Kama kuna magomvi tunashughulikia magomvi kwa magomvi, lakini sio kama unawavunja nguvu watendaji. Afadhalii mimi! Mimi nina moyo mgumu, sina shida. Ila mnawapa *stress* watendaji wangu, hawa wasaidizi wangu. Kusema hakuna kitu TAMISEMI, jamani hii kazi yote kubwa inayofanyika. Watu hawalali kwa ajili ya kuwahudumia Watanzania. Tu-appreciate kidogo jamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana nasema, mimi nina moyo mgumu, sina shida, lakini Serikali inafanya kazi kweli kweli. Naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli, naomba niwaambie, hii ni *legacy* anaiweka, itadumu kwa miaka mingi. Hata kama mtu hupendi lakini *legacy* ipo. Haya mambo yote kwa uchache niliyowaelezea, siyo haba, shughuli nzito imefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hii kazi, naomba sana nimshukuru Waziri Mkuu wetu. Waziri Mkuu wetu halali, hapumziki. Wanaopitia vyombo mbalimbali, kila siku Waziri Mkuu yuko katika *assignment*. Lengo kubwa ni kwamba imani waliyotoa Watanzania kwa Serikali yao ya Awamu ya Tano mambo yaende vizuri, Waziri Mkuu hapumziki. Ningekuwa katika mikutano ya kisiasa ningesema pigeni makofi kwa Waziri Mkuu kidogo. (*Makofi/Vigegele*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema mnyonge mnyongeni...

WABUNGE FULANI: Haki yake apewe.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, kazi inafanyika ndugu zangu, kazi inafanyika na hii inafanyika bila hiana, watu wanahangaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, namkushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwanza kwa kuwa kiongozi mahiri, anatuongoza vizuri. Naomba niseme kwamba Bunge hili na Serikali inaenda kwa utendaji wako chini ya usimamizi wa Dkt. John Pombe Magufuli na mama Samia Suluhu Hassan. (*Vigelegele/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utaratibu wa kanuni yetu, napenda kuwatambua wote, kwa sababu nikimtaja mmoja mmoja itakuja kuwa sokomoko. Waheshimiwa Wabunge hapa mmechangia vya kutosha katika hoja hii. Hakuna hata mtu mmoja; ndio maana nimesema wote kwa sababu utaratibu umewekwa kikanuni, niseme Wabunge wote mmechangia kwa kiwango kikubwa. Kwa hiyo, mmenipa nguvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwaambie, ile *speed* yetu ya mwanzo tuliyokuwa tunafanya, kwa michango yenu, naomba niwaahidi *inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, *speed* ile itakuwa mara mbili zaidi kwa mwaka wa fedha unaokuja. Tunafanya hivi ili Wabunge mfurahi na mfurahi wote. Unajua Mbunge ukifurahi, unaondoa *stress*. Mambo yakienda huko hakuna shida, una uhakika mambo yako yanaenda yametulia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba niwaambie, sisi jukumu letu ni kutengeneza mazingira. Tutawatengenezea mazingira kutekeleza miradi yote kwa wananchi. Ile inayowezekana yote tutaitekeleza kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu. Lile tutakaloshindwa kwa hali ya

kibinadamu, basi hatuna namna, lakini kwa dhamira yetu inatuelekeza tufanye kila liwezekanalo kwa ajili ya wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa zaidi naomba nishukuru familia yangu kwa malezi mazuri sana; na watoto wangu na wake zangu. Siyo kwamba nina wake wanenye, yule mtani wangu katania tu, kachomekeaa. Watoto wangu nawashukuru sana, ni watoto wasikivu sana, wanani-*encourage* baba yao kufanya kazi, napata *spirit* kubwa ya kufanya kazi. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia namshukuru sana mama yangu mzazi Khadija binti Mwalimu, namwombea sana mzazi wangu baba yangu Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema Peponi alipotangulia mbele ya safari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru wananchi wa Kisarawe, wapiga kura wa Kisarawe wamekuwa wakinivumilia hata wakati niko katika michaka michaka. Kwa kweli nawashukuru sana na wengine wapo humu ndani nawaona wapiga kura kule. Nawashukuru sana, wanani pa nguvu. Naomba niwahakikishie kwamba *commitment* yangu kama kiongozi niliyepewa dhamana, ambapo Mheshimiwa Rais amenipa dhamana, lakini Mungu amenipa dhamana hii kuweza kuwatumikia wananchi, nitajitahidi kwa moyo wangu wote na nguvu zangu zote kutimiza wajibu wangu wote unaotakiwa, nikijua wazi mimi ni binadamu, nina maswali mawili; nina swali la duniani na nina swali siku nitakaporudi mbele ya mikono yake. Mungu anisaide niendelee kutenda wema huo na kuhakikisha naweza kuwashudumia wananchi wote kwa moyo wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho zaidi nimshukuru Mheshimiwa Rais tena kwa mara nyingine kwa mapenzi yake, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, lakini niwashukuru Mawaziri wote wakiongozwa na *Chief Whip* wetu hapa dada yangu Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa kazi yao mahiri, dada yangu Mheshimiwa Mhagama halali, hapumziki

anafanya kazi kubwa sana, huyu ndiye kiranja wa Mawaziri humu ndani, tunakushuuru sana dada yangu, Mheshimiwa Jenista Mhagama. Pia niwashukuru Wabunge wote, Wabunge wamekuwa wema kwangu wanani pa moyo, hongera sana. Mungu awalipe sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Tutaendelea na utaratibu wetu, sasa nimuite mtoa hoja Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora ahitimishe hoja yake. Mheshimiwa Waziri una dakika 45.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushukuru kwa kupata nafasi hii ya kujibu hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezitoa pamoja na Kamati. Kama nilivyoshukuru kwenye hotuba yangu napenda kuwashukuru viongozi wa Taifa letu. Viongozi wa kitaifa wakiongozwa na Mheshimiwa Dkt. Magufuli Rais wetu, napenda kumshukuru Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti jinsi mnavyotuongozza humu ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwashukuru sana Wabunge wote, kila mtu anajua kwamba, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora ni Wizara ambayo ina uzito wa pekee ni Wizara ambayo Wabunge nawapongeza wa CCM na wa Upinzani walipokuwa wanachangia humu ndani kila mmoja nilimwona ameweka mbele maslahi ya Taifa letu. Kwa hiyo, nataka niwashukuru sana na niwaahidi kuwa sitawaangusha katika majibu niliyowaandalieni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa nataka niseme, nchi yetu ipo salama wala haina matatizo ya kiusalama, kikubwa niseme vita dhidi ya rushwa katika nchi yetu ina mafanikio makubwa, wachunguzi wa ndani wanasesma hivyo, wachunguzi wa nje wanasesma hivyo. Vile vile kubwa zaidi mimi ndio Waziri wa Watumishi wa Nchi hii. Nataka

nichukue nafasi hii kuwapongeza watumishi wa umma popote walipo, mtumishi yoyote awe kwenye shirika la Serikali, awe kwenye Wizara, awe kwenye Wakala ilimradi analipwa na Serikali Waziri wao ndio mimi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Watumishi wa Umma. Ukisikia tumenunua ndege za Serikali, ninyi ndio mmekushanya kodi, tumefanya nini, tumefanya nini, haya yote ni kwa sababu watumishi wa umma mmetekeleza wajibu wenu, huku nikizingatia wapo wachache wanaotuharibia sifa, lakini wengi mnafanya kazi nzuri na ndio maana mimi naona fahari ya kuwa Waziri wenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme jambo moja ambalo Waheshimiwa Wabunge walilizungumza hapa nisije nikalisahau, *TASAF* haijafika katika vijiji na shehia zote nchi zima. Kuanzia tarehe Mosi Julai tunajipanga tunataka tufike katika vijiji vyote, tunatakiwa tufike shehia zote bara na visiwani. Kwa hiyo hilo msiwe na wasiwasi, tulikuwa tunajipanga maana wanasema unajikuna pale unapofikia mkono, sasa mkono tumeurefusha. Hivyo, tuna uhakika tutakapoanza mwezi huo tutafanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nichukue nafasi hii kuwashukuru Wabunge Wizara yangu imechangiwa humu ndani na Wabunge 85 orodha ninayo hapa, itaingia kwenye *Hansard*. Wizara yangu imechangiwa kwa maandishi na Wabunge 20, majina yenu ninayo hapa yataingia kwenye *Hansard*. Kama nilivyosema mambo yangu yapo mengi nikasema basi ngoja niende moja kwa moja kujibu hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wamechangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu yangu Mheshimiwa Edwin Ngonyani anasema Serikali iangalie suala la watumishi wa afya walioajiriwa kihalali na Serikali kwa mkataba, lakini sasa wanaondoshwa. Maelezo yako hivi, Katibu Mkuu Kiongozi alitoa kibali kwamba watumishi wa afya wakati wa ajira badala ya kufuata mlolongo wa kawaida wa *interview* na kitu gani na kitu gani na kwa sababu walikuwa wanahitajika haraka akalegeza masharti kwamba badala

ya kwenda kwenye *Interview* sasa waandikieni barua waende moja kwa moja wakaripoti kwenye maeneo ya kazi na ndivyo ilivyofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kuajiriwa kwa mkataba kwa mtindo ule haikuwa sababu ya wewe kutohakikiwa kama wenzio. Kwa hiyo kwenye uhakiki wapo walibainika pamoja na kwamba walikuja na vyeti vile hospitali, walibainika kwamba walikwenda kusoma lakini hawakuwa na elimu inayotakiwa kabla ya yeYe kwenda kusoma. Hao ndio ambao baadaye waliondolewa, kwa nini? Kwa sababu walikwenda kusoma wakati hawana elimu inayotosheleza wao kwenda kusoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika masuala ya utawala bora, ndugu yangu hapa Msemaji wa Kambi ya Upinzani, hayupo lakini mtandao wake mkubwa ndugu yangu, yanga mwenzangu, alisema hivi kumeanza kujitokeza viashiri vya ubaguzi ndani nchi yetu kwa mitazamo ya itikadi ya vyama vya siasa, aidha viongozi wamekuwa wanavunja sheria kwa kutoa kauli na mtamko kinyume cha sheria. Maelezo ya Serikali yanasema hivi hakuna ushahidi uliowasilishwa kuona kuwa kuna hali ya ubaguzi kwa misingi iliyotajwa. Hata hivyo, kupitia Bunge hili naomba viongozi wa vyama vya siasa na sisi Waheshimiwa Wabunge wote tushirikiane kukemea matendo hayo yanapojitokeza. Watu wa upinzani wanataka amani, CCM wanataka amani, asiye na chama anataka amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu, inapotokeza dalili kama hizo tushirikiane wote kukemea, kuna mtu mwininge akikemewa na CCM na ni wa CCM atasikiliza vizuri; kuna mtu mwininge wa upande mwininge akikemewa na Waziri wa Utumishi na Utawala Bora, anaweza asimsikilize vizuri, lakini akikemewa na Kiongozi na wa chama chake atasikia. Rai yangu wote tushirikiane linapotoka jambo kama hili wote kwa pamoja tulikemee, kila moja kwa nafasi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, amesema Msemaji wa Kambi ya Upinzani Tanzania imejitoa katika Mpango wa

Uendeshaji wa Shughuli za Serikali Kwa Uwazi (*Open Government Partnership*) na akasema kwamba kujitoa kule kunaweza kukaathiri uendeshaji wa Serikali yetu kwa uwazi. Maelezo ya Serikali ni kwamba *Open Government Partnership* ilianzishwa na Rais wa Marekani Obama na Waziri Mkuu wa Uingereza, haikuwa katika nchi zote duniani, lakini sisi Afrika Tanzania tuna mpango unaofanana huu wa kuendesha Serikali kwa uwazi unaitwa *African Peer Review Mechanism* na tena juzi juzi hapa Tanzania sisi, Mtanzania Balozi Sefue amechaguliwa kuwa katika Bodi ya *African Peer Review Mechanism* mpango wa Afrika wa kujitathimini uendeshaji wa Serikali yao kwa uwazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukaona kwamba hizi kazi zinafanana, tukaona hakuna sababu ya kuwa katika hi na ile, lakini niseme tu kwamba hata wale ambao waliingia katika hiyo *Open Government Partnership* nchi zingine zimeshajitia kwa mfano Urusi imejitoa, Hungary imejitoa na nchi zingine zimejitoa. Kwa hivyo maelezo ni kwamba, sisi tuliiingia kwa hiari, tumetoka kwa hiari yetu wenyewe baada ya kutosheka kwamba shughuli zile zinazofanywa na *African Peer Review Mechanism*, Mpango wa Afrika wa Kujitathimi wenyewe katika suala la utawala bora, tukaona inatosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimtoe hofu Mheshimiwa kwamba asiwe na wasiwasi Tanzania bado tunaendesha Serikali kwa uwazi na ukweli na ninataka niseme mfano ipo. Zamani tulikuwa tunaletewa hapa taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali, wanapelekewa Halmashauri, wanapelekewa Mawaziri wanaambiwa watekelezwe mle, lakini leo kila mwaka taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaletwa hadharani hapa Bungeni, inasomwa hapa Bungeni na inajadiliwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekaa kidogo muda mrefu katika Serikali nimewapoteza marafiki zangu wengi waliokuwa Mawaziri kutokana na ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wa Serikali, ilijadiliwa hapa ndani Wabunge wakasema tunaomba mtupishe. Kwa hiyo hakuna mashaka juu ya Tanzania kuendesha Serikali kimya kimya, ingekuwa

tunaendesha kimya kimya tusingeleta majadala kama huu ndani ya Bunge ukajadiliwa na kila mtu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna maoni ya Upinzani kwamba, kutokuwa na mifumo thabiti ya uratibu, ufuutiliaji na tathmini ya utendaji kazi wa kila siku ambao unatoa fursa kusomeka moja kwa moja kwenye kitengo kinachohusika na amesema hili Msemaji wa Kambi ya Upinzani Bungeni. Maelezo ya Serikali ipo mifumo ya kielektoniki ya kukusanya mapato ya Serikali kutoka katika vyanzo mbalimbali kwenda Hazina moja kwa moja, mifumo hiyo ni pamoja na *Government Electronic Payment Gateway, Local Government Revenue Collection Information System* na malipo ya mshahara kwa njia ya mtandao *Government Sales Payment Platform (GSPF)*.

Mheshimiwa Nailbu Spika, hivyo napenda kuwaambia Waheshimiwa Wabunge kuwa, utaratibu wa kuratibu, kufuutilia na kutathmini mapato na matumizi ya Serikali kwa njia ya mtandao upo, unafanya kazi na baadaye kama nilivyosema humu ndani tuna mpango baadaye wa kubadili Wakala wa Serikali Mtandao kuufanya ni Mamlaka ya Serikali Mtandao ili tunapokuja katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali kama haya pasiwe na uhiari wa mtu kujunga au kutojiunga ili mradi ni chombo cha Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyiningine inasema matumizi sahihi ya dola' kumekuwepo na matumizi mengi ya wananchi kupigwa, kujeruhija, kufariki kwenye vituo vya polisi ikiwa ni kubambikizwa kesi na kuwaweka mahabusu kwa makusudi hata kwa kesi zinazodhaminiwa. Maelezo ya Serikali vyombo vya dola vimeduwa vinatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizowekwa, aidha kuna mifumo mbalimbali iliyowekwa kwa ajili ya kuhakikisha vyombo hivyo vinatenda haki na pale panapokuwa na ukiukwaji wa sheria hatua huchukuliwa dhidi ya wanaohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, matukio ambayo yamebainishwa kwa mwananchi Musa Adam Said kubambikizwa kesi ya mauaji ni upungufu wa watendaji

wachache tulionaona ambao wanatia doa Serikali yetu. Hata hivyo Mheshimiwa Rais ameелеkeza wote waliohusika na tukio hilo wachukuliwe hatua kukomesha tabia hiyo na hatua zinaendelea kuchukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyiningine inasema Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya wanapotumia mamlaka yao ya kuweka mtu mahabusu kwa saa 48 na 28, wazingatie Sheria za Tawala za Mikoa. Maelezo ya Serikali kama nilivyooleza huko nyuma ni kweli Sheria ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ya mwaka 1997 inawapa mamlaka Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kumweka mtu ndani pale inapohibitika anahatarisha amani. Naomba Waheshimiwa Wabunge wanisikilize hii sheria inavyosema, nawaomba na huko walipo wanisikilize, mtu anawekwa ndani kama amehatarisha amani, sio watu wanadaiana madeni huko huyu hataki kunillipa, unampeleka kwa Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa unamweka ndani. Hawa wanadaiana, hawajahatarisha amani. Sasa hilo la kwanza, mtu asiwekwe mpaka awe amehatarisha amani, aidha Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya akitekeleza sheria kinyume na utaratibu anaweza akachukuliwa hatua ikiwa ni pamoja na ye ye mwenyewe kushtakiwa binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeke mea hili jambo, tukakemea, tukakemea, Mwanasheria Mkuu wa Serikali hatamtetea mtu aliyevunja sheria makusudi kumweka mtu ndani bila sababu, Wazungu wanasema *unlawful confinement* umeshughulika na *unlawful confinement*, umetumia sheria hii vibaya utapelekwa mahakamani na huyo uliyemweka ndani na Mwanasheria Mkuu wa Serikali hatakuja kukutetea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali sisi tumeeleza kisiasa, Mwanasheria wa Serikali sasa ametoa waraka kwa wale wote waliopewa mamlaka ya kumweka mtu ndani, kila mmoja ana barua ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, nami amenipa nakala ninayo. Ikieleza ni mazingira yepi mtu anaweza kukwekwa ndani na ameelleza *so emphatic*, moja ujiridhishe

kwamba ametenda kosa jinai; pili, uhakikishe kwamba asubuhi unaweka *in writing*, kwa nini unamweka ndani, nami nimesema humu ndani mara nyingi *government moves on paper*, hawa watu wengi wanaowekwa ndani ni kauli tu weka ndani, weka ndani. Ukimwambia hebu niandikie hawataki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo sheria inasema lazima wawekwe kwa maandishi; sheria inasema asubuhi yake afikishwe mahakamani, lakini lingine nataka nimalizie kuwaomba wenzangu wenyewe madaraka kama haya, utawala bora unasema kesi ikiwa mahakamani *DC hasikilizi*, Waziri hasikilizi, Waziri Mkuu hasikilizi, sheria inasema mahakama ya chini, uamuzi wake unaweza kutenguliwa na Mahakama ya juu. Wenzangu wengine wamejingiza kwenye katika mambo ambayo tayari *yalishahukumiwa* mahakamani. Acheni, acheni acheni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyiningine, je, Serikali huwa inafanya utafiti na kuangalia athari za maamuzi inayoyafanya? Maelezo hapa ni kwamba, Serikali inafanya tathmini kwa mfano, sisi katika Baraza la Mawaziri hatuamui kuna kikao cha wataalam wanakaa, kuna kikao cha Makatibu Wakuu wote, wao wanajadili mada ile, wanatoa ushauri, unaletwa kwenye Baraza la Mawaziri, Mawaziri tunafanya maamuzi baada ya kushauriwa na wataalam. Kwa hiyo niwatoe hofu ndugu yangu Mheshimiwa Msigwa *Reverend hayupo* hapa, amekosa uhondo wa majibu yake maana nilimwandalia yeye. Sisi hatufanyi maamuzi bila kutafakari, tunatafakari, tunashuriwa, lakini sio hivyo tu tunashaurika. Tukishauriwa na wataalamu ndio maana tunawasikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na tuhuma dhidi ya usalama wa Taifa, kuratibu na kuendesha vitendo vya utesaji wa raia wasio na hatia likitolewa mfano tukio la utekwaji wa mfanyakia shara maarufu Mohamed Dewji. Mwaka jana siku nahitimisha kama leo nilikuja hapa na Sheria ya Usalama wa Taifa, nikawasomeeni, jukumu la Usalama wa Taifa ni kukusanya habari na kuishauri Serikali *full stop*. Mtu

ameuawa ni kesi ya polisi, mtu amepotea ni kesi ya polisi, mtu ametekwa ni kesi ya polisi. Kwa hiyo nasema, katika hili jambo tumekwishalieleza, wasiipake matope Idara yetu ya Usalama wa Taifa, hawa vijana wangu wanafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitoa mfano hapa siku moja, kiongozi wa upinzani, kiongozi wa kwenye upande wa pili wa chama cha upinzani, watu walipanga kumdhuru na wenyewe wanajua. Vijana wa Idara ya Usalama wa Taifa wakamfuata wakamwambia mzee tuondoke hapa, tuondoke hawa watu hawana nia nzuri na wewe, wakamtorosha. Sasa badala ya kuwapongeza watu wanaonusuru maisha ya mtu, ndio sasa tunawapakazia, Mohamed Dewj amepotea *it is a police case*. Sheria ya Usalama wa Taifa mnayo nendeni mkasome, kazi yake, ni kukusanya habari na kuishauri Serikali kwisha, kila nchi utakayokwenda, utaratibu ndio huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, iwe huru na kufanya kazi bila ya kuingiliwa na mamlaka yoyote. Jambo hili liko kwa mujibu wa kifungu cha 4 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Na.11 ya mwaka 2007. Lengo kuu ni kuhakikisha kunakuwa na ustawi wa utawala bora na kuondoa rushwa nchini. Ili kutekeleza jukumu hilo, kifungu cha 5 cha Sheria iliyotajwa hapo juu imebainisha wazi kuwa taasisi hiyo iko huru na haiingiliwi na mamlaka yoyote. Kwa hiyo, napenda kuunga mkono hapa matakwa ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwamba taasisi iwe huru na niseme kwamba hivyo ndivyo sheria inavyosema, pale mnapoona kwamba sheria imepotoshwa ni jukumu la Mtanzania na Mbunge ye yoyote kuiambia Serikali kwamba hapa mmepotoka na mimi kama Waziri mwenye dhamana ya chombo tutaunda Tume, tutafuatilia na kama ikibainika kinachosemwa kipo tutachukua hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, TAKUKURU kufanya kazi kwa hisia bila ya kuzingatia ushahidi dhidi ya watuhumiwa. Napenda niseme, kazi ya TAKUKURU ni kukamata na

kupeleleza lakini anayefanya maamuzi Mahakamani siyo TAKUKURU. Kazi ya TAKUKURU ni kupeleleza na kupeleka mashauri Mahakamani mengine moja kwa moja, mengine kuititia kwa Mkurugenzi wa Mashtaka lakini anayeamua kwamba yule mtuhumiwa ana kosa au hana kosa ni Hakimu au Jaji anayesikiliza shauri hilo. Kwa hiyo, nafasi ya kumtia mtu hatiani TAKUKURU bila ushahidi haipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, watendaji wa TAKUKURU wasiteuliwe na Rais. Maelezo ya Serikali yako hivi, TAKUKURU wanafanya kazi kama jeshi, Rais wa nchi cheo chake kingine ni Amiri Jeshi Mkuu, watendaji wote wa vyombo vyta ulinzi na usalama kwa mujibu wa sheria tulizojoivekea wanateuliwa na Rais. Endapo Bunge hili siku moja mtaamua kubadilisha sheria mkasema wawe wanateuliwa na Waziri wa Utawala Bora na ikipita mimi nitawateua. Mimi mtumishi wa Bwana, nitatenda kama Bwana anavyotaka. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, TAKUKURU itupie macho Idara ya Uhamiaji na Uwekezaji kwani zimegubikwa na rushwa na urasimu unaoathiri uwekezaji. Hoja hii imetolewa na Mbunge wa Liwale ndugu yangu Mheshimiwa Kuchauka. Sisi hapa tunasema tu kwamba taarifa tumeipokea, tutaifanyia kazi ili tujiridhishe kama yaliyosemwa ni kweli au hapana.

Mheshimiwa Naibu Spika, TAKUKURU imekuwa ikiwashtaki wafanyabiashara kwa kuwabadilishia makosa yanayohusu kiasi kidogo cha fedha na kuyafanya makosa ya uhujumu uchumi. Sisi hapa tumeeleza kwamba kwa mujibu wa aya ya 21 Jedwali la Kwanza la Sheria ya Uhujumu Uchumi ya 1984 makosa yote yanayoainishwa kwenye Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa isipokuwa tu kwa kifungu 15 ni makosa ya uhujumu uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu watuhumiwa kushtakiwa kwa makosa ya utakatishaji fedha ni vyema ikafahamika kuwa kifungu cha 3 cha Sheria inayokataza kutakatisha fedha Na.12/2006 kosa la rushwa ni mojawapo ya makosa yanayosababisha mtumishi kushtakiwa kwa kosa la utakatishaji fedha. Kwa hiyo, wanashtakiwa kwa mujibu

wa sheria tuliyonayo. Inaweza kubadilika mpaka hapo Bunge hili litakapoamua kufanya mabadiliko. Kwa msingi huo, watuhumiwa hushtakiwa kwa makosa ya uhujumu uchumi na utakatishaji fedha kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilisema watendaji TAKUKURU wasiteuliwa na Rais. Hili nimekwishaliezea kwamba yeche ndiyo Amiri Jeshi wao Mkuu ndiye anayeteua wakuu wote wa vyombo vyana ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni ya ndugu yangu Mheshimiwa Zitto, kwa nini fedha kwa ajili ya uendeshaji wa TAKUKURU hazikaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wakati kila mwaka wanatengewa mabilioni ya fedha na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya mwaka 2007 inataka wakaguliwe. Kwanza, ndugu yangu Mheshimiwa Zitto, nakupongeza siku hizi umepata wanachama wapya wengi. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo hapa ndugu yangu Mheshimiwa Zitto ni kwamba fedha zinazopokelewa kwa ajili ya utendaji wa majukumu ya TAKUKURU zinajadiliwa na Bunge lako Tukufu kuititia Fungu 30 ambalo hukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kwa hiyo, nikutoe mashaka ndugu yangu kwamba fedha zao zinakaguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa kwamba Wabunge wanatunga sheria ambapo zingine zinanyima haki, kuna watu wanasingiziwa kesi za *money laundering*. Maelezo ya Serikali hapa yanasema TAKUKURU haina mamlaka ya kisheria kuzungumzia shauri lolote ambalo liko Mahakamani. Kwa hiyo, katika suala hili hatuna maelezo zaidi ya hapo kwa sababu jambo hili lipi Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na swali kuhusu Sekretarieti ya Maadili linasema Serikali iingize katika mtaala elimu ya maadili katika shule na vyuo ili kuwajenga watoto wetu katika masuala ya maadili na utawala bora. Suala hili

limetoka kwenye Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Utawala Bora na Serikali za Mitaa. Maelezo ya Serikali ni kwamba mtaala wa elimu kuhusu maadili kwa shule za msingi upo na ulianza kutumika kuanzia mwaka 2017. Kwa hiyo, kwa upande wa elimu ya msingi mtaala upo na wanaendelea kufundishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika shule za sekondari mada kuhusu maadili imejumuishwa katika somo linaloitwa *general studies*, zamani tukiita uraia. Hata hivyo, tumeupokea ushauri wa Kamati kwamba tuendelee kuzungumza na Wizara ya Elimu ili sasa na vyuo vikuu navyo wapate masomo haya yanayohusu uadilifu, maadili na kupambana na rushwa wanapokuwa vyuo vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilioletwa inahusu Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*), inasema utambuzi wa walengwa katika maeneo ambayo ni asilimia 30 ya vijiji, mitaa shehia nchini ufanywe mapema. Maelezo ya Serikali tunasema, utambuzi wa walengwa katika maeneo ambayo hayajafikiwa katika sehemu ya kwanza ya Mpango wa Maendeleo wa Kunusuru Kaya Maskini ambapo ni vijiji 5,693 utafanyika katika sehemu ya pili ya mpango inayotarajiwa kuanza 1 Julai, 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Serikali ni kuzifikia kaya maskini zote tulizonazo katika nchi hii. Kama nilivyoeleza pale mwanzoni wakati naanza kuongea kwamba tuna malengo kwamba Mbunge unapata tabu jimbo ni moja kuna vijiji wamo kwenye mpango vingine hawamo. Wewe Mbunge hawakuelewi na hata sisi Mawaziri tukienda mikoani hatueleweki, inaonekana kama kuna ubaguzi wa namna fulani lakini hoja ilikuwa ni masuala ya fedha. Sasa hivi kama nilivyosema tumejiandaa ikifika tarehe 1 Julai, 2019 tunataka tuwafikie walengwa wote ambao wanastahili kusaidiwa na mfuko huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilisema Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini unafadhiliwa na wadau wa maendeleo lakini hakuna nia ya dhati ya Serikali kusaidia

kaya maskini kwa sababu kuna tofauti ya malipo kati ya walengwa waliopo Dar es Salaam na waliopo Kaliua. Jambo la kwanza nataka nilieleze Bunge lako Tukufu na sijui kwa nini hii habari imeenea hivi, fedha za *TASAF* ni za Serikali ya Tanzania, tumezikopa nje na zitalipwa na Serikali ya Tanzania. Kwa hiyo, maelezo kwamba *TASAF* inafadhiliwa na watu wa nchi za nje si kweli, fedha zile zitalipwa na Serikali yenu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango huu tulipouanza ziko nchi marafiki wakasema katika mambo Watanzania mnayoyafanya mojawapo zuri ni hili la kuhakikisha kila mtu anapata chakula, malazi, nyumba, sisi tutawaunga mkono. Kiwango walichokiunga huwezi hata mara moja ukalinganisha na kiwango ambacho Serikali yenu italipa. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge, wanufaika wa *TASAF* nje huko, Watanzania wenzangu wote muelewe kwamba fedha ya *TASAF* ni fedha inayotoka katika Serikali ya Tanzania inayoongozwa na Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu yangu Mheshimiwa Zitto alisema Serikali inaficha nini kutokana na uamuzi wa kuhamishwa Wakala wa Ndege za Serikali kutoka Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwenda Ofisi ya Rais, Ikulu tarehe 23 Aprili, 2018 kuititia Tangazo la Serikali alilolita. Majibu yake Mheshimiwa Zitto yako hivi, kwa mujibu wa sheria za nchi yetu anayegawa majukumu ya kila Wizara ni Mheshimiwa Rais na inasema Rais atapanga kazi hizo kwa Wizara mbalimbali kwa jinsi atakavyoona inafaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, humu ndani hakuna Waziri aliyejipangia kazi za kufanya wote tumpangawi na Rais. Hata hivyo, hii si mara ya kwanza, hili mbona ni jambo la kawaida. Kwa hiyo, kwa mujibu wa sheria za mgawanyo wa kazi hufanywa na Mheshimiwa Rais, sheria inasema *as he may deem it fit*, kwa jinsi atakavyoona yeye inafaa, siyo kwa jinsi atakavyoona Baraza la Mawaziri au jinsi atakavyoona baada ya kukaa na Abrahman na Mussa, hapana, kwa jinsi

atakavyoona inafaa, nani, Rais. Ndiyo madaraka aliyotumia Rais kufanya hivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka niseme hajafanya hivyo kwetu, kwa mfano, *Tanzania Investment Centre* imehamishwa kutoka Wizara ya Viwanda, Biashana na Uwekezaji imepelekwa Ofisi ya Waziri Mkuu, haikutokea hoja, limeonekana ni jambo la kawaida tu. Basi vilevile ilivyohama *Tanzania Investment Centre* kutoka Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kupelekwa Ofisi ya Waziri Mkuu ndivyo alivyofanya kwa Wakala wa Ndege za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sitaki kufafanua zaidi nisije nikaharibu lakini nataka niseme hao *Air Tanzania* mnaotaka wakabidhiwe ndege zote nane leo leo ndiyo wametufikisha hapa nchi hii ikawa haina ndege. Sasa tumejikusuru tumenunua ndege nane, walewale ambao tayari walishatufilisi si lazima tuwe tunawaangalia kabla hatujawakabidhi kila kitu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana Shirika la Ndege la Tanzania hizi ndege inazikodi kutoka Wakala wa Ndege za Serikali na tuna-*monitor* kila mwezi kuhakikisha wanalipa hela. Kwa sababu shirika lile likifilisika tena Serikali yenu ndiyo itabeba lawama hapa, militafuta hela, mkanunua ndege, mkawapa wabadhirifu walewale, limefilisika tena, mimi nitakuwa mgeni wa nani tena *Air Tanzania* ikifilisika? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana tunasimamia ili kuhakikisha kwamba tunakwenda vizuri kibashara na ili tusilalamike tena kwa sababu watu wengi wamefurahi sana. Nilikwenda kwenu kule ndugu yangu Mheshimiwa Zitto kutembelea Kasulu na sehemu nyingine kwa kutumia ndege hizi mpya. Miaka ya nyuma kabla ya hapo nilikuwa nakwenda na gari, mara ya mwisho nilipokuwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa nilikwenda kwa gari nikitokea Dodoma mpaka Kaliua, ukitoka Kaliua pale pori fulani hivi mnapita, ukiharibikiwa na gari ni wewe na Mungu wako. Juzi naambiwa Mheshimiwa Waziri kwa niaba ya Shirika

la Ndege la Tanzania, safari yetu kwenda Kigoma itatuchukua muda wa saa mbili, nikapewa na peremende na soda, baada ya saa mbili niko Kigoma. Mwenyewe Mheshimiwa Zitto huyu wala haji kwa gari siku hizi, wapongeze *Air Tanzania*. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja kuhusu Wizara yangu ni nyingi sana, nisingependa kupoteza muda wenu, tumeandaa majibu yote, tukishamaliza kikao hiki cha Bunge tutatengeneza kitabu, tulichagua tu maeneo fulani tuyasemee lakini kwa yale maeneo ambayo mmeona hatukusema siyo kwamba hatuna majibu, majibu tunayo tutayaweka katika kitabu na tutawapatia. Nataka nichukue nafasi hii tena kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano mliotupa Wizara yetu. Tumeweza kufanya haya kwa sababu Kamati yetu ya Utawala na Serikali za Mitaa illiomba Bunge litupitishie makisio, mkatupitishia na leo tumekuja hapa kuomba mtuwezeshe tena ili tuweze kutekeleza majukumu tuliyokabidhiwa na Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, sasa tutaendelea na utaratibu wetu, Katibu.

NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 56 - Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Kif. 1001- *Administration and HR Management*
Division Sh. 3,831,328,000/=

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kifungu hiki ndicho chenyе mshahara na kwa mujibu wa kanuni zetu nimeshaletewа majina hapa. Kuna Wabunge ambaо watahitaji ufanuzi. Tutaanza na Mheshimiwa Bonnah Kamoli.

MHE. BONNAH L. KALUWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kama nilivyoongea kwenye hoja yangu nilivyochangia na kama walivyoongea Wajumbe wenzangu kwamba kumekuwa kuna bajeti ndogo sana asilimia 30 kwa TARURA. Sasa nilikuwa ninaomba *commitment* ya Serikali katika hii bajeti ya TARURA tukizingatia kwamba TARURA ndio wenyе mtandao mkubwa na TANROADS kama nilivyosema kwamba barabara zao wameshaunganisha. Sasa nilitaka nijue Serikali inatoa *commitment* gani? Nisiporidhika nitaondoka na mshahara wa Mheshimiwa Waziri, nitaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu waniunge mkono. (*Makofи*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOА NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana dada yangu Mheshimiwa Bonnah kwa mchango wake wa mwanzo. Naomba nimhakikishie kwamba mchango wake wa mwanzo ndiyo mionganoni mwa jambo lilofanya mpaka Serikali imeweza kuongeza takribani shilingi billioni 33. *That is respect number one.* Hata hivyo, ni kwamba kulikuwa na hoja za Wabunge kwa ujumla wake kwamba huu mgawanyo wa asilimia 70 kwa 30 uweze kurekebishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imesikia jambo hili na ndiyo maana sasa hivi Bodi ya Mfuko wa Barabara inafanya tathmini kuhusu jambo hili kuangalia mtandao wote wa barabara halafu, kwa sababu yeye ndiyo mwenye mamlaka, mwisho wa siku tutapata jibu. Lengo ni kwamba kweli

Wabunge walichokisema, jambo hili Serikali inalifanya kazi. Kwa hiyo, hiyo *status* ya Serikali. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bonnah Kamoli, naona umesimama.

MHE. BONNAH L. KALUWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Sawa. Pamoja na majibu ambayo ameongea Mheshimiwa Waziri, namkubali sana na kazi zake na amefanya kazi nyingi sana Jimboni kwangu za kunisaidia pamoja na wananchi wote, lakini bado naona asilimia 33 bado ni ndogo sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bonnah ili tutunze muda, kama hukuelewa majibu yake wewe toa hoja ili Waheshimiwa Wabunge wakuunge mkono halafu utoe shilingi.

MHE. BONNAH L. KALUWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja Wabunge wenzangu waniunge mkono.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja illitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Hoja imeungwa mkono. Sasa wale wanaotaka kuchangia. Waliounega mkono hoja wanawenza wakakaa kama hawataki kuchangia.

Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Mheshimiwa Bobali, Mheshimiwa Mwamoto, Mheshimiwa Amina Mollel na Mheshimiwa Kwandikwa. Haya, hao watakuwa wametosha kwenye hii hoja ya Mheshimiwa Bonnah Kamoli.

Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuunga mkono hoja ya TARURA kuongezewa bajeti. Hiyo aliyozungumzia Mheshimiwa Waziri bado naiona ni ndogo na ninataka Serikali ijkite kuelezea

zile asilimia 40 au 50 wakigawana katikati na watu wa *TANROARDS*. Kwa sababu ukiniambia umeongeza hizo bilioni ulizosema, inaweza ikawa ni mwaka huu, lakini je, kwa mwaka ujao! Tunataka tupange kitu ambacho kitasimamia na kitafanya wenzetu wa *TARURA* waweze kufanya kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kabisa kwamba barabara nyingi sana za vijiji zinahitaji sana bajeti iwe kubwa ili mazao yetu na barabara ziweze kupitika na wananchi waweze kufikiwa kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia kwa mwaka huu, tunakuwa hatujatatu tatizo bado. Hata hiyo aliyosema Mheshimiwa Waziri bado hatujajua kama inaweza ikakidhi bajeti ambapo sisi kama Wawakilishi wa Wananchi tunataka *TARURA* iweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri pamoja na Serikali wajaribu kulifkiria suala ambalo Mheshimiwa Bonnah amelizunguzia kwamba *TARURA* inahitaji pesa zaidi kwa ajili ya barabara zetu ambazo zinaenda kusaidia wananchi wetu wa vijiji. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bobali.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Bonnah. Kwa bahati mimi ni Mjumbe wa Kamati ya TAMISEMI na tumekuwa tukizunguka maeneo mbalimbali kwenda kuangalia miradi ya barabara ambayo inajengwa na *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kuwapongeza *TARURA*, wanafanya kazi kubwa sana. Tatizo liliopo ni mgawanyo mdogo wa fedha, lakini *commitment* waliyonayo na namna wanavyofanya kazi unaonesha kabisa kama tutawaongezea fedha, watafanya mambo makubwa kuliko haya wanayoyafanya. Wana barabara nyingi; wana *community roads*, wana *feeder roads*; na mara nyingi hapa umesikia Wabunge wakiomba barabara zao kupandishwa

hadhi kutoka kwenye *feeder roads* kwenda kwenye barabara za *TANROAD*. Maombi haya yanafanywa ni kwa sababu wanajua barabara zikiwa chini ya *TANROAD* zina matengenezo yaliyo bora kuliko barabara zilizo chini ya *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tupunguze watu kuomba barabara zao zipandishwe hadhi, ni vyema hawa *TARURA* wakapewa fedha za kutosha ili wafanye kazi zao ipasavyo. Kwa hiyo, ninaunga mkono. Nami napendekeza kabisa, badala ya asilimia 30 tuwaongezee angalau wapate asilimia 40 naamini watafanya kazi vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.
(*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zitto Kabwe.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Wakati mwingine ni vigumu sana kupinga hoja ambayo inaonekana ni *popular* ndani ya Bunge. Waheshimiwa Wabunge, naomba mfahamu kwamba nchi yetu hii siyo yote tuko sawa; kuna watu ambao hatujunganishwa kabisa na barabara kuu. Sisi Mkoa wa Kigoma, Wilaya zetu zote kuu kwa maana ya Kasulu, Kibondo na Kigoma havijaunganishwa kwa barabara ya lami. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge ambao tayari mikoa yenu imeunganishwa kwa barabara za lami, mnataka mpunguze fedha za *TANROADS* ziende mkatengenezee barabara za vijijini, sisi hatujapata barabara. Hii siyo haki. Sisi ni Watanzania kama Watanzania wengine. Subirini Kigoma ipate lami iunganishwe kama nyie, ndiyo tuanze kugawana barabara za vijijini. Sasa hivi tusubirini na sisi tupate barabara za lami. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suingi mkono hii hoja mpaka hapo mikoa yote nchi hii itakapokuwa imeunganishwa kwa barabara za lami. Naongea kwa niaba ya wananchi na

Wabunge wote wa Mkoa wa Kigoma waliomo ndani ya Bunge hili. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Amina Mollel.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Ni kweli kabisa tunafahamu katika maeneo mengi na hasa mikoani kwetu na kama walivyotangulia kusema baadhi ya Waheshimiwa Wabunge ili tuweze kufanikiwa katika hili ni kweli kabisa fedha zinahitajika. Pamoja na hayo, tufahamu kazi nzuri inayofanywa na Serikali na Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi tunafahamu ina nia njema katika kuwatetea wananchi wake na katika kuhakikisha kwamba inawaletea maendeleo; na maendeleo yanakuja kutokana na miundombinu ikiwa imeboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba tu Mheshimiwa Bonnah kwamba kwa sababu Serikali tayari imeshasikia, uhitaji ni mkubwa na hii ni Serikali sikivu, namwomba tu Mheshimiwa Bonnah arudishe shilingi ya Mheshimiwa Waziri ili basi kwa sababu tayari Serikali inatusikia nini tunachohitaji tuweze kushirikiana nao katika kuhakikisha kwamba yote yanafanikiwa. *TARURA* kweli wanahitaji fedha, lakini Serikali kilio mmekisikia. Kwa hiyo, Mheshimiwa Bonnah nakuomba sana uweze kurudisha mshahara wa Mheshimiwa Waziri ili basi Serikali iweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwamoto.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Kamoli. Niseme tu wazi kwamba nia nzuri ya kuanzisha *TARURA* ilikuwa ni kuhakikisha kwamba barabara zile ambazo wanatumia watu wengi wa vijijini zinakuwa sawa sawa. Hili jambo lipo kisheria, mgao upo kisheria. Kwa hiyo, naiomba Serikali na ninamwomba Mheshimiwa Zitto Kabwe, ni rafiki yangu, akubali tu kwa sababu Serikali tayari kwa upendeleo mzuri

Iami itakwenda Kigoma na bila kubagua kwamba nani wa chama gani yupo, kwa hiyo, asiwe na wasiwasi, itakwenda mpaka Rukwa, Kilolo na sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kwa kuwa tayari Serikali imeshaonyesha mwelekeo na mpango mzuri wa kuhakikisha kwamba mambo yanakwenda vizuri, basi Mheshimiwa Bonnah Kamoli wewe rudisha ile shilingi ili tuweze kuisimamia Serikali ili mgao uweze kwenda vizuri, lakini mgao uongezeka kwa kweli.

MWENYEKITI: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe tu kwa ujumla zile kanuni zetu zinazokataza kupita katikati ya Kiti na Mbunge anayezungumza. Ni mazingira hayo hayo Kiti hakiruhusiwi kupewa mgongo na Mbunge. Unapotaka kuzungumza na Mbunge mwingine usigeuze kiti unazungumza naye hivi, ndiyo maana viti vyote vimeelekezwa huku ili uweze kusikiliza kama kuna jambo Kiti kinakuagiza uweze kufahamu.

Hapa sitaki kutaja mifano, lakini nawaambia tu kwa ujumla, huruhusiwi kugeuza hicho kiti upande ule ambao Kiti hakipo. Kama unahitaji kuzungumza na Mbunge, unanyanya, unakwenda ama uzungumze naye ukiwa kwa namna ambayo una uwezo wa kuona Kiti. Kwa hiyo, hilo lilikuwa ni la ujumla. Sasa siyo lazima nianze kutaja mifano hapa.

Mheshimiwa Kwandikwa.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKW): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninakushukuru kwa kunipa nafasi, lakini nianze kwa kumwomba Mheshimiwa Bonnah dada yangu hapa kwamba amrudishie Mheshimiwa Waziri shilingi. Hii ni kwa sababu Serikali inafanya kazi jambo hili. Kwa kweli Serikali imekuwa ikilizingatia maoni ya Wabunge, kwa sababu kwa historia utaona kwamba mgao wa mwanzo kwa sheria hii

ilikuwa ni 80 kwa 20, lakini baadaye kwa kuzingatia mahitaji tulikwenda kuwa na mgao huu wa 70 kwa 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa tumekuwa na chombo hiki cha *TARURA* ambacho kinafanya kazi nzuri sana kuweza kufanya tathmini ya barabara zetu za vijijini ili sasa kuja na uwiano mzuri kwa sababu kazi inafanyika vizuri na *TARURA*, amrudishie shilingi Mheshimiwa Waziri akafanyie kazi na sisi tutalisimamia jambo hili ili sasa tuweze kuzichambua barabara hizi na pia kuzilinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaona kwamba barabara zinavyojengwa asilimia 90 ya fedha ni kwa ajili ya kuzirejesha na kuzisimamia, asilimia kumi tu ndiyo inayokwenda kwa ajili ya kutengeneza barabara mpya. Kwa hiyo, linafanyiwa kazi, Mheshimiwa Bonnah nakuomba urudishe shilingi ya Mheshimiwa Waziri tukafanye kazi. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bonnah, mtoa hoja, uhitimishe hoja yako.

MHE. BONNAH L. KALUWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza napenda niseme kwamba nillivyoomba kuongezewa kwa bajeti ya *TARURA* sikusema kwamba *TANROADS* watolewe hizo hizo pesa. Kwa sababu mimi ni Mbunge wa Mjini, nimeomba kulingana na barabara ambazo ziko mjini na nikasoma nikaona kwamba bajeti haitoshi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine nataka niongee kwamba kutokana na *commitment* ya Serikali iliongea hapa, nilitaka niliflikishe hilo kwamba bajeti haitishi, basi nimerudisha shilingi. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaye pia Mheshimiwa Stanslaus Mabula.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nami kwa kunipa nafasi. Wakati wa michango

yangu nilizungumzia juu ya suala la posho za Madiwani. Posho hizi ziko za aina mbili; tunazungumzia posho ya mwisho wa mwezi na posho ya kikao kwa siku. Nimesikiliza majibu ya Waziri, yanatoa matumaini, lakini bado nilitaka nijikite kwenye posho ya kikao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke, Diwani huyu tunayemzungumza hapa ni Diwani ambaye ameachwa na kila Mbunge kule kwenye Majimbo. Diwani huyu ni Diwani anayekwenda kwenye kikao kila baada ya miezi mitatu. Walikuwa na utaratibu wao wa posho; na tukumbuke Diwani mwingine analazimika kutoka kijiji fulani kuja mjini ili ashiriki kikao cha siku inayofuata. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuondolewa kwa posho hizi za siku kunawanyong'onyeza Madiwani hawa na kuwavunja moyo. Kwa hiyo, nilitaka Mheshimiwa Waziri wakati Serikali inashughulikia ile posho ya mwezi, basi iangalie hii posho ya siku ili tuone.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo yasiponiridhisha, nakusudia kushika shilingi na nitaomba Wabunge waliunge mkono.

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha. Mheshimiwa Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze mtani wangu Mheshimiwa Stanslaus kwanza kwa hoja yake nzuri na ndiyo maana wakati nilipokuwa najibu nilikiri wazi kwamba hoja hii ni nzuri yenyе mashiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nimezungumza wazi katika suala la posho ya vikao kwamba hili jambo tunaenda kulifanyia kazi. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunaenda kulifanyia kazi vizuri

na hili wala lisimpe shida, hii ni kazi kubwa ya ofisi yetu, tutaenda kulifanyia kazi na matunda mazuri yataenda kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge. Tena hana hata sababu ya kushika shilingi kwa sababu nimeshatoa *commitment* kwamba tunaenda kulifanyia kazi haraka iwezekanavyo. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Stanslaus Mabula.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ameongea vizuri, nami lengo langu ilikuwa ni kupata *commitment* hasa ya Serikali. Naombe basi atembee kwenye maneno haya na iwe haraka sana kuliko kuchukua muda mrefu zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Japhary Michael.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi kubwa ambayo Waziri anafanya, lakini nilikuwa nime-*raise* hoja ya kanuni za uchaguzi, ikihusiana na tangazo la Serikali kwamba Uchaguzi wa Serikali za Mitaa sasa utafanyika mwezi wa Novemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali ya kawaida, kama tayari kuna tangazo la Serikali la kufanya uchaguzi mwezi wa Novemba, tulitegemea sasa Vyama vya Siasa ambaeo ni wadau wakubwa waruhusiwe kufanya mikutano ya kisiasa ili wajilande kwa ajili ya uchaguzi huo. Mpaka tunavyozungumza sasa hivi hapa, Vyama vya Siasa havifanyi kazi za siasa. Sasa huo uchaguzi utakuwaje ni uchaguzi *fair* kama Vyama vya Siasa havishiriki katika hilo zoezi la uchaguzi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali kupitia kwa Waziri itoe tangazo la kuondoa zolio la Serikali la kuzuia Vyama vya Siasa kufanya mikutano ili vijiandae kwa ajili ya huo uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama majibu ya Mheshimiwa Waziri hayataniridhisha, nitaomba kutoa hoja ya kushika shilingi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ufanuzi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Japhary na Waheshimiwa Wabunge wengine wote kwa ushiriki mzuri katika suala zima la mjadala wa kanuni zile. Nikiri wazi kwamba kwa kweli kanuni zetu zimepata mafanikio mazuri kwa sababu wadau wote wameshiriki kwa njia moja au nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii anayoizungumzia, nikiri wazi kwamba katika kanuni zile zinazungumzia mchakato mzima wa uchaguzi wakati wa uandikishaji na wakati wa kampeni. Sasa kwa suala la kwenda katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa, kanuni zimeonyesha wazi kwamba kuna kipindi gani ni cha kampeni ambao watu wataenda kushiriki katika kampeni. Kwa hiyo, nadhani haliko vibaya kwa mujibu wa zile kanuni, *unless otherwise* kama kuna jambo lingine la ziada hapo. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Japhary naona umeelewa, umeamua ku...

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba Ofisi ya Rais ndiyo inayosimamia chaguzi kwa maana ya TAMISEMI. Tayari taratibu zote za chaguzi zimeshaandaliwa. Sasa tunakwenda kwenye hizi chaguzi wakati wadau hawaruhusiwi kushiriki katika shughuli za kisiasa. Kwa hiyo, nilikuwa naomba nitoe hii hoja ili angalau Wajumbe wengine wajadili tuone *way forward* ya jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Hoja imeungwa mkono. Sasa wabaki wamesimama wale wanaotaka kuchangia hoja hii. Mheshimiwa Aida Khenani, Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Mheshimiwa Kangi Lugola, Mheshimiwa Magereli.

Mheshimiwa Aida Khenani.

MHE. AIDA J. KHENAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja kwa sababu shughuli anayoizungumzia mto hoja siyo kwenda kufanya uteuzi bali ni uchaguzi na huo uchaguzi ina maana unazungumzia mambo ya shughuli za kisiasa. Kwa namna yoyote ile lazima vyama vya siasa vifanye majukumu yake na kwa namna hiyo ni vyema tu kama Serikali wakawa *fair* kwenye hili jambo, wala halihitaji hata kuomba kwa sababu liko kwa mujibu wa sheria za nchi yetu. Kwa hiyo, ni vizuri kama kweli wanaamini wanachokwenda kukifanya na wanajua wanachokifanya kwa sababu wametuhakikishia hapa kwamba ushindi upo na kama upo huwezi kujipiga mwenyewe na ukajisifia, acha vyama vya siasa vifanye kazi zake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni busara tu itumike, hakuna haja ya kuvutana, Serikali inajua kwamba hili jambo liko kwa mujibu wa sheria, waache vyama vifanye kazi yake. Vyama vimesajiliwa siyo kwa ajili ya kwenda kusubiri uteuzi, ni kwa sababu ya kutimiza majukumu yao ya kisiasa, hawa wenyeviti hawateuliwi na Rais, wanachaguliwa kutoka kwenye vyama vya siasa. Vyama vitajuaje nani anastahili kuwa kiongozi, lazima vikafanye kazi yake vitimize wajibu wake kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Marwa Chacha Ryoba.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kilichozuiwa ni mikutano kabla ya kampeni na ratiba za kufanya kampeni ziko kwenye utaratibu wake zimetolewa. Sasa, unajua ili chama cha siasa kishinde kitu cha kwanza lazima uhakikishe kwamba chama chako kinakuwa na *roots*, mizizi kule chini na shughuli kama hizi za kutengeneza chama kule chini, kwa mfano CHADEMA, wana CHADEMA ni msingi *they are doing*, hakuna anayewazuaia wasifanye CHADEMA ni msingi. Endeleeni na CHADEMA ni msingi, *then* kwenye kampeni tupambane, leo unataka ukafanye kampeni kwa nani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naungana na Serikali kwamba, mikutano isifanyike mpaka kampeni zitakapoanza, *full stop*. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lucy Magereli.

MHE. LUCY S. MAGERELI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa fursa. Naomba kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Japhary pamoja na kwamba nimesikia majibu ya Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI. Mheshimiwa Waziri anakumbuka alikutana na wadau wa vyama vyaa siasa ambaao walikuja kumpa maoni na namna wanavyoona na kuna maeneo ambayo ni *very critical* ambayo kwa kweli hawajayafanya mabadiliko. Zile siku saba ambazo walisema ndizo siku za kampeni, hazitoshelezi mgombea kujitangaza, kujieleza, kueleweka kwa wapiga kura, naamini hili la kufanya siku saba walikuwa wana hoja ambayo siyo yenewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri anisaidie, hivi ni sheria ipi inayovizua vyama vyaa siasa vyenye uwakilishi katika maeneo yako kufanya siasa, lakini je, ni sheria ipi inayowapa fursa vile vyama siasa ambavyo havina uwakilishi Bungeni kufanya siasa, kueleza sera na kupata fursa ya kuchaguliwa? Linasemwa tu, viongozi, Wabunge waliochaguliwa kwenye maeneo yako wanaweza kufanya siasa, lakini jana tu, juzi

tumeshuhudia Mheshimiwa Kubenea, Mbunge wa Ubungo amezuiliwa kufanya mukutano wake wa kisiasa, kuongea na wapigakura na wakati huo huo siku mbili zilizotangulia, Mheshimiwa Polepole alikuwa Ubungo anafanya siasa, tuondoe *double standards*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuunga mkono Mheshimiwa Japhary kwamba hili linatakiwa kujibiwa kwa usahihi na Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwigulu Nchemba.

MHE. MWIGULU L. NCHEMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, siiungi mkono hoja iliyotolewa na sababu kubwa ni kwamba, moja utaratibu unaotumika wa kuwa na mikutano ya kisiasa wakati wa chaguzi ni taratibu *standard* duniani kote, hivi ndivyo inavyotumika. Hakuna nchi ambayo kila wanapomaliza uchaguzi wanaendelea na kampeni kama kawaida, hata zile ambazo wanasema demokrasia zao zimekuwa, wanatumia utaratibu huu tunaotumia sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ninachokisisitizia ni kwamba utaratibu tuliokuwa tukiutumia huu wa mikutano ya holela ya watu kwenda kwenye maeneo yasiyo ya kwao na kufanya mikutano, umetusababishia kupoteza maisha ya Watanzania na wale waliohusika na taratibu hizo hata zile familia walizozisababishia kupoteza watu wao hawaziangallii tena. Kwa maana hiyo, utaratibu aliota Mheshimiwa Rais wa mikutano ya kisiasa kufanyika wakati wa chaguzi ni utaratibu *standard*, hata tukaenda Marekani, tukaenda Uingereza, hivi ndivyo wanavyotumia. Kwa maana hiyo hata hapa kwetu kwa sheria, sheria zinalekeza hiki hiki ambacho tunakitekeleza, hamna sheria inayovunjwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, nadhani Waheshimiwa tusiendelee kutumia mazoea kama sheria, twende kwenye utaratibu wa kisheria na twende kwenye utaratibu ambao utawahakikishia wananchi wetu usalama wa maisha yao. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kangi Lugola, Mheshimiwa Zitto umevumiliwa sana na kiti siyo kwamba husikiki ama huonekani, unasikika na unaonekana. Mheshimiwa Kangi Lugola.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyezekiti, kwanza kabisa sikubaliani na hoja ya Mheshimiwa Japhary anayopendekeza kwamba kwa kuwa uchaguzi unakuja Novemba, basi kuanzia sasa vyama vyaa siasa viruhusiwe kufanya mikutano. Mikutano ambayo naamini alikuwa analenga ni mikutano ya kampeni na mikutano ya kampeni itafanyika ndani ya ratiba itakayotolewa na TAMISEMI, kwa hiyo wasubiri ratiba itakapotolewa hakuna chama hata kimoja kitakachozuiwa kufanya mkutano wake wa kampeni. Vyama vyote vyaa siasa ikiwemo CCM, haviruhusiwi kufanya mikutano ya hadhara wakati wowote wanaotaka wao bila kupata vibali kwa mujibu wa Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi, Sura ya 322, Kifungu cha 43 na cha 44.

Mheshimiwa Mwenyezekiti, kwa hiyo tunachobishana hapa ni suala la utaratibu, hakuna chama kinachozuiwa. Kwa hiyo wakifuata utaratibu kwa mujibu wa sheria hii Mkuu wa Kituo cha Polisi katika eneo lile atakutana nao. Akiona kwamba mazingira hayaruhusu, atawaambia wasifanye mkutano, akiona mazingira yanaruhusu, maana yake sisi jeshi la polisi tunaangalia pamoja na vitendea kazi, tunaangalia pamoja na ikama ya askari, pamoja na vifaa tulivyonavyo kuona kwamba tunaweza tukahudumia hivi vyama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyezekiti, kwa hiyo wasiwe wanaangalia sheria nyingine tu, kwamba kuna Sheria ya Vyama, kuna Sheria ya Serikali za Mitaa, kuna Sheria ya Jeshi la Polisi na yenyewe inatakiwa iheshimiwe sawa na wanavyotaka sheria nyingine ziheshimiwe. Kwa hiyo, kupitia hoja hii ni kwamba vyama vyote vyaa siasa haviruhusiwi kufanya mikutano ya hadhara mpaka wasubiri ratiba itakayotolewa na TAMISEMI kwa ajili ya mikutano ya hadhara, vinginevyo wakitaka kufanya mikutano wataleta maombi yao halafu Jeshi la Polisi litayaangalia pale

watakaporuhusiwa, wataruhusiwa; pale ambapo hawataruhusiwa watapewa na sababu ili tusilet machafuko na kuvunja amani. Ni amani, usalama na utulivu wa nchi hii, haiwezekani katika siku 365 katika mwaka, tukawa na siku chache tu za kufanya maendeleo, sasa hii bajeti tunayopitisha ya maendeleo inaenda kufanya kazi gani kama wakati wote ni masuala ya kufanya mikutano ya hadhara. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mto hoja Mheshimiwa Japhary.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, amani katika Taifa inajengwa na wananchi wote na pande zote zikiwa zinaridhishwa na huo utaratibu na hasa tukiwa tumesimamia misingi ya Katiba yetu, kwa sababu wote hatujaona sheria ambayo inakataza vyama vya siasa visifanye kazi yake. Hilo nimesema ni zuio la Mheshimiwa Rais na nikasema uchaguzi ni *process*, sasa hivi sizungumzii kampeni nazungumzia kwamba kuna zoezi la kuandikisha wapigakura wakazi, mpaka kufikia zoezi la kuteuwa wagombea, mpaka uchaguzi wenye hiyo ni *process* inahitaji *activities* za vyama vya siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna zuio la Mheshimiwa Rais na zuio la Mheshimiwa Rais ni amri kubwa sana ambayo lazima wasaidizi wake watekeleze, inawezekana watu wakawa kwenye *process* hiyo, wakaonekana kama wanafanya mikutano ya hadhara, matokeo yake wakaadhibiwa bila sababu yoyote. Ndiyo maana nikasema, kwa sababu tunaenda kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa ni vema lile zuio la Serikali lingondolewa ili *activities* za kisasa zifanyike. Hiyo ndiyo amani tunayoizungumzia, amani siyo ya upande mmoja, amani haiwezi kuwa upande wa CCM tu halafu isiwe ya upande huu mwengine, ili mradi hivi vyama viro kwa mujibu wa sheria, kwa mujibu wa Katiba, navyo lazima viruhusiwe kutumiza wajibu wake ili watu wote wawe pamoja katika Taifa lao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa utengamano wa Taifa hili, kwa utulivu wa Taifa hili, kwa upendo na mshikamano wa Taifa hili, turuhusuni vyama vyasi vifanye kazi yake kuelekea uchaguzi. Kwa hiyo kama Serikali inaona kwamba haioni ulazima huo, namna gani kwamba wako wana *pride* ya amani wenye sisi hatuna hiyo *pride* ya amani, niombe jambo hili liamuliwe kwa kura ndani ya Bunge hili. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wajumbe, sasa nawahoji kwa hoja ya Mheshimiwa Japhary Michael.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja illiamuliwa na Kukataliwa)*

MWENYEKITI: Wasioafiki wameshinda, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni mkakati wa Serikali kuwalinda wanafunzi wa kike wasipate mimba na hasa wale wa sekondari na ndani ya mkakati huo wa kuwalinda wanafunzi wa kike ni pamoa na kujenga shule za mabweni. Imedhihirika na imebainika kwamba Serikali suala la kuwalinda wanafunzi wasipate mimba kwao siyo muhimu na ndyo maana hawatengi fedha za kuweza kujenga shule za mabweni na hata fedha zikitengwa ni fedha za wafadhili kama inavyoonekana kwenye *Subvote 2004 - Basic Education Coordination Division* ya Mheshimiwa Jafo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *commitment* ya Serikali, naomba Serikali ituambie ni kwa nini imekuwa ikipuuza kutotenga fedha za ndani kwa ajili ya kuwalinda wanafunzi wa kike wasipate mimba, badala yake kunakuwa na fedha za wafadhili ambazo huwa hazitolewi na tatizo hili limekuwa likiendelea, kama sikupata maelezo mazuri naondoa shilingi ya Mheshimiwa Waziri mapema. Nashukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI uafanuzi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru kaka yangu kwa hoja zake nzuri *zinazo-base* katika mambo ya elimu, lakini Serikali ina *mechanism* mbalimbali za kufanya kitu kinaitwa *resource mobilization* na ndiyo maana hapa mwanzo nilizungumza kwamba, zaidi ya shilingi bilioni 56 ambayo tunaenda kujenga zaidi ya mabweni 200 *plus*, lakini kuna fedha ambazo mmeona hapa kuna mabweni ambayo nimezungumza hapa zaidi ya 300 yanaenda kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kazi kubwa ya Serikali, hata hivyo kuna mabweni mengine yameendelea kujengwa kwa wakati mbalimbali, fedha hizi ni fedha ambazo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Inapowekwa katika mfumo mkubwa inasema kipi kifanyike na fungu gani, hiyo ndiyo maana ya Serikali. Kwa hiyo, Serikali iko *committed* kwa kiwango kikubwa. Ukiangalia hata hii orodha ya idadi ya mabweni niliyozungumza hapa, yote yanaenda kujengwa, ni kwa ajili ya nia njema ya Serikali kuhakikisha kwamba wananchi hasa watoto, wasichana wanalindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kaka yangu Masoud aelewe kwamba Serikali ina nia njema sana kuliko maelezo. Naamini kwamba hiyo shilingi itaishia tu hapa kaka yangu, nadhani amenielewa vyatatosha. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masoud.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemskia Mheshimiwa Waziri akieleza maelezo yake. Hoja yangu ya msingi katika *Subvote 2004 - Basic Education Coordination Division...*

MWENYEKITI: Sasa Mheshimiwa Masoud, kama una lengo la kutoa shilingi kwa sababu utapewa tena nafasi ya kuhitimisha hoja yako. Kwa hiyo lazima tuutunze muda wetu vizuri, kama unataka watu wakuunge mkono wewe toa hoja waunge mkono hoja yako ijadiliwe, ama kama unarejesha shilingi...

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja ili wenzangu waniunge mkono juu ya suala hili.

MWENYEKITI: Hoja imeungwa mkono Waheshimiwa Wabunge, sasa wabaki Wabunge wanaotaka kuchangia hoja hii. Mheshimiwa Maftaha, Mheshimiwa Mbatia, Mheshimiwa Mwijage, Mheshimiwa Ally Keissy, Mheshimiwa Kiula, Mheshimiwa Profesa Ndalichako. Mheshimiwa Maftaha.

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Masoud kwa sababu suala hili la wanafunzi kuzuiwa kupata ujauzito kwa kujenga mabweni ni jambo la msingi sana. Wakati fulani nilikuwa Mkuu wa Shule ya Sekondari Mchinga, mionganoni mwa mambo ambayo tuli-*discuss*kwa muda mrefu sana na tukaandika sana kuandikia Wizara, ni hizi shule za Kata kuweza kuwa na mkakati mahususi wa kujenga mabweni kwa sababu inaonesha na uzoefu unaonesha kwamba, kipindi kile ambapo tulikuwa tunachukua watoto na kuwaweka shulenii wakawa wanakaa kama kambi walikuwa wanafanya vizuri sana hawa watoto wa kike na watoto wa kiume. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la kujenga mabweni siyo tu kwamba linaondoa ujauzito, bali pia linaongeza ufaulu wa hali ya juu kwa wanafunzi wetu kwa sababu watoto wanapata muda mwangi wa kujisomea usiku, wanapata muda mwangi wa kukaa pamoja *ku-discuss* na mwisho wa siku kuweza kufanya vizuri zaidi. Kwa hiyo, naunga mkono hii hoja kwamba kuna ulazima wa Serikali kuwa na mkakati mahususi wa kujenga mabweni katika shule zote za kata na shule zile nyingine za Serikali ili tuweze kuboresha elimu yetu na kuongeza ufaulu. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbatia.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Lengo la nne la maendeleo endelevu ya dunia ni elimu bora, sawa, shirikishi kwa wote. Tunategemea zaidi ya

usawa jinsia zaidi ya asilimia 40 mpaka 50 ifikapo mwaka 2030, hili ni janga la kitaifa. Mkoa wa Tabora tu mwaka juzi zaidi ya wanafunzi 71,000 walipata ujauzito kati ya miaka 14 na 19; Mwaka jana 44,000; kitaifa ni janga takriban asilimia 27 ya mabinti wetu wako kwenye hali mbaya. Ili kuweza kufikia hata huo usawa wa jinsia nashauri Serikali ikubali kwamba utu wa mwanadamu kwanza, miundombinu baadaye, hili ni suala utu, utu, utu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo Serikali ikubali kuongeza fedha hizi tuokoe mabinti zetu ili waweze kukuza utu wao, wana haki katika jamii ni zaidi ya asilimia 50 ya Watanzania wote, tuweze kupata mabinti wengi jinsia ya akinamama hii iweze ikapata uhalali kwa kushiriki kwenye maendeleo na uongozi na hasa uongozi wa kisiasa, vyombo vya kufanya maamuzi katika jamii. Kwa hiyo naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Masoud kwamba fedha hizi ziongezwe kwa maslahi endelevu na shirkishi kwa watanzania wote bila ya ubaguzi na kumung'unya maneno tu hasa jinsi hii tuifanye kwa vitendo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwijage.

MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nimemwelewa vizuri Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI na maelezo yake kwenye kitabu chake. Ni kwa misingi hiyo nimesimama kumsihi Mheshimiwa Masoud kwamba kwa mipango ya Waziri huyu alivyoelezea njia zake za *ku-mobilize resources* ikiwemo ile kushirikisha wananchi kwamba wajenge maboma ye ye aje ayavamie ayamalizie, tumuache aende kwa sababu mzingo alionao ni mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapozungumza shule za Kata zaidi ya 5,000, sasa tukisema bajeti ya shule 5,000 bwana huyu atengeneze mabweni, tunataka kumtwisha punda mzigo ambao itabidi punda afe. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Masoud tumwache bwana huyu aende

tukajenge maboma kule halafu baada ya kujenga maboma atatukuta mbele ya safari atupe mabati, atupe sementi, atupe vitanda watoto wa kike wakae mabwenini. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Ally Keissy.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza namwomba Mzee Mbatia afute kauli yake kwamba 71,000 Tabora peke yake walipata mimba, ifutwe kabisa. Mimi siamini kama wanafunzi 71,000 walipata mimba Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja ya Mheshimiwa Masoud kwa kuwa wanafunzi wanapata mimba hata wakiwa likizo sasa ina maana kwamba watoto wakae bila likizo? Kwanza tupate hesabu wanaopata mimba wakiwa shulen na likizo, nina hakika wakati wa likizo ndiyo mimba nydingi zinaingia. Kwa hiyo, hakuna sababu maalum ya kusema tujenge mabweni kwa sababu ya wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siungi mkono hoja kwa sababu wanafunzi wengi wanapata mimba wakiwa likizo kwa wazazi wao wenyewe. Wanakwenda *disco*, video mpaka saa saba usiku, ni wazazi waangalie watoto wao vizuri wanapokuwa likizo. (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, sasa tumsikilize Mheshimiwa Kiula.

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nishukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia. Kwanza kabisa, nimwombe Mheshimiwa Masoud amrudishie tu Waziri shilingi ili tuendelee kufanya kazi. Tumeona nia nzuri ya Waziri kwenye hotuba yake ukurasa wa 123, kuna shule maalum zinajengwa 26 lakini ukurasa unaofuata kuna mabweni 300 ambayo yanajengwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Waheshimiwa Wabunge tukubaliane kwamba huo kwa sasa hivi ndiyo uwezo wa Serikali kwa sababu keki iliyopo ni ndogo na pesa

hizi zinakwenda katika Wizara mbalimbali kuleta maendeleo. Kama alivyosema Mheshimiwa Mwijage, sisi tujenge kwenye kata huko halafu tuombe pesa za kufunika hayo maboma na kuleta miundombinu mingine, itakuwa ni jambo jema. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa aweze tu kumrudishia Waziri shilingi ili tuweze kusonga mbele. Ahsante. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Prof. Ndalichako.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na ningeanza kwa kumwomba Mheshimiwa Masoud arudishe shilingi ya Mheshimiwa pacha wangu Jafo ili tuendeleze kazi nzuri katika sekta ya elimu. Napenda tu kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali hii inawathamini sana watoto wa kike na ndiyo maana Bunge lako Tukufu lilipitisha sheria kwa mtu ye yeyote ambaye anaharibu au anakatisha ndoto za watoto wa kike kupata elimu miaka 30 jela inamhusu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba ulinzi wa mtoto wa kike unaanza na mzazi mwenywewe. Tumeshuhudia baadhi ya maeneo watoto wa kike wanaruhusiwa kwenda kucheza ngoma (vigodoro usiku) halafu leo hii Serikali inaambiwa kwamba haimlindi mtoto. Serikali hii imefanya kazi kubwa sana, tayari mabweni zaidi ya 367 yamejengwa kwa ajili ya watoto wa kike, imanzisha elimu ya unasihi shulenii ili kutoa nafasi na mahali ambapo mtoto wa kike kama ana changamoto anaweza kwenda kuzzungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata katika bajeti hii ambayo tunawaomba Waheshimiwa Wabunge waipitishe iko mipango ya kuendeleza mabweni na ulinzi kwa watoto wa kike. Kwa hiyo, suala la kusema kwamba Serikali haitengi fedha si sahihi kwa sababu fedha ambazo Serikali imetenga zinaonekana katika vitabu vyetu na tunaomba Waheshimiwa Wabunge waipitishe. Ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa mtoa hoja hitimisha hoja yako, Mheshimiwa Masoud.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Niwapongeze Waheshimiwa Wabunge sita waliochangia lakini nataka nimwambie tu Mheshimiwa Waziri wa Elimu, tufahamiane kwamba ukienda kwenye *Vote 56, subvote 2004, basic education coordination division, item 4312* na 4590 zote zinafafanua zitajenga shule hizo, fedha zilizotengwa ni za wafadhili na hiyo ndiyo hoja yangu. Ni kwa nini Serikali isiandae mazingira ya kuwajali wanafunzi hawa kupambana na suala hili la kupata mimba kwa kuweka fedha za ndani na hiyo ndiyo yangu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninacho kitabu hiki hapa, angalia kwenye *subvote 2004, item 4512* na 4590, *Tanzania secondary education quality improvement* Mheshimiwa Waziri ipo. Haya mambo yapo na vitabu na randama hivi hapa, kila kitu ninacho. Hoja iliyo mbele yetu mwaka jana Serikali halkutenga fedha hizo na mara hili fedha ambazo wameweka ni fedha za wafadhii ambao fedha hawaleti kwa sababu zao mbalimbali. Mtuambie sasa mkakati wenu wa ziada wa kuwalinda wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba Bunge liamue kwa sababu hamtaki kuweka fedha za ndani, mmeweka fedha za wafadhili ambao hawatoi fedha. Naomba Bunge liamue kwa sababu bado sijaridhika.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Mheshimiwa Masoud.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, pamoja na hii hoja Mheshimiwa Masoud ni muhimu kuyatenganisha haya mambo mawili, ukiunganisha moja kwa moja mabweni na ujauzito kidogo inakuwa tunaenda mbele, tunarudi nyuma. Mabweni yanajengwa ili elimu ya mtoto wa kike anayopata kama anaenda mwendo mrefu apate na yeye haki sawa na mtoto wa kiume. Sasa ukiweka kwa namna ambayo bweni litazuia mimba tutajenga hayo mabweni na kama

hatuchukui hatua kama viongozi mimba zitaendelea kuwepo hata mabweni yakiwepo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lazima sisi kama viongozi tutenganishe haya mambo mawili, mimba ni mojawapo ya jambo linaloweza kutokea lakini si pekee kwa sababu pia mtoto anaweza akafeli ila viwango vyake vyta elimu vinapanda ikiwa atawezeku kaa eneo ambalo yuko salama na yuko karibu na shule. Hata sisi huko tunakoomba misaada ili waje kutusaidia tuone namna ya kuweka lugha, ukiweka kuzuia mimba peke yake, wako wanaosoma shule za bweni na wanapata mimba, sisi kama viongozi lazima tuchukue hatua.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Julius Kalanga.

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Wakati Waziri anahitimisha alieleza habari ya ujenzi wa hospitali mpya lakini kama ambavyo Serikali imeamua kuboresha huduma za afya katika maeneo mbalimbali nchini, hospitali nydingi za zamani zimechakaa na zingine hazina miundombinu na nydingine hazijakamilika lakini inaonekana Serikali sasa inajikita zaidi katika kujenga hospitali mpya. Nataka *commitment* ya Serikali kwamba ina mpango gani kuboresha afya katika hospitali zile za zamani ambazo mpaka sasa hazijakamilika.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, ufanuzi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Julius Kalanga kwa kazi kubwa anayofanya kule jumboni kwake na nikiri wazi kwamba nimefika mara kadhaa kule, anafana kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lengo letu kuhakikisha kwamba miundombinu hii inakamilika. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge licha ya ujenzi mpya

wa hospitali za wilaya lakini tuna mkakati vilevile wa kuendelea kuzihuisha zile hospitali za wilaya ambazo ziko katika hali mbaya. Ndiyo maana mwaka huu ukiangalia katika orodha unaikuta Hospitali ya Kongwa na Hospitali ya pale Kwigwa, hii ina maana kwamba tumeanza kazi hii. Pia katika mpango huo tuna Hospitali za Magu, Mkuranga, Monduli na maeneo mengine. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba tutaziboresha hizi hospitali zote na zitakuwa katika malengo ambayo Mheshimiwa Mbunge anayazungumzia hapa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kalanga, naona umesimama.

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeridhika na maelezo ya Waziri. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji kuhusu kifungu hiki.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1002 – *Finance and Accounts Unit*.....Sh.747,643,000/=

Kif. 1003 – *Policy and Planning Division*..... Sh. 948,118,950/=

Kif. 1004 – *Information, Communication and*

Technology Division.....Sh. 3,238,926,000/=

Kif. 1005 – *Legal Services Division*..... Sh. 601,187,000/=

Kif. 1006 – *Internal Audit Unit* Sh.410,144,000/=

Kif. 1007 – *Government Communication*

Unit.....Sh.339,592,000/=

Kif. 1008 – *Procurement Management*

Unit.....Sh. 503,724,000/=

Kif. 1009 – *Infrastructure Development*

Division Sh.21,105,611,653/=

Kif. 2001 – *Regional Administration*

Division.....Sh.580,021,000/=

Kif. 2002 – *Local Government Division*..... Sh.5,738,450,112/=

Kif. 2003 – <i>Sector Coordination Division</i>	Sh. 857,425,000/=
Kif. 2004 – <i>Basic Education Coordination Division</i>	Sh.12,261,841,500/=
Kif. 2005– <i>Urban Development Division</i>	Sh.754,698,592/=
Kif. 2006 – <i>Inspectorate and Finance Tracking Unit</i>	Sh.372,808,193/=
Kif. 2007 – <i>Health, Social Welfare and Nutrition Services</i>	Sh.762,968,000/=
Kif. 3001 – <i>Management Services Improvement Unit</i>	Sh. 382,683,000/=

(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni zetu na muda uliokuwa umetengewa Ofisi ya Rais TAMISEMI umeisha sasa tutapitia mafungu yote kwa pamoja, Katibu tunaendelea.

Fungu 2 – Tume ya Utumishi wa Walimu

Kif. 1001 – <i>Administration and Human Resource</i>	Sh.1,501,630,000/=
Kif. 1002 – <i>Finance and Accounts Unit</i>	Sh.105,615,000/=
Kif. 1003 – <i>Planning, Monitoring and Evaluation Unit</i>	Sh.122,332,000/=
Kif. 1004 – <i>Internal Audit Unit</i>	Sh. 80,903,000/=
Kif. 1005 – <i>ICT and Statistics Unit</i>	Sh. 69,706,000/=
Kif. 1006 – <i>Government Communication Unit</i>	Sh.67,153,000/=
Kif. 1007 – <i>Legal Unit</i>	Sh. 81,356,000/=
Kif. 1008 – <i>Procurement Management Unit</i> ..	Sh. 60,753,000/=
Kif. 2001 – <i>Recruitment and Development Division</i>	Sh.1,309,864,000/=
Kif. 2002 – <i>Teachers Service Commission – District</i>	Sh.12,501,845,000/=

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

NDG. MOSSY LUKUVI - KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuchukue Kitabu cha III (*Volume III*) kwa ajili ya bajeti za mikoa, ukurasa wa pili.

KITABU CHA TATU

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 36 – Mkoa wa Katavi

Kif. 1001 – <i>Administration and Human Resources Management</i>	Sh.985,896,800/=
Kif. 1002 – <i>Finance and Accounts Unit</i>	Sh.106,956,000/=
Kif. 1003 – <i>Internal Audit</i>	Sh. 66,600,000/=
Kif. 1004 – <i>Procurement Management</i>	Sh.40,130,000/=
Kif. 1005 – <i>DAS – Mpanda</i>	Sh. 307,894000/=
Kif. 1006 – <i>DAS – Mlele</i>	Sh. 334,125,000/=
Kif. 1007 – <i>DAS – Tanganyika</i>	Sh.132,651,000/=
Kif. 1014 – <i>Legal Services Sector</i>	Sh.43,993,000/=
Kif. 1015 – <i>Information and Communication Tech. Unit</i>	Sh.33,474,000/=
kif. 2001 – <i>Planning and Coordination</i>	Sh.185,420,000/=
Kif. 2002 – <i>Economic and Productive Sector</i>	Sh. 228,111,200/=
Kif. 2003 – <i>Infrastructure Sector</i>	Sh.81,195,000/=
Kif. 2005 – <i>Local Gov. Management Services</i>	Sh.110,695,000/=
Kif. 2006 – <i>Education Sector</i>	Sh.192,352,400/=
Kif. 2007 – <i>Water Services</i>	Sh.93,585,000/=
Kif. 3001 – <i>Regional Hospital</i>	Sh.176,547,600/=
Kif. 8075 – <i>Transfers to LGAS – Primary Education</i>	Sh. 20,696,812,052/=
Kif. 8076 – <i>Transfers to LGAS – Secondary Education</i>	Sh.599,613,000/=
Kif. 8078 – <i>Transfers to LGAS – Public Health Services</i>	Sh. 1,724,373,536/=
Kif. 8079 – <i>Transfers to LGAS – Preventive Services</i>	Sh.1,296,851,896/=
Kif. 8080 – <i>Transfers to LGAS – Health Centers</i>	Sh. 1,792,488,401/=

Kif. 8081 – *Transfers to LGAS – Dispensaries*.....Sh.18,492,210/=
Kif. 8082 – *Transfers to LGAS – Works*.....Sh.707,075,000/=
Kif. 8083 – *Transfers to LGAS – Rural Water Supply*.....Sh.441,908,000/=
Kif. 8086 – *Transfers to LGAS – Agriculture*.....Sh.39,256,000/=
Kif. 8089 – *Transfers to LGAS – Planning, Trade and Economy*.....Sh.6,315,307,000/=
Kif. 8091 – *Transfers to LGAS – Administration & General*.....Sh.18,234,409,905/=

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 47 – Mkoa wa Simiyu

Kif. 1001 – *Administration and HR Management*.....Sh.958,454,000/=
Kif. 1002 – *Finance and Accounts Unit*.....Sh.150,852,000/=
Kif. 1003 – *Internal Audit Unit*.....Sh. 76,100,000/=
Kif. 1004 – *Procurement Management Unit*.....Sh.29,944,000/=
Kif. 1005 – *DAS – Bariadi*.....Sh.275,136,000/=
Kif. 1006 – *DAS – Maswa*.....Sh.299,777,000/=
Kif. 1007 – *DAS – Meatu*.....Sh.263,467,000/=
Kif. 1008 – *DAS – Busega*.....Sh.245,883,000/=
Kif. 1009 – *DAS – Itilima*.....Sh.285,075,000/=
Kif. 1014 – *Legal Services Unit*.....Sh.58,100,000/=
Kif. 1015 – *Information and Communication Tech. Unit*.....Sh.18,700,000/=
Kif. 2001 – *Planning and Coordination*.....Sh. 202,460,000/=
Kif. 2002 – *Economic and Productive Sector*.....Sh.205,364,000/=
Kif. 2003 – *Infrastructure Sector*.....Sh.165,552,000/=
Kif. 2004 – *Social Sector*.....Sh.209,680,000/=
Kif. 2005 – *Local Government Management Services*.....Sh.105,500,000/=
Kif. 2006 – *Education Sector*.....Sh.325,301,000/=
Kif. 2007 – *Water Sector*Sh.77,028,000/=
Kif. 3001 – *Regional Hospital*.....Sh.57,780,000/=
Kif. 8075 – *Transfers to LGAS – Primary Education*.....Sh.57,638,055,000/=

Kif. 8076 – *Transfers to LGAS – Secondary Education*.....Sh.22,894,286,000/=
Kif. 8078 – *Transfers to LGAS – Public Health Services*.....Sh. 5,406,079,000/=
Kif. 8079 – *Transfers to LGAS – Preventive Services*.....Sh.1,398,114,000/=
Kif. 8080 – *Transfers to LGAS – Health Centers*Sh.4,020,327,000/=
Kif. 8081 – *Transfers to LGAS – Dispensaries*..Sh.4,017,314,000/=
Kif. 8082 – *Transfers to LGAS – Works*.....Sh.930,173,000/=
Kif. 8083 – *Transfers to LGAS – Rural Water Supply*.....Sh. 661,414,000/=
Kif. 8086 – *Transfers to LGAS – Agriculture*...Sh. 2,628,201,000/=
Kif. 8087 – *Transfers to LGAS – Livestock Operations*.....Sh.1,882,327,000/=
Kif. 8091 – *Transfers to LGAS – Administration& General*.....Sh.19,124,972,000/=

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 54 – Mkoa wa Njombe

Kif. 8083 – <i>Transfers to LGAS – Rural Water Supply</i>	Sh. 0
Kif. 8086 – <i>Transfers to LGAS – Agriculture</i>	Sh. 0
Kif. 8088 – <i>Transfers to LGAS – Water Supply</i>	Sh. 0
Kif. 8091 – <i>Transfers to LGAS – Administration & General</i>	Sh. 9,729,772,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

NDG. MOSSY LUKUVI - KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake kwa Wizara ya TAMISEMI.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Bunge lilitrudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Mtoa Hoja, Taarifa!

TAARIFA

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi likakamilisha kazi yake na kupitisha Bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kifungu kwa kifungu, pamoja na marekebisho ya ongezeko la fedha ya maendeleo katika Fungi Namba 56.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.
(Makof)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa ilihamuliwe)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji kwa mujibu wa utaratibu wetu.

(Hoja Ilihamuliwa na Kuafikiwa)

(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2019/2020 – Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa yalipitishwa na Bunge)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nichukue fursa hii kwa niaba yenu kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Suleiman Jafo, pamoja na Naibu Mawaziri na Ofisi yake nzima na Wataalam wake walioko hapa kwa kuleta bajeti ambayo kwa sehemu kubwa sana imeungwa mkono na Waheshimiwa Wabunge.

Hata Waheshimiwa Wabunge walifanya kazi kwa niaba yetu, kwa maana ya Kamati ambayo inahusika na utawala, tunawashukuru, wamefanya kazi nzuri. Vilevile hata

ninyi mmepokea ushauri, mmebadilisha hapa na pale, kwa hiyo, tuwapongeze sana kwa kazi nzuri.

Tuwatakie kila la kheri kwenye utekelezaji wa yale ambayo mmeomba kwa Bunge na Bunge limeridhia, tunaamini kwamba mnaenda kuifanya kazi hiyo kwa weledi mkubwa kama ambavyo mmekuwa mkifanya siku zote. Kwa hiyo tunawatachia kila la kheri.

Jambo la jumla tu ni kwamba Wabunge hawa pamoja na kufurahi kwa kazi kubwa sana inayofanywa na upande wa TAMISEMI kwa upande wa elimu, afya na mambo mengine wangetamani, nadhani ndiyo maana kulikuwa na maswali maswali hapa, kwamba wale ambaao kama ni shule za zamani ziko maeneo yao zitafikiwa lini hizo shule, kwa sababu ukisema tu 15 zinawezekana zote ni za mkoa ule ule ambaao ulishafikiwa. Vilevile kuhusu ujenzi wa hivvi vituo ambaao unaendelea, ujenzi wa hospitali, tunashukuru umetutajia hapo. Kwa hiyo tuwatakie kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yenu.

Waheshimiwa Wabunge baada ya kusema hayo kwa kuwa lilitokea jambo hapa wakati tukiwa kwenye Kamati ya Matumizi, sasa tunataka kuweka kumbukumbu sawasawa kwenye takwimu zilizokuwa zimetolewa kwa sababu kwenye Taarifa Rasmi za Bunge tutakuwa na taarifa inayozungumzia 70,000 ya wanafunzi kwa Mkoa wa Tabora pekee, taarifa nilizoletewa hapa zinazungumzia mimba, lakini sasa nitalizungumza mwishoni nitakapomaliza Mheshimiwa Waziri ameleta sasa takwimu hapa za mimba ili taarifa zetu zikae vizuri.

Mheshimiwa Waziri ameleta taarifa ambazo ziko kwa asilimia, kwa hiyo sasa zimetaja asilimia kwa upande wa sekondari ni asilimia 8.3, upande wa msingi ni asilimia 1.6. Sasa hizi ili tuweze kujua kama ile 70,000 kwa sababu ile ilitaja idadi, haikutaja asilimia, ili tuwe na hakika na hizi takwimu utaniwekea vizuri hapa ili taarifa zetu za Bunge zikae sawasawa. Nipate idadi ya hizi asilimia ili iwe rahisi kwamba,

mimba si 70,000 katika Mkoa wa Tabora, lakini ni tofauti na hapa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tunaendelea na utaratibu wetu, Katibu.

NDG. MOSSY LUKUVI-KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

**OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA
UTAWALA BORA**

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tukae, Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa kanuni zetu, naongeza nusu saa ili tuweze kumalizia kazi ambayo imesalia. Katibu.

Fungu 32 – Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora

Kif.1001-*Administration and HR Management*.....Sh.12,156,510,477/=

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kifungu hiki ndicho chenyeh mshahara wa Waziri na kwa mujibu wa kanuni zetu, ninayo majina hapa ya watu wanaotaka ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Tutaanza na Mheshimiwa Cosato Chumi.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza napenda kupongeza jitihada mbalimbali ambazo Serikali awamu imekuwa ikizifanya na hatua mbalimbali inazochukua katika kushughulikiwa masuala ya Utumishi wa Umma. Tumeshuhudia wenye Serikali imeokoa mabilioni mengi katika masuala ya watumishi hewa na wale wenye vyeti feki. Hata hivyo, pamoja na jitihada hizi nzuri ambazo zimeokoa mabilioni ya pesa ambayo yataenda kufanya kazi nyingine,

naomba ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, kuna wafanyakazi wengi ambao katika zoezi hilo waliondolewa katika mfumo wa *payroll*/kwa makosa na baadaye ikabainika kwamba waliondolea kimakosa hivyo wakarejeshwa katika mfumo, lakini walikosa mishahara katika kile kipindi ambacho walikuwa nje ya mfumo na mpaka sasa bado wanaidai hayo malimbikizo yao, wako ambao wanadai miezi mitatu, kumi, ni suala ambalo lina *cut across* nchi nzima. Hata hivyo kama utaniruhusu nitatoa mfano wa Mafinga ambako watumishi 51 waliondolewa na wakarejeshwa na wanadai jumla ya milioni 118,164,330. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufanuzi kutoka kwa Serikali na kama sitaridhika nitashika shilingi ili tujadili suala hili.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, ufanuzi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Cosato Chumi kwamba wakati wa uhakiki wako baadhi ya watu waliondolewa kwa makosa, Waraka wa Serikali ulitaka kwamba mtu yoyote ambaye ameona ameoneawa aondolewe kwa makosa akate rufaa kwa Katibu Mkuu Utumishi na iliundwa Kamati pale ya watu sita kutoka Idara mbalimbali wakiwemo Baraza la Mitihani, Polisi, Wataalam wa kufoji wanaoangalia muundo, miandiko ambayo imefojiwa, vyeti vimefojiwa. Kamati ile ndiyo inamshauri Waziri kumwambia kwamba huyu aliondolewa kwa makosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukishapokea taarifa hiyo tunapeleka kwenye nanii yetu *Lawson* yetu pale; Lakini nataka nikubali, imetokea kwamba majina unayaingiza leo, mshahara unatoka baada ya miezi mitatu, baada ya miezi minne. Kikubwa ndugu yangu Mheshimiwa Cosato Chumi nataka tu kumhakikishia kwamba tumechukua hatua ya kuingiza majina yao katika mtandao, wasubiri kulipwa muda utakapofika watalipwa. Hiyo imetokea siyo kwa wao tu hata kuna baadhi tunao hapa Bungeni, waliingia wakaanza

kulipwa mshahara wa mwezi uliofuata ule wa kwanza walipoingilia nadhani bado hawajalipwa na Wizara yangu inashughulikia kuhakikisha kwamba wote wanalipwa. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Cosato Chumi.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri. Hata hivyo, naendelea kusisitiza na ningeomba Waheshimiwa Wabunge kama wataridhia waniunge mkono ili tuweze kujadili jambo hili kwa sababu hoja hapa sasa...

MWENYEKITI: Toa hoja Mheshimiwa.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja tujadili.

MWENYEKITI: Hoja haijaungwa mkono, tunaendelea Mheshimiwa Rashidi Shangazi.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba ufanuzi, sina sana shida na shilingi ya Mheshimiwa Mkuchika kwa sababu najua anatembeza bakuli katika *club* anayoiongoza. Hata hivyo, nataka nipate ufanuzi, wakati kabla Serikali Kuu haijaanza kutoa *cheque* kwa ajili ya watumishi wanaoingia kwenye halmashauri na Idara za Serikali baadhi ya halmashauri zilikuwa zinalipa wafanyakazi kwa kutumia mapato ya ndani, lakini mpaka sasa hali hiyo bado inaendelea kwamba bado Serikali Kuu kuititia Utumishi haijapokea jukumu hili kutoka kwenye halmashauri zetu. Sasa nataka kupata ufanuzi, ni lini suala hili la kuzipokea halmashauri ambazo zinalipa mishahara kwa kutumia mapato yake ya ndani litakamilika?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa

Mwenyekiti, Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefafanua kwamba Serikali maana yake ni Serikali Kuu, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali za Mitaa. Sifa ya Serikali ina uwezo wa kuajiri na kufukuza; kwa hiyo sifa hizo zinahusu aina za Serikali zote hizo nilizozitaja. Serikali ilitoa ruhusa kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa, kwa kutegemea mapato yao waajiri watumishi kwa jinsi watakavyoona inafaa na wanawalipa kulingana na wanavyoona inafaa. Kwa hiyo inawezekana tatizo liko kwa ndugu yangu kule, lakini ziko halmashauri, ukienda kwa Manispaa zote zile za Dar es Salam hawana tatizo la kumwajiri mtumishi wakamlipa sh.200,000 au Sh.300, 000 kwa mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa inawezekana ni tatizo la uwezo wa halmashauri kulipia, sisi tunasema kwamba sisi kiserikali tunafanya, tuna *treat* Wilaya zote, halmashauri zote kuwa sawa, tunaendelea kuajiri watumishi ambao tutawalipa sawa halmashauri zote na bado tunafikiri ni sahihi, kila halmashauri kuwapa uhuru wa kuajiri na kufukuza wale wanaowapata, wanaowalipa kwa *own source*, kwa mapato yao, kwa jinsi watakavyoona inafaa; kuliko tukisema tutalipa wote sisi Serikali kuu, maana yake tunazuia hata wale ambao wana uwezo wa kuajiri wasiajiri, jambo ambalo linaweza kuathiri utendaji kazi katika halmashauri zao.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Shangazi ulisema huna haja na shilingi yake, sasa.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeridhika, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Ruth Mollel.

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ningependa kupata ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Utawala Bora kwamba tangu Awamu hii imeingia madarakani mwaka 2015 haijawahi kupandisha mishahara ya watumishi na ikiwa sitapata jibu la kuridhisha, nitaomba nitoe hoja wenzangu wanisaidie tuweze kulijadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na kauli kinzani kama nilivyoonesha katika hotuba yangu ambapo Mheshimiwa Rais alisema yeye hatoongeza mshahara mpaka uchumi umekuwa mzuri na hatujui huu uchumi utakua lini. Mheshimiwa Waziri wa Utawala Bora yeye akasema akishamaliza mambo ya vyeti *fake* na wale ambao watumishi hewa, basi hili jambo litafanyika halikufanyika. Sasa amekuja na *gearya* kusema kwamba mpaka baada ya hii Kamati ya Kuboresha Mishahara imalize kazi na mimi najua kazi ya *job evaluation* na *job description*, inachukua muda mrefu. Ni kwa nini sasa Serikali isichukue *intervention* hapo katikati ya kuongeza mishahara ya watumishi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mishahara ya watumishi inaongezwa kwa mara mbili; kuna *annual increment* ambayo iko kwenye *standing order* na *standing order* inasema; "an increment is an increase of salary, within salary scales in which the prescribed amount which is granted annually to holder of post on increment of scales of salary until the maximum of the scale is reached. In all cases information obtained through performance appraisal should be used in awarding or withholding increment provided that certain conditions are satisfied." Hii hapa *standing order*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa nini mtu anajua mshahara wake labda toka shilingi 200,000/= mpaka shilingi 500,000/= labda kwa nini hizi *increments* za kila mwaka ambazo ziko provided kwenye *Standing Order* kwa nini hazitolewi? (*Makofii*)

La pili kuna *increment*...

MWENYEKITI: Mheshimiwa ngoja upate ufanuzi kwanza, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu ndugu yangu Ruth Mollel, Katibu Mkuu wa zamani wa Wizara hii ya Utumishi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna ubishi kwamba nchi hii, Serikali ya Awamu ya Tano tangu ilipoingia imeboresha, imeongeza kiwango cha makusanyo ya kila mwezi, hakuna ubishi; tumetoka bilioni nane, tuko *1.3 billion*, tumeongeza bilioni tano kwa mwezi. Fedha ukiwa nayo mkononi Baba wa Taifa alitufundisha kupanga ni kuchagua, katika dhiki zako zote ulizonazo unataka kuanza na ipi, unataka mwongeze mshahara, uwanja wa ndege wa Tabora usikarabatiwe; mnataka hivyo *Standard Gauge* ijengwe na nini na nini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumekaa ndani ya Serikali, tumejipanga tukasema tunataka kwanza *Standard Gauge*, tunataka ukarabati uwanja wa ndege wa Mtwara, uwanja wa ndege wa Tabora, uwanja wa ndege wa Kigoma na tukasema muda utakapofika tutatoa nyongeza ya mshahara. Naona watu wanashambulia, lakini nataka niseme ungewauliza walio na dhiki ya uwanja wa ndege wangekwambia tupe ndege kwanza kwanza. Hilo la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilitaka niseme hivyo. La pili, kabla ya sikuu ya *May Day* tuna kikao cha Serikali na Vyama vya Wafanyakazi, wameorodhesha hoja zao zote ikiwemo na hiyo. Tupeni nafasi tukutane na Vyama vya Wafanyakazi; na huu ndiyo utaratibu wetu kila mwaka tukishakutana naye tutatoa majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *salary increment*, sifichi, hakuna mahali ambapo kumepigwa marufuku na tunasema ni kwa mujibu wa sheria wanapewa nyongeza, lakini mwajiri akikuona kwamba utendaji wako wa kazi wewe ulikuwa hovyo mwajiri ana madaraka ya kusema mwaka huu huna; kwa hiyo siyo *automatic*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ruth Mollel.

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja ili jambo tulijadili.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Hoja imeungwa mkono sasa wabaki Wabunge watakaochangia hoja hii. Mheshimiwa Juma, Mheshimiwa Susan Kiwanga, Mheshimiwa Gimbi Masaba, Mheshimiwa Simbachawene, Mheshimiwa Dkt. Mollel, Mheshimiwa Ole Nasha na Mheshimiwa Jenista Mhagama.

Tunaanza Mheshimiwa Juma.

MHE. JUMA KOMBO HAMAD: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii fupi. Ni ukweli usiopingika kwamba Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi, Serikali ya Awamu ya Tano pamoja na majigambo yote ambayo yanapita, lakini wameamua kuwatelekeza watumishi, kwa sababu hakuna na si hoja ya msingi kusema tunataka kuboresha uwanja wa ndege, tunataka kujenga barabara, tunataka kujenga mahospitali, suala la watumishi ni suala la msingi na ni suala la maisha ya Watanzania. Kwa hiyo, ni wazi kwamba suala la kuongeza mshahara ni suala la msingi na lilifanywa kila mwaka na barabara zilijengwa, hospitali ziliendelea kujengwa, madaraja yaliendelea kujengwa na mishahara ya wafanyakazi iliongezwa kila baada ya mwaka mmoja. Sababu hii haipo kama ni sababu ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Tayari Mheshimiwa ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Susan Kiwanga.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ruth Mollel kwa sababu suala la mshahara ni la kisheria wala siyo makubaliano. Katika llani ya CCM na kampeni zao haijawahi kusema kwamba wakiingia madarakani hawataongeza mishahara ya kisheria, matokeo yake walikuwa wanawapa

matumaini Watanzania. Ndiyo maana kwenye Mkutano wa Wafanyakazi, Mei Mosi-Iringa, wafanyakazi walikuwa *bored* katika *video*, wamesinzia wakati Rais anahutubia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hizo ni haki za watu, achene kuvunja sheria. Kama huu utawala unaheshimu sheria kwa nini mnavunja sheria? Hivi inawezekana kweli una watoto nyumbani una shilingi 10 zote unakwenda kununua matofali na kujenga nyumba watoto wanakaa ndani na njaa? Huo ni unyama na haukulaliki ndani ya nchi hii, tunaongea na wafanyakazi mbalimbali, taasisi za Serikali na za umma...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa, kengele imegonga. Mheshimiwa Gimbi Masaba.

MHE. GIMBI D. MASABA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami naomba nichangie hoja ya Mheshimiwa Mollel na naunga mkono hoja yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii ni ya msingi sana. Tangu Awamu ya Tano iingie madarakani haijawahi kuongeza mishahara kwa watumishi, ni jambo ambalo linasikitisha sana. Mheshimiwa Waziri pale ameeleza kwamba hoja hapo ni kwa sababu Serikali imejipambanua kuleta maendeleo kama *Standard Gauge* na mambo mengine. Siamini kama suala la kuongeza mishahara ya watumishi linaingiliana popote pale na vitu ambavyo tunavifanya hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuongeza mishahara ya watumishi ni takwa la kisheria na wala siyo hisani ya binadamu yoyote hapa duniani. Kwa hiyo, naomba Serikali ione ni jambo la msingi sana kuongeza maslahi ya wafanyakazi na ndiyo maana mnaona hata morali ya kufanyakazi haipo. (*Makof*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Kengele imeshagonga Mheshimiwa, ahsante sana. Mheshimiwa Dkt.Godwin Mollel.

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, suingi mkono hoja ya mama yangu mpendwa Mheshimiwa Ruth Mollel kwa sababu naelewa vizuri sababu ya kizalendo ambayo pamoja na kuongezeka mapato, Serikali imeamua kuwekeza kwenye miundombinu ya kimkakati ili kuboresha maisha ya baadaye ya watoto na ndugu za wafanyakazi na kuongeza viwanda ili kuweza kuajiri watoto wa hao wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni tofauti na CHADEMA ambayo pamoja na ruzuku kuongezeka hawalipi hata mtu mmoja mshahara, wameamua kujinunulia magari na kumpa mtu kwa miaka miwili na akarudisha limekuwa bovu ambapo ni kinyume na sheria na utaratibu. Wameamua kuhakikisha ruzuku yote inaishia kwa wasiojulikana na ni kinyume cha sheria wanatakiwa kushtakiwa fedha zirudi. Kwa hiyo, mimi niseme kwamba suingi mkono hoja yake kwa sababu anayesimama siyo mfano mzuri, siyo tu kwamba hawaongezi mshahara, hawalipi kabisa pamoja na ruzuku kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mollel. Mheshimiwa Simbachawene.

MHE. GEORGE. B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kumsihi dada yangu Mheshimiwa Mollel kuachia shillingi ili Mheshimiwa Waziri aende akawahudumie Watanzania ikiwemo na kuwalipa mishahara yao ya msingi. Nimesema hivi kwa sababu *salary increment* siyo *automatic*, kuna *form* za kujazwa kwa ajili ya kufanya *evaluation*, utaratibu unaitwa *OPRAS* na ukishafanyika ule ndipo mwajiri anaweza akaongeza au asiongeze. Kwa hiyo, kwa sababu Kamati ile inaendelea kufanya kazi hiyo akubali na asubiri utaratibu ukikamilika wataongezwa mshahara lakini siyo *automatic* kama alivyoisoma na kwa tafsiri aliyoisemea, *is not an automatic event*, kwa hiyo nimsihi sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la nyongeza ya mshahara ile inayosemwaga na mamlaka wakati unapofika, Mheshimiwa Rais kwa maneno yake alisema atakapoongeza ataongeza kweli kweli. Kwa hiyo, tusubiri hiyo nyongeza ya kweli kweli. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa William Tate Ole Nasha.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami namwomba sana dada yangu Mheshimiwa Ruth Mollel aachie shilingi ili Mheshimiwa Waziri aendelee kutekeleza wajibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna ubishi kwamba ongezeko la mishahara kwa wafanyakazi ni jambo la msingi na ni kipaumbele cha Serikali lakini pia hakuna ubishi kwamba Mheshimiwa Ruth Mollel ni moja kati ya Watanzania waliobobe a sana katika sekta ya utumishi wa umma. Anafahamu kwamba kwa muda mrefu sekta ya utumishi iliingiliwa na upungufu mkubwa na ikapelekea tukawa na wafanyakazi zaidi ya 34 amba walikuwa wanalipwa lakini wengi walikuwa ni watumishi hewa na vilevile wenye vyeti *fake*. Sasa ilikuwa ni vigumu kuendelea kuongeza mishahara wakati nyumba ya utumishi ilikuwa siyo safi na kwa vyovoyote vile anajua kwamba huu udhaifu umekuwepo kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali ina dhamira hiyo lakini ilikuwa ni muhimu kuendelea kusafisha nyumba hiyo na ikishamalizika ndiyo unaweza ukaongeza kwa sababu ungeweza kuongeza wafanyakazi hewa na wenye vyeti *fake*. Kwa hiyo, naomba aachie shilingi tuendelee kuwashudumia Watanzania. Shukurani sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Jenista Mhagama.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa

Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba kwanza niseme kwamba hakuna kulinzana kati ya hoja ambayo anaieleza Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Utumishi na Mheshimiwa Rais, wote wanazungumza kitu kimoja, naomba niliweke hilo sawasawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tunapozungumzia *welfare* ya wafanyakazi ni pamoja na hiyo mishahara na *increment* lakini *welfare* ya maisha ya wafanyakazi ni pamoja pia na huduma za afya zilizo bora, barabara safi, maji safi na salama wanakoishi, huduma ya umeme vijijini na mazingira yote ambayo yatawasaidia. Ukitazama haya mambo yote kwa sasa, Serikali imeshajidhatiti na kutekeleza mambo makubwa ya awali ambayo yote yanajenga msingi huo huo wa huduma bora kwa wafanyakazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunapoenda kumalizia hayo ambayo yalitangulia ya kuhakikisha wanapata huduma bora za afya, maji salama, barabara, nyumba, vifaa vyta kufundishia na kila kitu, sasa ajenda hii inayofuata baada ya uhakika wa ujenzi wa uchumi wa ndani na tumesema hapa kwa utaratibu huo huo wa kisheria, Waziri wa Utumishi amesema na mimi ni Waziri mwenye dhamana ya wafanyakazi tunao muda wetu wa kukaa mezani, *negotiate* na kuona kero za wafanyakazi tunaendelea kuzitatua moja baada ya nyingine. Kwa hiyo nimuombe dada yangu Mheshimiwa Ruth aelewete tu kwamba Serikali iko kazini itatekeleza kila jambo kwa wakati ambao utakuwa umefaa na kwa namna ambayo ni sahihi kabisa kwa wafanyakazi. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mollel, hitimisha hoja yako.

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nasikitishwa sana. Mimi nikiwa kama Katibu Mkuu Mstaafu wa Ofisi ya Rais, Utumishi nasikitika kuona Waheshimiwa Wabunge hawawezi kutofautisha kati ya huduma, maji na umeme, hivi nani wanafanya hizo kazi? Hao wanaozifanya hizo kazi ndiyo hao watumishi ambao hamuwapi *morale* wafanyakazi zao, watafanyaje kazi kwa

raha. *We are not investing on people*, lazima tu-invest kwa watu, tuwape *morale* wafanye kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *salary increment* ni haki kwa sababu *OPRAS* haifanyi kazi Mheshimiwa Mkuchika. Mheshimiwa Mkuchika *OPRAS* bado haija-take off na tunatakiwa kuendelea kuwapa *increment* mpaka *OPRAS* itakapo-take off, haija-take off *OPRAS*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *salary adjustment* ya Mei ambayo ndiyo inasaidia kupunguza *inflation* haitoki, sasa hawa watafanyaje? Gazeti la Mwananchi limeonyesha sembe imepanda kutoka shilingi 900 mpaka shilingi 1,200 mahali pengine ile kilo tano imetoka shilingi 4,000 sijui mpaka shillingi 6,000 wataishije hawa watumishi kama hawaongezewi mishahara? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hoja hii iamuliwe na Bunge. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Kwa utaratibu wetu wa Kikanuni sasa nitawahoji.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja illiamuliwa na Kukataliwa*)

(*Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane. Kwa muda wetu uliobaki tutapitisha mafungu kwa jumla kwa mujibu wa Kanuni zetu zilivyo, Katibu.

NDG. MOSSY LUKUVI - KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya fedha zinazoombwa na Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora) yenye Mafungu nane ni shilingi 483,676,705,000.

Fungu 32- Menejimenti ya Utumishi wa Umma

Kif.1001 - <i>Administration and HR Management</i>	Sh.12,156,510,000/=
Kif.1002 - <i>Finance and Accounts Unit</i>	Sh.327,943,000/=
Kif.2003 - <i>Government Communication Unit</i>	Sh.184,900,000/=
Kif.1004 - <i>Procurement Management Unit</i>	Sh.206,118,000/=
Kif.1005 - <i>Internal Audit Unit</i>	Sh.228,111,000/=
Kif.1006 - <i>Planning Division</i>	Sh.369,835,000/=
Kif.1007 - <i>Legal Service Unit</i>	Sh.113,416,000/=
Kif.2001 - <i>Policy Development Division</i>	Sh.510,181,905/=
Kif.2002 - <i>Management Service Division</i>	Sh.574,355,000/=
Kif.2003 - <i>Establishment Division</i>	Sh.735,755,000/=
Kif.2004 - <i>Ethics Promotion Division</i>	Sh.372,456,000/=
Kif.2005 - <i>Human Capital Management Division</i>	Sh.1,173,043,067/=
Kif.2006 - <i>Performance Contracting</i>	Sh.362,068,000/=
Kif.3001- <i>Human Resources Development Division</i>	Sh.5,997,003,000/=
Kif.3004 - <i>Remuneration and Staff Welfare Division</i>	Sh.106,490,000/=
Kif.4002 - <i>Management Information System</i>	Sh.8,094,136,551/=

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 04- Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa

Kif.1001 - <i>Administration and HR Management</i>	Sh.1,255,279,790/=
Kif.1002 - <i>Finance and Accounts Unit</i>	Sh.128,483,296/=
Kif.1003 - <i>Planning, Monitoring and Evaluation Unit</i>	Sh.99,361,355/=
Kif.1004 - <i>Information and Communication Technology</i>	Sh.137,145,540/=
Kif.1005 - <i>Legal Service Unit</i>	Sh.35,620,000/=
Kif.1006- <i>Internal Audit Unit</i>	Sh.101,620,000/=
Kif.1107 - <i>Government Communication Unit</i> ..	Sh.26,020,000/=

Kif.1008 - *Procurement Management Unit*.....Sh.94,861,853/=
Kif.4001-*Archieve Management Division*.....Sh.232,463,130/=
Kif.4002 - *Records Management Division*....Sh. 321,816,618/=
Kif.4003 - *Records Center Division*.....Sh.228,133,126/=
Kif.4004 - *The Founders of the Nation Center
Division*.....Sh.113,261,292/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 09 – Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma

Kif. 1001 – *Administration and HR Mgt*.....Sh.662,490,342/=
Kif. 1002 – *Finance and Accounts Unit*Sh.113,358,000/=
Kif. 1003 – *Planning Unit*Sh.71,422,00/=
Kif. 1004 – *Internal Audit Unit* Sh.13,100,000/=
Kif. 1005 – *Legal Services*Sh.141,610,000/=
Kif. 1006 – *Information and Comm. Techn.*.... Sh.36,368,000/=
Kif. 2001 – *Productivity and Research Unit*...Sh.343,576,458/=
Kif. 2002 – *Remunaration Unit*.....Sh.92,325,200/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 20 – Ofisi ya Rais, Ikulu

Kif. 1001 – *Administration and HR Mgt*.... Sh.23,144,913,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 30 –Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri

Kif. 1001 - *Administration And HR Mgt*.....Sh.404,574,560/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts*.....Sh.509,179,000/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning*Sh.531,396,000/=
Kif. 1004 - *Internal Audit Unit*Sh. 300,875,000/=
Kif. 1005 – *Info. & Comm. Tech. Unit*.....Sh. 292,970,000/=
Kif. 1006 – *Procurement Management Unit*...Sh.274,360,000/=

Kif. 2001 -Cabinet Secretariat	Sh.2,006,867,000/=
Kif. 2002 – Government Communication.....	Sh.370,970,000/=
Kif. 2003 – Good Governance	Sh.799,922,000/=
Kif. 2004 – Public Service Appeal	Sh.461,940,000/=
Kif. 2005 – Public Sector Reform Coordination Unit.....	Sh. 0

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 33- Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma

Kif.1001 - <i>Administration and HR Management</i>	Sh.1,742,590,736/=
Kif.1002 - <i>Finance and Accounts Unit</i>	Sh. 345,874,400/=
Kif. 1003 – <i>Planning, Monitoring & Evaluation Unit</i>	Sh. 233,171,500/=
Kif. 1004 – <i>Government Comm. Unit</i>	Sh.149,320,700/=
Kif. 1005 – <i>Procurement & Mgt. Unit</i>	Sh.132,600,000/=
Kif. 1006 – <i>Internal Audit</i>	Sh.200,328,000/=
Kif. 1007 – <i>Info. and Comm. Tech. Unit</i>	Sh.183,009,152/=
Kif. 1008 – <i>Legal Service Unit</i>	Sh.247,693,120/=
Kif. 2001 – <i>Public Service Leaders Division</i>	Sh.689,456,221/=
Kif. 2002 – <i>Public Leaders Ethics Promotion</i> ...Sh.472,149,393/=	
Kif. 2003 – <i>Zonal Offices</i>	Sh. 0
Kif. 2004 – <i>Zonal Office- Northern Zone</i>	Sh.325,691,900/=
Kif. 2005 – <i>Zonal Office- Southern Zone</i>	Sh.400,145,700/=
Kif. 2006 – <i>Zonal Office-Central Zone</i>	Sh.400,751,000/=
Kif. 2007 – <i>Zonal Office-Eastern</i>	Sh.289,116,200/=
Kif. 2008 – <i>Zonal Office-Southern Highlands</i> ..Sh.364,374,200/=	
Kif. 2009 – <i>Zonal Office-Lake Zone</i>	Sh.373,688,656/=
Kif. 2010 – <i>Zonal Office-Western Zone</i>	Sh.303,026,000/=
Kif. 2011 – <i>Zonal Office Dar es Salaam</i>	Sh.529,088,122/=

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 67 - Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma

Kif. 1001 – *Administration And HRM*.....Sh.968,514,000/=
Kif. 1002 – *Finance and Account*Sh.150,781,000/=
Kif. 1003 – *Planning, Monitoring & Evaluation*Sh.58,153,105/=
Kif. 1004 – *Government Comm. Unit*.....Sh.59,525,895/=
Kif. 1005 – *Legal Service Unit* Sh.67,062,000/=
Kif. 1006 – *Procurement Management Unit*....Sh.70,840,000/=
Kif. 1007 – *Mgt. Information System Unit*.....Sh.149,770,000/=
Kif. 1008 – *Internal Audit Unit*Sh.96,595,000/=
Kif. 2001 – *Recruitment Mgt Division*Sh.573,950,000/=
Kif. 2002 – *Quality Control*Sh.181,252,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 94 - Tume ya Utumishi wa Umma

Kif. 1001- *Administration & HR Mgt*.....Sh. 2,320,246,891/=
Kif. 1002 –*Finance and Accounts Unit* Sh.252,242,000/=
Kif. 1003 – *Planning, Monitoring & Evaluation Unit*.....Sh.323,878,000/=
Kif. 1004 – *Internal Audit Unit* Sh. 85,160,000/=
Kif. 1005 – *Procurement Management Unit*...Sh. 84,484,000/=
Kif. 1006 – *Legal Service Unit* Sh.75,992,000/=
Kif. 1007 – *Government Com. Unit*.....Sh.118,361,109/=
Kif. 1008 – *Info. Comm.Tech.Unit*Sh. 86,662,000/=
Kif. 1009 – *Guidelines Formulation, Dissemination and Research*.....Sh.284,650,000/=
Kif. 2001 – *Civil Service*.....Sh. 0
Kif. 2002 – *Local Government Service*Sh. 0
Kif. 2005 – *Health's Service*.....Sh. 0
Kif. 2006 – *Appeals and Complains Department*Sh.690,920,000/=
Kif. 2007 – *HR Standars and Compliance Department*.....Sh.576,010,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MIPANGO YA MAENDELEO

NDG. MOSSY LUKUVI - KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitabu cha Maendeleo, *Volume IV*, jumla ya fedha zinazoombwa katika mafungu yaliyo chini ya Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora) ambapo mafungu yaliyotengewa pesa ya maendeleo ni Fungu 32, 04, 30 na 33. Jumla ya Fedha zinazoombwa katika Mafungu haya ni Sh. 199,867,255,617.

Fungu 04 - Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa

Kif. 1001- <i>Administration and HRM</i>	Sh. 0
Kif. 1003 – <i>Planning, Monitoring & Evaluation</i>	Sh. 0
Kif. 4001 – <i>Archieve Management Division</i>	Sh.1,500,000,000/=
Kif. 4002 – <i>records Management Division</i>	Sh.500,000,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 30 – Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri

Kif. 1003 – <i>Police And Planning</i>	Sh.154,189,384,717/=
--	----------------------

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 32 – Menejimenti ya Utumishi wa Umma

Kif. 1001 – <i>Administration & HRM</i>	Sh.500,000,000/=
Kif. 1006 – <i>Planning Division</i>	Sh.16,212,000,000/=
Kif. 4002 – <i>Mgt. Info. System Division</i>	Sh. 24,348,000,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 33 – Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma

Kif. 1001 – *Administration and HRM*.....Sh. 200,000,000/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts*.....Sh.32,160,000/=
Kif. 1003 – *Planning, Monitoring & Evaluation*.....Sh.328,295,000/=
Kif. 1004 - *Government Communication*.....Sh.219,805,000/=
Kif. 1007 – *Information and Comm. Tech. Unit* Sh.399,302,200/=
Kif. 1008 –*Legal Service Unit*.....Sh.12,380,000/=
Kif. 2001 – *Public Service Leaders Division*.....Sh.486,296,100/=
Kif. 2002 – *Public Leaders Ethics Promotion Division*.....Sh.240,375,000/=
Kif. 2003 – *Zonal Offices*.....Sh. 0
Kif. 2004 – *Zonal Office-Northern Zone*.....Sh.89,660,000/=
Kif. 2005 – *Zonal-Southern Zone*.....Sh.106,480,200/=
Kif. 2006 – *Zonal Office- Central Zonal* Sh.97,648,200/=
Kif. 2007 – *Zonal Office- Eastern Zone*Sh.123,230,200/=
Kif. 2008 – *Zonal Office-Southern Highland*.....Sh.89,719,000/=
Kif. 2009 – *Zonal Office-Lake Zone*..... Sh.89,660,000/=
Kif. 2010 – *Zonal Office- Western Zone*..... Sh.89,660,000/=
Kif. 2011 – *Zonal Office – Dar es Salaam*.....Sh.13,200,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Bunge lilitrudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mtoa hoja, taarifa.

T A A R I F A

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 104(3)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi zake zote. Hivyo, naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.
(Makofi)

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono na kwa utaratibu wetu sasa nitawahoju juu ya hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora) kuhusu mapato na matumizi ya ofisi yake kwa mwaka 2019/2020.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba yenu wote tumpongeze Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, (Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora) kwa usikivu wa yale yote ambayo Waheshimiwa Wabunge waliyasema kuanzia kwenye ngazi ya Kamati na hata ushauri uliotolewa hapa Bungeni. Kwa hiyo, tunawatakania kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yenu kwa yale ambayo mmeliahidhi Bunge kwamba mnakwenda kufanya kazi kwa fedha zile ambazo Bunge limeidhinisha. Tunawatakania kila la kheri na tunaamini mtakwenda kufanya kazi kwa weledi kama ambavyo mmekuwa mkifanya na pengine mkaongeze zaidi. Yale ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyalalamikia kwa upande wa Utumishi naamini mtayafanya kazi ili wananchi waweze kuhudumiwa vizuri na Wizara hii muhimu sana ambayo ndiyo inayotufanya sote tuwepo.

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na hayo, nimeletewa sasa takwimu ili Taarifa zetu Rasmi za Bunge zikae vizuri. Taarifa zilizopo kwa upande wa mimba kwa mwaka 2017, wanafunzi wote walioacha shule upande wa shule za msingi kwa nchi nzima ni 66,142 ambayo ni asilimia 1.6 ya wanafunzi wote na waliacha kwa sababu mbalimbali siyo mimba pekee. Kwa hiyo, hawa 66,142 waliacha shule kwa sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na utoro ambaao ndiyo unaoongoza, utoro peke yake uko asilimia 94. Katika hawa walioacha shule wavulana ni 34,746 kwenye utoro na wasichana ni 27,395. Kwa maana hiyo ukizungumza kuhusu wale walioacha shule kwa sababu ya mimba asilimia inakuwa ni 1.6 ya wanafunzi wote.

Waheshimiwa Wabunge, upande wa shule za sekondari wanafunzi walioacha shule kwa sababu ya mlimba ni 5,443 na hawa ni asilimia 8.3 kati ya wanafunzi 65,700 ambaao waliacha shule kwa sababu mbalimbali. Kwa hiyo, ukiangalia idadi maana yake ni kwamba mimba ni sehemu tu ya hizo changamoto nyngine siyo kwamba peke yake ndiyo imebeba idadi ile aliyokuwa ameitaja Mheshimiwa Mbatia. Hata hivyo, ukiangalia hizi takwimu, haiwezekani Mkoa mmoja ukawa na 70,000 kama nchi nzima ina 65,700. Kwa hiyo, zile takwimu hazikuwa sawasawa na wenzetu watunza Kumbukumbu za Bunge waweke taarifa hii vizuri. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tumalize na jambo ambalo lilitokea leo asubuhi. Mheshimiwa Mnyika aliletta hoja hapa kuhusu Haki za Bunge na wote tunafahamu Kanuni zetu zinasemaje jambo hilo na mimi niliahidi kwamba kwa kuwa hatujalisoma gazeti tutalifuatilia tulisome ili tuweze kutoa utaratibu wa jambo hili tutalimaliza kwa namna gani.

Waheshimiwa Wabunge, mnamo tarehe 15 Aprili, 2019 katika Kikao cha Kumi cha Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge la Bajeti unaoendelea, Mheshimiwa John John Mnyika alisimama na kuomba nafasi ya kueleza kuwa anayo hoja kuhusu Haki za Bunge ambayo anaamini imevunjwa.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kuwa nililifahamisha Bunge kuwa nikiwa Mezani nililetewa taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mnyika ya kusudio lake la kuwasilisha Hoja kuhusu Haki za Bunge. Taarifa hiyo ya hoja haikuwa imewasilishwa mapema kama Kanuni zetu zinavyotaka na pia haikuwa na muhuri wa Katibu wa Bunge.

Hata hivyo, kutokana na umuhimu wa kudumisha Haki za Bunge, niliona ni vyema nimpe nafasi ili aelete msingi wa hoja yake ili kuniwezesha kujua jambo lenyewe ipasavyo na kutoa uamuzi.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mnyika alitumia wasaa huo kueleza kuwa Gazeti la Fahari Yetu limeandika katika ukurasa wa mbele wa gazeti kile ambacho kimesomeka kama 'Bunge Iamtupa Rasmi CAG, Iamtaka akajieleze kwa Rais Dkt. Magufuli. Mheshimiwa Mnyika aliendelea kueleza kuwa hakuna uamuzi wowote ambao Bunge hili limeufanya kwa kumtupa *CAG* wala wa kumtaka *CAG* kwenda kujieleza kwa Rais Magufuli. Alifafanua zaidi kuwa kupitia Azimio la Bunge, Bunge liliamua kutofanya kazi na Profesa Assad.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hapo alihoji kitendo cha Gazeti la Fahari Yetu kuandika kwamba Bunge lilitupa rasmi *CAG* iwapo si kitendo cha kuingilia Haki za Bunge. Halikadhalika alihoji kitendo cha gazeti hilo kuandika kuwa Bunge limefanya uamuzi wa kutaka *CAG* akajieleze kwa Mheshimiwa Rais kuwa huo ni uingiliaji wa Haki za Bunge kwa kuzingatia kuwa Bunge halikuamua hivyo.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mnyika alienda mbali zaidi alitaka kutoa hoja kwamba suala hilo lijadiliwe kwa kuwa limegusa haki za Bunge ili maelezo hayo yatupiliwe mbali na Bunge lipewe haki ya kufanya kazi kama inavyotakiwa. Nikitoa ufanuzi kuwa kabla ya kuunga mkono hoja yake ni vyema kulisoma gazeti lilitolalamikiwa na kuwa iwapo itathibitika kuwa ni kweli basi hatua za kawaida kwa chombo au kwa mtu anayeingilia haki na hadhi ya Bunge zitachukuliwa. Nimelitafuta gazeti hilo na kulisoma.

Waheshimiwa Wabunge, kutokana na taarifa na maelezo ya Mheshimiwa Mnyika, yapo mambo mawili makubwa ambayo inhabidi niyatolee uamuzi. Jambo la kwanza ni je, taarifa ya Mheshimiwa Mnyika imezingatia masharti ya Kanuni za Bunge? Pili, ni je, Gazeti la Fahari Yetu Tolea Na.118 la Jumatatu tarehe 15 Aprili, 2019 limekiuka na kuingilia haki na kinga za Bunge?

Waheshimiwa Wabunge, hoja kuhusu Haki za Bunge na utaratibu wake wa kuiwalisha umewekwa chini ya Kanuni ya 51(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kanuni hiyo inamtaka Mbunge anayetaka kuwasilisha hoja kuhusu Haki za Bunge kumtaarifu Spika mapema kuhusu kusudio hilo akitaja jambo analolitaka kuliombea mwongozo huo. Kanuni inayohusika nainukuu, Kanuni ya 51(1), inasema: "Mbunge anayetaka kuwasilisha jambo ambalo anaamini linahusiana na haki za Bunge atafanya hivyo wakati unaofaa kufuatana na mpangilio wa shughuli za Bunge uliowekwa na Kanuni hizi na atakuwa amemuarifu Spika mapema kuhusu kusudio lake hilo na jambo ambalo anataka kuliwasilisha."

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni hii inamtaka Mbunge anayetaka kuwasilisha hoja ya Haki za Bunge kumuarifu Spika na kueleza jambo analotaka kuliwasilisha mapema kwa lengo la kumwezsha Spika kufahamu msingi wa hoja na kuona kama hoja hiyo inafaa kupokelewa au haifai. Endapo itaonekana hoja hiyo inafaa Spika ataipa kipaumbele katika kupanga shughuli za Bunge katika kikao kinachohusika ili iwasilishwe.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyoeleza awali Mheshimiwa Mnyika hakumtaarifu Spika mapema kuhusu kusudio lake hilo na wala taarifa yake haikugongwa muhuri wa Katibu wa Bunge kuthibitisha kupokelewa. Kwa hali hiyo, ni wazi kuwa taarifa ya hoja ya Mheshimiwa Mnyika ilikiuka masharti ya Kanuni ya 51(1) kwa kutowasilishwa mapema kama ilivyotakiwa. Mapungufu hayo yanaifanya taarifa yake kutokukubalika kikanuni japokuwa alipewa fursa na kitu kwa kuzingatia kwamba ni muhimu kulinda hadhi ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu suala kama gazeti hilo limeingilia uhuru wa Bunge, nimelazimika kusoma Gazeti la Fahari Yetu, Toleo Na.118 la tarehe 15 Aprili, 2019 lenye kichwa cha habari, 'Bunge lamtupa CAG, lamtaka akajieleze kwa Rais Dkt. Magufuli, lakazia msimamo wa kutokufanya naye kazi'. Kimsingi kwa namna nilivyoona Fahari Yetu sawa na magazeti mengi mengine nchini yaliyochapishwa tarehe 5 Aprili, 2019 yamerejea na kufafanua kuhusu Azimio la Bunge la tarehe 2 Aprili, 2019 kuhusu uamuzi uliofikiwa na Bunge wa kutokufanya kazi na Profesa Mussa Assad kutokana na kitendo chake cha kulidharau, kulidhalilisha na kushusha heshima ya Bunge. Maelezo hayo kwenye gazeti hayajaingilia kwa vyovoyote vile haki na madaraka ya Bunge kama Mheshimiwa Mnyika alivyoamini.

Waheshimiwa Wabunge, haki na kinga za Bunge zimetajwa katika Ibara ya 100 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na pia katika kifungu cha 3 cha Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge, Sura ya 296. Bunge hili linao uhuru wa mawazo, majadiliano na lina madaraka ya kutoa uamuzi. Uhuru huo wa Bunge hautahojiwa na mtu ye yeyote au chombo chochote nje ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, endapo ingethibitika kuwa gazeti linalolalamikiwa limeingilia haki na madaraka ya Bunge, watusika wangeflikishwa kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuchunguzwa kwa mujibu wa Kanuni ya 4(1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2016. Huu ndio utaratibu ambao Bunge hili limekuwa likiuzingatia kwa chombo au mtu ye yeyote anayeingilia haki, kinga na madaraka ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, napenda kuhitimisha kwa kueleza kuwa Azimio la Bunge kuhusu suala la CAG linaeleweka. Kwa mujibu wa Kanuni ya 54(4) na 64(1)(c) ya Kanuni za Bunge halipaswi kuendelea kuibuka humu Bungeni kwa namna yoyote ile kutaka lijadiliwe isipokuwa kwa hoja mahsus. Aidha, hoja dhidi ya haki na madaraka ya Bunge dhidi ya Gazeti la Fahari Yetu hajathibitika na kwa kuwa hoja

yenye we haikuja kikanuni, Bunge haliwezi kuipa hoja hiyo nafasi.

Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo mwongozo wangu kuhusu jambo hili ambalo lilitokea mapema leo.
(Makof)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.27 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne,
Tarehe 16 Aprili, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*